Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

**Kikao cha Pili - Tarehe 4 Februari, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HAZI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Bodi ya Kahawa kwa Mwaka Ulioishia Tarehe 30 Septemba, 2002 *(The Annual Report and Accounts of the Tanzania Coffee Board (TCB) for the year ended 30th September, 2002).*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 16

**Matumizi ya Jina la Baba wa Taifa**

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA** aliuliza: -

Kwa kuwa Mwasisi wa Taifa letu Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alipoaga dunia alituachia Watanzania wote hazina kubwa ya mawazo, maelekezo na wosia kuhusiana na jinsi ya kuendesha Jamhuri yetu na kwa kuwa baada ya kifo chake Taasisi mbalimbali kama shule, barabara, mitaa na kadhalika zimechukua jina lake kwa nia ya kuvipatia vyombo hivi umaarufu, kuvutia biashara au kumkumbuka tu.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwepo kwa chombo kitachopewa jukumu la kuratibu, kukubali na kukataa matumizi ya jina hilo ili kuondokana na utitiri uliopo wa matumizi ya jina la Baba wa Taifa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Prof. David H. Mwakyusa, Mbunge wa Rungwe Magharibi, kama ifuatavyo: -

Kwanza, nakubaliana kabisa na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge. Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine itaangalia uwezekano wa namna nzuri ya kutekeleza ushauri uliotolewa na Mheshimiwa Mwakyusa.

Na. 17

**Mchango wa Halmashauri za Wilaya**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza: -

Kwa kuwa Halmashauri za Wilaya zinatakiwa kuchangia asilimia 10 ya mapato yake kwa ajili ya Mfuko wa Mikopo ya Maendeleo ya Wanawake na Vijana: -

(a) Je, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2001 hadi Julai, 2003 ni Wilaya ngapi zimetimiza agizo hilo kikamilifu na ni kwa kiasi gani kwa kila Halmashauri?

(b) Je, ni Halmashauri zipi ambazo hazikutimiza agizo hilo kwa kipindi hicho hicho na zinadaiwa kiasi gani?

(c) Je, Serikali inasema nini juu ya madeni ya Halmashauri hizo ili kutimiza azma ya kusaidia maendeleo ya makundi yaliyokusudiwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, tangu Mfuko wa Mikopo kwa Wanawake na Vijana ulipoanzishwa mwaka 1995, maendeleo ya Mfuko huu yamekuwa si ya kuridhisha kutokana na sababu mbalimbali kama vile kutokuwepo kwa utaratibu mzuri na endelevu wa uendeshaji wa Mfuko, utaratibu mbovu wa utoaji mikopo kwa walengwa, wakopaji kutorejesha mikopo na ushauri wa kitaalam kutokidhi mahitaji ya walengwa wa Mfuko. Aidha, hali mbaya ya ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri kutokana na vyanzo vyake pamoja na Halmashauri kuwa na majukumu mengine ya kuleta maendeleo kwa jamii, imechangia kwa kiasi kikubwa kutofikiwa kwa malengo ya Mfuko.

Mheshimiwa Spika, kutokana na sababu nilizozieleza hapo juu, Halmashauri karibu zote hazijaweza kufikia lengo la kutenga asilimia 10 ya mapato yake kwa ajili ya Mfuko huu tangu ulipoanzishwa. Kwa mfano, kwa kipindi cha mwaka 1996 - 2000, Halmashauri ziliweza kuchangia Sh.2,755,645,575/= tu ikilinganishwa na makadirio ya jumla ya Sh.9,776,737,717/= zitokanazo na asilimia 10 ya fedha kutoka vyanzo vya mapato yake ambazo ni sawa na asilimia 28 ya makadirio ya fedha zilizohitajika kutolewa. Aidha, kutokana na taarifa za jumla tulizonazo, Halmashauri nyingi hazikuweza kufikia lengo la kutenga asilimia 10 ya mapato yake kwa ajili ya Mfuko huu hata kwa kipindi anachoulizia Mheshimiwa Mbunge cha 2001 - 2003. Hata hivyo, ili kuwawezesheni Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla kuweza kuwa na picha kamili juu ya suala hili, Ofisi yangu inaandaa taarifa kamili kuhusu utekelezaji wa Mfuko huu tangu uanzishwe na itakapokamilika tutaiwasilisha kwa Waheshimiwa Wabunge.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu la (a) hapo juu, kwa sasa ofisi yangu inakamilisha taarifa kuhusu hali ya uchangiaji wa Halmashauri zote hapa nchini ambayo pamoja na mambo mengine itaonyesha Halmashauri zinazodaiwa kutokana na kushindwa kuchangia hiyo asilimia 10 ya mapato yao. Baada ya hapo tutazifanyia uchambuzi na kama nilivyosema tutawasilisha kwa Waheshimiwa Wabunge.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kusisitiza umuhimu wa kuwepo Mfuko huu wa mikopo kusaidia maendeleo ya Wanawake na Vijana. Ofisi yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Wizara za Viwanda na Biashara na Mashirika yasiyo ya Kiserikali, inachukua hatua mbalimbali za kuutazama tena Mfuko huu ili uweze kuwa endelevu na wenye manufaa kwa walengwa.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri. Pamoja na hayo, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa lengo la kuanzishwa kwa Mfuko huu ilikuwa ni kukidhi haja ya lengo la kuondoa umaskini na mkakati mmojawapo ulikuwa ndiyo huu wa utekelezaji wa kuanzisha Mfuko huu. Je, kwa kuwa lengo hilo halijatimizwa sasa, Serikali haioni haja ya kufikiria mpango mwingine ambao utawezesha Halmashauri kuwa na uwezo wa kuendeleza Mfuko huu kama ilivyokusudiwa?

(b) Kwa kuwa Halmashauri zimekuwa zikipata mapato japokuwa ni kidogo na kwa kuwa sheria ilikuwa inawataka watenge asilimia ya mapato hayo japokuwa ni madogo. Je, ni kwa nini Halmashauri hizo hazikutenga na ni kwa nini tumenyamaza kimya bila kuzikumbusha na kuzishauri Halmashauri hizo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mntangi kwamba, lengo kubwa la Mfuko huu ilikuwa ni kusaidia kupambana na hali ya umaskini katika makundi hayo mawili na ni dhahiri kabisa kutokana na maelezo niliyoyatoa hatujaweza kufikia kiwango hicho kinachotakiwa.

Kuhusu kwamba tufanye nini, tunaloweza kusema kama Serikali ni kwamba, juhudi ambazo sasa Serikali inafanya ni kujaribu kuutazama Mfuko huu tena ili uweze kuwa na misingi ya kuweza kujiendesha wenyewe na unaweza ukasaidia kwa kiasi kikubwa sana. Lakini pili, uamuzi wa Serikali wa hivi karibuni wa kutoa ruzuku kwa vyombo hivi, tunaamini vile vile kwamba utasaidia kwa kiasi kikubwa kuweza kujibu baadhi ya hoja ambazo zinauzunguka Mfuko huu kwa hivi sasa.

Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kuhusu Halmashauri hizi si kwamba tumenyamaza, tunaendelea kwa juhudi kubwa sana kuzibana kwa kadri inavyowezekana ili ziweze kuendelea kuchangia Mfuko huu. Lakini naomba niseme tu kwamba, majukumu ya Halmashauri zetu kwa ujumla ni mengi na hata makato haya ya kisheria ni mengi. Kwa hiyo, katika hali kama hiyo ndiyo maana naona inakuwa wakati mwingine si rahisi sana kuweza kukidhi haja ambayo kwa sasa wote tunatamani ingetekelezwa.

Na. 18

**Pikipiki za Makatibu Tarafa**

**MHE. PASCHAL C. DEGERA** aliuliza: -

Kwa kuwa Tarafa ya Kwamtoro Wilayani Kondoa haijapatiwa mgao wake wa pikipiki zilizogawiwa na Serikali hivi karibuni kwa Makatibu Tarafa: -

(a) Je, ni kwa nini Tarafa hiyo haikupata mgao wa pikipiki hizo mpya?

(b) Je, ni lini sasa Tarafa hiyo itapatiwa pikipiki hiyo?

(c) Je, Serikali haioni kwamba kuendelea kuchelewesha mgao wa pikipiki hizo kunachangia kuzorota kwa maendeleo ya Tarafa hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2001/2002 Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya kuwanunulia Makatibu Tarafa pikipiki zipatazo 512 ambazo ziliagizwa kutoka Japan na zote

zimeshagawiwa kwenye Mikoa 21 ya Tanzania Bara. Wakati makisio ya awali yanafanywa kwa ajili ya kununua pikipiki hizo, Tanzania Bara ilikuwa na Tarafa 512 tu. Wakati utaratibu wa kuagizwa pikipiki hizo unaendelea zilianzishwa Tarafa nyingine ambazo zilikuwa haziko kwenye makisio. Hivyo, wakati wa kuja kuchukua pikipiki Mikoa ilitakiwa kuja na orodha halisi ya Tarafa kama ilivyokuwa imeagizwa hapo awali. Kutokana na hali hii, wakati wa kuchukua pikipiki Mkoa wa Dodoma ukakosa pikipiki moja kwa kuwa baadhi ya Mikoa ilikuja na orodha ambayo ilikuwa ni kubwa kuliko idadi iliyokuwa inafahamika hapo awali.

(b) Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, inalifahamu tatizo la pikipiki kwa ajili ya Katibu Tarafa huyo na imekwishamwagiza Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma kwa barua Kumb. Na. CAB/30/154 01/72 ya tarehe 06 Novemba, 2003 ili aweke kwenye bajeti yake ununuzi wa pikipiki kwa Katibu Tarafa huyo.

(d) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu (a), mgao wa pikipiki ulikwishafanyika isipokuwa kwa Tarafa zile ambazo hazikupata kutokana na kuanzishwa upya au taarifa za Mkoa za idadi ya Tarafa kutokuwa sahihi. Hivyo, kwa Tarafa zilizoathirika napenda kutoa wito kwa Uongozi wa Halmashauri na Mikoa, ziwasaidie Makatibu Tarafa hao ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo wakati hatua zinachukuliwa na Mikoa husika za kuwapatia vyombo vya usafiri.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza, pia namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

(a) Kwa kuwa Tarafa ya Kwamtoro si Tarafa mpya, walitumia vigezo gani kufanya Tarafa ya Kwamtoro ambayo ni Tarafa ya zamani kukosa haki yake ya kupata pikipiki?

(b) Kwa kuwa katika uchambuzi wa Bajeti ya TAMISEMI kupitia Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Waziri aliahidi kwamba Wizara ingetenga fedha za kununua pikipiki katika Bajeti hii ya 2003/2004 ni kwa nini sasa katika jibu naambiwa kwamba *RAS* ndiyo atenge pesa hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika maelezo ni kwamba, baadhi ya Mikoa ilipokuja kuchukua hizo pikipiki, ilikuwa tayari imekwishapata Tarafa za ziada na ilichukua pikipiki zaidi kwa maana ya idadi ya awali ya Tarafa zilizokuwepo na matokeo yake ni kwamba, Kwamtoro ikakosa pikipiki kwa sababu pikipiki hiyo ilikwenda kwenye Mkoa mwingine. Sasa, matatizo haya ni ya kiutekelezaji, lakini kama nilivyosema, tuna uhakika jambo hili litasahihishwa baada ya muda si mrefu.

Ni kweli kwamba, sasa tunauagiza Mkoa uweze kuweka katika bajeti yake na sababu yake kubwa ni kwamba, wakati tunaagiza zile pikipiki 512 tuliamua hivyo kwa sababu ulikuwa ni mpango maalum na mkubwa na ulihitaji fedha nyingi. Hii ni pikipiki moja ndiyo maana tunasema *RAS* ashughulikie, *in any case*, bado mtoaji ni Waziri wa Fedha yule yule. Kwa hiyo, haina tofauti sana.

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa hata Makatibu Tarafa waliopata pikipiki hawazitumii kikamilifu kwa sababu ya ukosefu wa mafuta. Je, isingekuwa vyema gharama za mafuta zikaingizwa kwenye mishahara yao moja kwa moja badala ya kusubiri hisani ya Mkuu wa Wilaya kuwapatia mafuta? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, utaratibu ulivyo sasa ndiyo huo ambao bahati nzuri Profesa Mwaga ameutaja kwamba, wanapata mafuta kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ambayo ndiyo yanawawezesha kuweza kutoa huduma inayohitajika.

Ni kweli ushauri alioutoa kuingiza fedha hizi moja kwa moja kwenye mshahara wake pengine unaweza ukaonekana ni ushauri mzuri, lakini katika kulitafakari katika utekelezaji inawezekana kabisa fedha hizi zisitumike vile vile kwa lengo lililokubalika.

Mheshimiwa Spika, tunachokitambua sasa ni kwamba, fedha hiyo ni ndogo na ndiyo jambo ambalo tunajaribu kulifanyia kazi ili wawe na kiwango cha kuweza kutosheleza kuweza kutoa huduma inayohitajika. Kwa sasa wengi wanawapa lita 10 kwa mwezi, kwa hiyo, ni kiasi kidogo sana. Lakini tunalishughulikia na tunaamini tutafaulu kuliweka vizuri.

Na. 19

**_TANESCO_ Kukata Umeme Zanzibar**

**MHE. SIJAMINI MOHAMED SHAAME** aliuliza: -

Kwa kuwa majukumu makubwa ya Shirika la Ugavi wa Umeme *(TANESCO)* na Shirika la Umeme Zanzibar ni kupeleka umeme wenye uhakika Zanzibar na kwamba ni imani ya Watanzania wote kuona vyombo hivyo vinafanya kazi kwa uelewano: -

(a) Je, Serikali haioni kuwa kitendo cha kukata umeme Zanzibar kimeleta dosari na hasa kwa wakati huu ambapo nguvu ya kuwepo kwa Muungano imara ni muhimu?

(b) Je, Serikali ya Muungano haikuona umuhimu wa kuitaarifu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kabla ya kuchukua hatua hiyo?

(c) Je, Serikali haikuona njia nyingine ya busara ambayo ingelifaa zaidi kuliko kitendo cha kuikatia umeme Zanzibar ambayo ni sehemu muhimu kwa uhai wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sijamini Mohamed Shaame, Mbunge wa Kitope, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* inaiuzia umeme Shirika la Umeme na Mafuta Zanzibar, ambalo kwa upande wake nalo linatoa huduma ya umeme kwa Wananchi wa Zanzibar ikiwemo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kama ilivyoelezwa kwa kirefu Bungeni wakati wa Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nishati na Madini, mkataba kati ya *TANESCO* na Shirika la Umeme na Mafuta Zanzibar ni mkataba wa kibiashara.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, tangu *TANESCO* kuikatia umeme Shirika la Umeme na Mafuta Zanzibar, pamekuwa na mikutano kadhaa kati ya Mashirika hayo na kati ya Wizara za Nishati na Madini za Muungano na Zanzibar ili kuhakikisha kuwa kila Shirika linatimiza wajibu wake na hivyo kuzuia kabisa kutokea tena kwa kukatiwa umeme Shirika la Mafuta na Umeme Zanzibar.

**MHE. MOHAMED ABDULLY ALLY:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza, nachukua nafasi hii kuwapongeza wote wanaohusika kutuhakikishia kwamba umeme hautakatwa tena kule Zanzibar.

Kwa kuwa katika upelekaji wa umeme kule kisiwani Zanzibar kuna umeme unaopotea njiani, je, Wizara inayohusika imeshafikiria ni nani ana jukumu la kulipa hasara hiyo inayotokea?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, suala la upotevu wa umeme linatokana na matatizo ya kiufundi na si kwa njia ya kupeleka umeme Zanzibar tu, lakini pia kwa umeme ambao unasambazwa sehemu mbalimbali huku Tanzania Bara. *TANESCO* kwa upande wake inachukua hatua mbalimbali katika kurekebisha mitambo na kurekebisha njia za umeme kupunguza upotevu wa umeme. Zanzibar wanacholipa kutokana na mkataba wa kibiashara ni ule umeme unaowafikia.

Na. 20

**Mahitaji ya Umeme Kuwezesha Wachimbaji wa *Nickel* na *Cobalt* - NGARA**

**MHE. GWASSA A. SEBABILI** aliuliza: -

Kwa kuwa kwa kipindi cha miaka 40 sasa Serikali imekuwa ikitoa majibu yasiyoridhisha juu ya suala la uchimbaji wa *Nickel* huko Ngara kwa kisingizio cha kwamba uchunguzi bado unafanyika; na kwa kuwa kilio cha wana Ngara na Mkoa wa Kagera kwa ujumla kwa Serikali ni kupeleka umeme kwenye migodi ya *Nickel,* kujenga barabara/reli ili kusafirisha madini hayo ya thamani kubwa; na kwa kuwa Kamishna wa Madini katika Semina ya Wabunge iliyofanyika tarehe 8 Novemba, 2003 akijibu hoja ya Mbunge wa Ngara alisema kwamba ukosefu wa umeme ndiyo unaosababisha ugumu wa kuchimba madini hayo na vile vile Mbunge husika alipotembelea Mdogi wa *Kabanga Nickel Mine Company* hapo tarehe 20 Septemba, 2003 aliambiwa kuwa madini yaliyopo ni mengi sana na ili yaweze kuchimbwa unahitajika umeme wa uhakika wa gridi ya Taifa na miundombinu ya usafirishaji wa madini hayo pamoja na mazao ya kilimo na mifugo: -

(a) Kulingana na matukio ya tarehe 8 Novemba, 2003 na 20 Septemba, 2003 kwenye swali hili; je, Serikali sasa itaondoa kigugumizi cha kutopeleka umeme Ngara na badala yake kupeleka umeme wa kuaminika mara moja na kuhakikisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji ili madini hayo yaanze kuchimbwa na kutoa ajira kwa vijana wetu?

(b) Kama Serikali inafahamu kwamba nchi yetu inao utajiri mkubwa sana wa madini hayo, ambayo yanapatikana kidogo sana nchini Urusi na Afrika ya Kusini; je, ni kitu gani kinachoifanya Serikali isifanye kila njia ili kuyachimba madini hayo ambayo yanahitajika sana ulimwenguni kutokana na umuhimu na uchache wake duniani?

(c) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba wawekezaji na wahisani wanashindwa kuwekeza katika Mikoa ya Kagera hususan kwenye migodi na Mkoa wa Kigoma wenye utajiri mwingi wa mazao ya mifugo, kilimo na utalii, kutokana na kukosekana kwa umeme miundombinu mbalimbali hivyo Serikali ipange maendeleo kuifikia Mikoa hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gwassa A. Sebabili, Mbunge wa Ngara, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Uchunguzi *(Exploration)* wa madini ya *Nickel* unaofanywa na Kampuni ya *Barrick Gold Corporation* bado haujakamilika. Kabla ya mwekezaji kufanya uamuzi wa kujenga mgodi, hapana budi ajiridhishe pamoja na mambo mengine na wingi wa madini, namna bora ya uzalishaji *(Processing)* na usafirishaji.

Pamoja na kwamba Ngara hakuna umeme wa gridi ya Taifa, wawekezaji watakapofikia hatua ya kutaka kuanza kuchimba madini haya ya *Nickel,* wataweza kuangalia uwezekano wa kuingia mkataba na *TANESCO* wa kujenga njia ya umeme hadi eneo la mgodi kama ilivyofanyika kwa mgodi wa Bulyanhulu. Kwa sasa, kama hatua za muda mfupi *(Short Term Measures)*, Serikali kupitia *TANESCO* inatekeleza mradi wa kupeleka umeme wa dizeli Ngara. Jengo la Kangavuke *(generator)* limekwishakamilika. Kangavuke lenyewe limekwishasafirishwa kutoka Babati hadi Ngara na kazi za kufunga mashine hizo zimeanza. Vile vile, kazi za ujenzi wa laini ya kusambaza umeme Mjini Ngara inaendelea.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuyachimba madini tuliyonayo. Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya sera, Serikali imejitoa katika kuwekeza moja kwa moja katika uchimbaji wa madini, badala yake inajenga mazingira mazuri kwa wawekezaji binafsi yanayoruhusu pamoja na mambo mengine, masuala ya kodi na vivutio, sheria na ujenzi wa miundombinu kulingana na uwezo. Kwa kuwa kiwango cha uwekezaji katika mgodi kama wa *Nickel* ni kikubwa, mwekezaji analazimika kufanya uchunguzi wa kina ili kuepuka kupata hasara.

(c) Mheshimiwa Spika, tunakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, masuala ya umeme na uendelezaji wa miundombinu mbalimbali ni mambo ya msingi katika kuwavutia wawekezaji na Wahisani katika Mikoa ya Kagera na Kigoma. Aidha, Serikali inafanya mazungumzo na uongozi wa *Geita Gold Mine* ili wajenge laini ya msongo 220 toka Kahama hadi Geita na ujenzi wa kituo cha kupoozea umeme ili pia kutoa fursa ya kuendeleza umeme wa gridi hadi Kagera ili kuupatia Mkoa huo umeme wa gridi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kigoma, kama ambavyo Serikali imetoa taarifa Bungeni mara nyingi wakati wa kujibu maswali, Serikali ipo katika mazungumzo na Serikali ya Sweden kupitia Shirika lake la Maendeleo la *SIDA* ili laini ya Tabora hadi Urambo iwe ya kiwango cha msongo 132 badala ya 33 iliyokubalika awali. Lengo kama ambavyo tumesema awali ni kutoa fursa kwa umeme wa gridi kupelekwa Kigoma. Wakati huo huo Serikali kupitia *TANESCO,* tayari imeagiza jenereta mpya kwa ajili ya Mji wa Kigoma ili kuondoa kero ya sasa ya ukosefu wa umeme.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika swali la msingi nimezungumzia kwamba, niliweza kufika katika eneo hilo tarehe 2 Septemba, 2003 na kukutana na Uongozi wa Kampuni hiyo. Bado nasimama pale pale kwamba ni miaka 40 ya uchunguzi, huo uchunguzi wa miaka 40 Bunge lako lingeweza kufahamu ni uchunguzi wa aina gani ambapo mtu aliyezaliwa wakati huo sasa amezeeka?

Mheshimiwa Spika, Uongozi wa Wilaya na Mkoa wamekwishafika pale, tatizo lao ni umeme na barabara ya kuweza kuchukua madini hayo kutoka pale yalipo kwenda yanapopelekwa. Naomba kufahamu, je, Mheshimiwa Waziri atakubali kuitembelea Kampuni hiyo na kuzungumza na Uongozi wa Kampuni hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni wajibu wetu kutembelea maeneo mbalimbali ya nchi ikiwa ni pamoja na eneo la mgodi huu au sehemu hii ambayo inafanyiwa utafiti wa *Nickel.* Kwa hiyo, pale itakapopatikana nafasi tutafanya hivyo. Lakini napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, suala la umeme endapo watafikia hatua ya kutaka kuchimba, upo uwezekano kabisa wa kuingia mazungumzo na *TANESCO* na kuhakikisha kwamba na wao pia wanachangia katika kufikisha umeme katika eneo husika na ndiyo utaratibu ambao umetumika katika migodi hii mingine mikubwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kwamba utafiti umechukua miaka 40, utafiti umefanywa katika hatua mbalimbali na Makampuni mbalimbali kama ambavyo tumewahi kujibu hapa Bungeni na umefanywa siyo kwa mfululizo kutokana na ukweli kwamba lile eneo liko mpakani na limekuwa ni eneo la wasiwasi kiusalama, pametokea matukio mbalimbali ya uvamizi wa eneo lile, hivyo, utafiti umekuwa ukifanyika na kuachwa na kufanyika tena na kuachwa. Lakini ni lazima hawa watu wanaofanya utafiti wajiridhishe kwamba watakapoanza kazi ya uchimbaji basi itafanyika kazi hiyo kwa faida.

**MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja tu la nyongeza na pia namshukuru mtunga swali. Kwanza, nimpongeze Waziri, Mheshimiwa Daniel Yona kwamba, amefika Kigoma na ameona hali halisi. Nampongeza kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yale matatizo aliyoyaona na ambayo Wananchi walimwambia sasa hivi wanataka yatekelezwe haraka iwezekanavyo. Kwa sababu katika jibu la msingi ...

**SPIKA:** Aah, uliza swali, uliza swali! *(Kicheko)*

**MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA:** Kwa sababu amesema kwamba kuna jenereta ambalo linazidi kuja huko na majenereta haya tumekuwa nayo ni mengi tu, tatizo bado ni lile lile. Je, huo umeme unaotoka Urambo kwenda Kigoma ukichukuliwa kwa miaka kama hiyo aliyoeleza Mheshimiwa

Sebabili (miaka 40), huoni kwamba tatizo ni kubwa kuliko lile ambalo ni la muda mrefu? Tunaomba umeme kuanzia leo na jibu liwe fupi zaidi. Hapo sasa! *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, kama ambavyo tumesema mara nyingi Bungeni, Serikali inatambua kero iliyopo Kigoma na ndiyo maana kama mwenyewe alivyokubali mpaka Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini amekwenda Kigoma kujionea mwenyewe. Ni muhimu ipatikane jenereta na jenereta hizi ni mpya, zitaweza kusaidia kuondoa tatizo la sasa kama ambavyo Mji wa Mtwara sasa hivi unaneemeka na jenereta mpya zilizonunuliwa na tayari zimeanza kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatujasema hapa kwamba suala la kupeleka umeme Kigoma litachukua miaka 40. Tumesema Serikali inafanya jitihada na pale fedha zitakapopatikana basi kazi hiyo itatimizwa. *(Makofi)*

Na. 21

**Utabiri wa Hali ya Hewa**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza: -

Kwa kuwa inafahamika kwamba utabiri wa hali ya hewa ni muhimu sana kwa shughuli mbalimbali za uchumi wa Kitaifa na Wananchi hasa wakulima, wavuvi na kadhalika; na kuwa lengo la utabiri ni kuwafikishia walengwa huko hali ya hewa katika kipindi husika ili waweze kuchukua tahadhari pale inapotarajiwa tukio la maafa, uhaba wa mvua, kimbunga, mafuriko, kuchafuka kwa hali ya hewa kwenye maziwa na bahari na kadhalika; na kwa kuwa huko nyuma Redio Tanzania ambayo inasikika maeneo yote hapa nchini na nje ya nchi ilikuwa inatangaza kipindi cha hali ya hewa lakini sasa hivi ni Vituo vya Televisheni tu vinatangaza kipindi hicho, ingawa televisheni hizo hazionekani nchi nzima na wanaoona na kusikia matangazo hayo ni watu wachache wenye uwezo wa kununua vyombo hivyo na ni wale wanaoishi Mijini: -

(a) Je, kwa nini Serikali haitangazi tena utabiri wa hali ya hewa kupitia Redio Tanzania?

(b) Je, Serikali haioni kwamba haiwatendei haki Wananchi wa Tanzania kwa kutotangaza hali ya hewa na ndiyo maana wanaathirika kwa ukame, mafuriko, vimbunga, mawimbi kwenye maziwa na bahari ambako kunaathiri shughuli za uvuvi na usafiri majini?

(c) Kwa kuwa jukumu la kutangaza hali ya hewa ni la Serikali, je, itakuwa tayari kuanza tena kutangaza hali ya hewa mara moja kupitia Redio ya Taifa?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgana I. Msindai Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Tangu kuundwa kwa Idara Kuu ya Hali ya Hewa kwa Sheria Na. 6 ya mwaka 1978, utabiri wa kila siku wa hali ya hewa na taarifa zote za hali ya hewa hupelekwa kwenye Vyombo vya Habari vya Serikali ikiwemo Redio Tanzania na magazeti ya *Daily News* na *Sunday News.* Utaratibu huu umekuwa ukiendelea hata baada ya kuanzishwa kwa Wakala za Serikali kuanzia mwaka 1999.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya kuundwa kwa Wakala za Serikali kama hii ya hali ya hewa ni kwa ajili ya kuhakikisha kwamba kazi zao zinafanyika kwa ufanisi na usahihi zaidi na pia ziweze kujiendesha zenyewe kwa kadri inavyowezekana kutokana na mapato yake zenyewe. Hata hivyo, pamoja na kutakiwa kujiendesha yenyewe, Mamlaka ya Hali ya Hewa, kwa kuzingatia kuwa ni Chombo cha Umma (Serikali) na umuhimu wa taarifa za hali ya hewa kuwafikia Wananchi, imeendelea kuandaa utabiri

wa hali ya hewa wa kila siku na wa misimu na kupeleka kwenye Vyombo vyote vya Habari vya Serikali ikiwemo Redio Tanzania ili kuwafikia Wananchi.

Mheshimiwa Spika, Redio Tanzania Dar es Salaam wametutaarifu kwamba wako tayari kutangaza taarifa za utabiri wa hali ya hewa katika kipindi cha majira au kinginecho watakachoona kinafaa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa utabiri wa hali ya hewa katika huduma za kiuchumi na kijamii, Wizara yangu imeiagiza Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania kujadiliana na *RTD* ili kuangalia uwezekano wa utekelezaji wa azma hiyo.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na kwa sababu inaonyesha dhahiri kwamba Redio Tanzania ilikwishaacha kutangaza habari za hali ya hewa na Wananchi wengi ...

**SPIKA:** Hatukusikii, weka *microphone* karibu zaidi.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na kwa kuwa imeonyesha dhahiri kwamba Redio Tanzania sasa itakuwa tayari kuanza kutangaza tena hali ya hewa kwa ajili ya faida ya Wananchi wetu: -

(a) Je, Serikali itahakikisha kwamba huo utangazaji unaanza mara moja?

(b) Kwa vile Redio Tanzania ni *Agency,* je, Serikali itakuwa tayari kulipia gharama ili utangazaji usikwame hata siku moja?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi kwamba, Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, imeiagiza Mamlaka ya Hali ya Hewa ikae na ijadiliane na *RTD* kuona namna bora ya kuweza kutangaza. Napenda tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, utangazaji wote unaofanywa kwenye Redio Tanzania unadhaminiwa na watu mbalimbali. Tulishindwa kutoa utabiri wa hali ya hewa kwa *RTD* kutokana na ukosefu wa fedha na kukosa mfadhili wa kutusaidia kufadhili kipindi hiki. Tutahakikisha baina ya idara hizi mbili tunawasiliana namna nzuri ya kuendesha huduma hizi na kuwafikia wananchi kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kulipia utabiri wa wiki moja ni shilingi 1,095,360/= . Tutaendelea kuwasiliana kuona shughuli hii inapata mfadhili na haitasita kutangazwa.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali kama ifuatavyo: Kwa kuwa hapo nyuma Serikali kwa kupitia idara ya hali ya hewa walikuwa wanatoa *Annual Hydrological Report* ambayo ilikuwa inatolewa kwa matumizi mbalimbali. Taarifa hiyo ilipotolewa hakuna nyingine tangu mwaka 1972. Je, Serikali inasema nini na kwamba sasa hivi wanaweza kuanza kutoa kitabu hicho ili kisaidie Mikoa pamoja na Wilaya katika kuona matatizo ya hali ya hewa pamoja na mwenendo wa mvua? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, napenda nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba, mamlaka ya hali ya hewa hutoa utabiri wa hali ya hewa kwa saa 24 hadi saa 48 na kusambaza katika vyombo vifuatavyo: *Television* ya Taifa, *Africa Media Group Television* ambayo hurushwa TVT, *DTV* na *Channel Ten, ITV, Africa Media Group, Radio Free Africa,* kwa ajili ya utabiri wa Mkoa wa Mwanza, Kanda ya Ziwa Victoria na Tabora, Magazeti ya *Daily News,* Mwananchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, *UNDP Representative, DAWASA* na sehemu nyingine. Si hivyo tu utabiri huu tunaupeleka Ofisi ya Mheshimiwa Rais, Ofisi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais, Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi Bara, Wizara ya Afya, Wizara ya Kilimo na Chakula, Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, Wakuu wa Vituo vyote vya Hali ya Hewa, kwa madhumuni ya kuzisambaza kwa ofisi husika ili watumiaji waweze kuzitumia. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutaendelea kufanya hivyo na akitaka taarifa hizo awasiliane na ofisi zinazohusika katika jimbo lake.

Na. 22

**Huduma ya Posta - Jimbo la Konde**

**MHE. MCHANDE SALIM MCHANDE** aliuliza:-

Kwa kuwa miaka ya nyuma katika Jimbo la Konde palikuwa na Huduma ya Posta lakini huduma hiyo muhimu iliondolewa mnamo miaka ya themanini ambapo mahitaji ya huduma hiyo yalikuwa makubwa.

(a) Je, ni sababu zipi zilizosababisha kuondolewa kwa huduma hiyo muhimu katika Jimbo la Konde?

(b) Je, kuna mpango gani wa kurudisha huduma hiyo muhimu kwa wananchi wa Konde?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mchande Salim Mchande, Mbunge wa Konde, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Huduma za Posta katika Jimbo la Konde zilihamishwa sambamba na Agizo la Serikali la kuhamisha Ofisi za Serikali ya Wilaya kutoka Konde na kupelekwa Micheweni, Pemba.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kuendelea kuwahudumia wakazi wa eneo la Konde, Shirika la Posta lilimteua wakala sehemu hiyo wa kuuza stempu za barua na shajala nyingine za posta. Kwa bahati mbaya utendaji wa wakala huyo haukidhi mahitaji ya huduma za posta za msingi kwa wakazi wa Konde. Aidha, baada ya kufanya tathmini upya juu ya mahitaji ya huduma ya posta kwa eneo la Konde, imedhihirika kuwa endapo Shirika la Posta Tanzania litafungua Ofisi Ndogo - Konde *(Konde Sub-Post Office* au *Konde Franchised Post Office),* mahitaji ya wananchi ya huduma za posta za msingi yatapatiwa ufumbuzi. Hivyo, Shirika la Posta Tanzania limepanga kufungua Ofisi ya Posta Ndogo - Konde mwaka 2004.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa wananchi wengi wanaoishi Tanzania Bara wanapenda sana kutumia huduma ya Posta ya *EMS*, pale wanapopeleka fedha kwa jamaa zao wanaoishi Pemba na kwa kuwa pale Pemba unakatika umeme, fedha hizo hazipatikani mpaka umeme unapowashwa tena hata kama ni kwa muda wa wiki moja. Je, Serikali ina mpango wa kuweka *generators* katika Posta za Pemba ili kuondoa usumbufu kwa wananchi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Hili ni swali jipya Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar liletwe kwa njia za kawaida.

Na. 23

**Uingizaji wa Sigara na Vileo Nchini**

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA** aliuliza:-

Kwa kuwa zipo taarifa kwamba wapo wafanyabiashara wanaoingiza sigara na vileo kinyume na taratibu za sheria za nchi. Je, Serikali inayo taarifa na jambo hilo na inachukua hatua gani dhidi ya hali hiyo?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, ningependa kuelezea kwa ufupi kuhusu taratibu ambazo mfanyabiashara anatakiwa kuzingatia kabla ya kuruhusiwa kuingiza sigara na vileo nchini. Taratibu hizo ni:-

(i) Leseni ya biashara ambayo hutolewa na Wizara yangu baada ya kuridhika kuwa anazo sifa zinazotakiwa;

(ii) Leseni ambayo inazingatia usalama wa bidhaa inayoagizwa nchini kwa mlaji kuzingatia masuala ya afya ya mlaji ambayo hutolewa na Mamlaka ya Chakula na Madawa ya Tanzania *(Tanzania Food and Drug Authority - TFDA)*, Mamlaka hii iko chini ya Wizara ya Afya;

(iii) Hati ya kusajiliwa kampuni ya mfanyabiashara kutoka Wakala wa Kusajili Biashara na Leseni za Viwanda *(Business Registration and Lincensing Agency - BRELA)* zimelipiwa kodi;

(iv) Hati kutoka Shirika la Viwango *(TBS)* inayoonyesha kuwa bidhaa husika inakidhi viwango vya ubora vya *TBS;* na

(v) *Taxpayers Identification Number(TIN), Value Added Tax (VAT)* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo machache, ningependa sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inayo taarifa kwamba, wapo wafanyabiashara wanaoingiza sigara na vileo kinyume na taratibu na sheria za nchi. Ili kupambana na tatizo hili, Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato *(TRA),* ilianzisha uwekaji stempu katika kila paketi ya sigara ili kuhakikisha kuwa sigara zote zinazoingizwa nchini zimelipiwa kodi na ambazo zimetayarishwa kwa ajili ya soko la nje haziuzwi nchini. Juhudi hizo zimepunguza tatizo hilo kwa kiasi kikubwa, lakini bado haijawezekana kudhibiti kabisa uingizaji wa sigara zenye alama bandia unaofanywa na wafanyabiashara wachache wasio waaminifu kwa nchi yao. Kwa upande wa vileo vile vile wamekuwepo siku hadi siku wafanyabiashara wanaoingiza vileo kinyume na taratibu za sheria za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pale Serikali inapowabaini wafanyabiashara wenye tabia hiyo mbaya, hatua kali zimekuwa zikichukuliwa dhidi yao. Hatua hizo ni pamoja na kuwakamata na kuwapeleka Mahakamani, kuwanyang'anya leseni zao na kadhalika.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kuuliza swali moja kama ifuatavyo: Kwa kuwa matatizo kama hayo yataendelea kuwepo na dawa yake ni kwa nchi kujitegemea yenyewe kwa kuzalisha vitu vya kutosha na vilivyo vingi. Je, Waziri anaweza kutuambia wameratibu vipi na bidhaa kiasi gani ambazo sisi wenyewe tuna uwezo wa kuanza kujitosheleza ili kupunguza kuwa tegemezi kwa kuagiza vitu kutoka nje? *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, haiwezekani kwa nchi kutojisheleza kwa kila kitu hata nchi zilizoendelea haziwezi kujitosheleza kwa kila kitu ambacho kinahitajika ndani ya nchi yao. Kwa hiyo, utaratibu wa kupata bidhaa kutoka nje lazima utaendelea kuwepo. Muhimu kupita yote ni namna gani ya kudhibiti hao wanaoingiza sigara au vileo kwa njia ya magendo *(smuggling)*, hilo ndiyo tatizo. Hilo tumesema kwamba tunachukua hatua muafaka kuwezesha hao wanaoingiza bidhaa kwa njia ya magendo wadhibitiwe kikamilifu.

Na. 24

**Viwanda vya Kusindika Nyanya**

**MHE. WILLIAM J. KUSILA** aliuliza:-

Kwa kuwa nyanya hulimwa kwa wingi katika Wilaya ya Dodoma Vijijini, Dodoma Mjini na sehemu nyingine hapa nchini. Je, vipo viwanda vingapi vya nyanya hapa nchini na vipo katika mikoa ipi?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa William Kusila, Mbunge wa Bahi, kama ifuatavyo:-

Kiwanda maarufu kwa usindikaji wa nyanya kipo Mkoani Iringa. Kiwanda hicho kinajulikana kwa jina la Dabaga. Kiwanda kingine na ambacho ni kipya kipo Mkoani Arusha na hutengeneza bidhaa zake kwa nembo ya *Red Gold.*

Mheshimiwa Spika, mbali na viwandani hivyo, pia wapo wazalishaji wadogo wadogo wa nyanya katika sehemu mbalimbali za nchi. Kama itakavyokuwa inafahamika, katika miaka ya hivi karibuni *SIDO* imekuwa ikiendesha mradi wa kutoa mafunzo ya kusindika mboga na vyakula zikiwemo nyanya. Chini ya mpango huu, zaidi ya akina mama 2000 hapa nchini wameweza kufaidika na mafunzo haya tangu mradi ulipoanza mwaka 1993 hadi sasa ambapo kati ya hao, 70% wameweza kuwa wajasiriamali wazuri katika fani hii. Aidha, zaidi ya nusu ya hao wajasiriamali wazuri wanajishughulisha zaidi na usindikaji wa matunda na mboga zikiwemo nyanya.

Mheshimiwa Spika, Dodoma ni moja ya mikoa iliyopatiwa mafunzo ya usindikaji na *SIDO*. Mnamo Machi, 2003, wananchi 32 Wilayani Mpwapwa walipatiwa mafunzo hayo na mnamo Septemba, 2003 wananchi wengine 32 wa Mjini Dodoma walipatiwa taaluma hiyo. Aidha, Mkoa una wakufunzi wawili wa usindikaji watakaoendeleza mafunzo hayo Mkoani Dodoma. Matumaini yetu ni kuwa wananchi hawa waliopata mafunzo watashirikiana na wataalamu wa *SIDO* na kadhalika kuona uwezekano wa kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya usindikaji zikiwemo nyanya.

**MHE. WILLIAM J. KUSILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupewa fursa hii na namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Swali langu ni kwamba, pamoja na jitihada ambazo zimeshachukuliwa na *SIDO* kuwasaidia wananchi wa Mkoa wa Dodoma kusindika nyanya, nadhani Waziri atakubaliana nami kwamba, bado kazi ambayo imefanywa ni ndogo sana na kwa vile nyanya ni zao linaloharibika haraka, Waziri atakubali kuwaelekeza *SIDO* Mkoani Dodoma ili waongeze kasi ya kazi hiyo nzuri ambayo wamekwishaianza ili tuweze kuimarisha kilimo cha nyanya katika Mkoa wa Dodoma na kuwapa fursa wananchi hasa vijana ya kujiajiri na kuondoa umaskini? *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nakubaliana naye kwamba, tutaendelea kuwahimiza *SIDO* waendelee kupanua juhudi zao katika Mkoa wa Dodoma. Lakini vile vile napenda niseme kwamba, hizi mashine ndogo za kusindika nyanya siyo ghali sana. Taarifa tuliyokuwa nayo ni kwamba, unaweza ukapata mtambo ambao utakuwa unasindika nyanya tani tatu katika muda wa saa 24 ambao utagharimu shilingi 110 milioni. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mtambo wa nyanya unasindika nyanya tani tatu kwa saa 24 kwa shilingi milioni 110 siyo nyingi. Kiwanda siku zote ni cha ghali, siyo sawa sawa na jembe, jembe ni shilingi 5,000, 10,000 lakini kiwanda lazima itakuwa ghali. Lakini hiki ninachosema mimi siyo ghali kwa sababu kwanza, mashine peke yake ni shilingi milioni 43. Tukiweza kukipata hicho, tatizo la nyanya kuharibika Dodoma litakwisha, ni mtambo mdogo huu siyo mkubwa. Ahsante. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niulize swali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Waziri amesema viwanda vikubwa vya nyanya nchini viko Iringa na Arusha na amekubaliana nasi kwamba Mkoa wa Dodoma nyanya ni nyingi sana ikiwa ni pamoja na Wilayani Kongwa. Sasa je, Mheshimiwa Waziri na Wizara yake, atakuwa tayari kuvutia wawekezaji kwa sababu kama alivyosema kiwanda kimoja ni zaidi ya shilingi milioni 110 ili waweze kuwekeza viwanda vya kusindika nyanya hasa Wilayani Kongwa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, niko tayari kuendelea kuwahamasisha wawekezaji wawekeze siyo tu Mkoa wa Dodoma na Wilaya ya Kongwa, bali sehemu zote nchini nafanya hiyo kazi siku zote ndiyo kazi yangu. Mahenge tunaweza tukakuacha. Lakini kitu cha msingi ambacho sote tunapaswa kukumbuka ni kwamba, wawekezaji wa nje wanakwenda katika sehemu ambapo kuna miundombinu rahisi ndiyo sasa hivi viwanda vingi vinajengwa Dar es Salaam, Tanga kidogo na Arusha. Kwa hiyo, ni muhimu kuandaa miundombinu inayostahili ili tuweze kuwavutia wawekezaji. Bila hilo hatuwezi kufanikiwa. Hilo la kwanza. Lakini la pili ni muhimu kuwavutia wawekezaji wa ndani kwa mfano, mimi nina hakika kabisa hapa Dodoma tuna wawekezaji wenye uwezo ambao wanaweza wakawekeza katika kiwanda cha kusindika nyanya, hao ndiyo tuwahimize na hao tuwawekee mazingira mazuri. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri, nina swali kama ifuatavyo: Kwa kuwa Waziri, ameeleza kuwa vikundi vingi vimeweza kufundishwa kusindika chakula zikiwemo mboga, hiyo tunashukuru sana. Je, inakuwaje vikundi hivyo vinavyojihusisha na shughuli hizo na kufanikiwa bado vinapata matatizo ya kupata nembo ya *TBS* katika vyakula vinavyosindikwa?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nembo za *TBS* zinatolewa kwa kuzingatia hatua fulani ya kiwango ndiyo maana ni muhimu kwa wenye viwanda vidogo vidogo wajitahidi kufikia hatua inayotakiwa ya kiwango, bila kuzingatia viwango hatuwezi kuwa tunafanya biashara inayofaa. Lazima suala la viwango tulizingatie wakati wote na wako wasindikaji wadogo wanaofikia viwango vya *TBS* na hawapewi. Lakini wale ambao wanataka wapendelewe kwa sababu wao ni wasindikaji wadogo wadogo haiwezi kukubalika kwa sababu suala la afya ya wananchi ni muhimu sana. Pia watu wa mamlaka ya vyakula na madawa ambao wako chini ya Wizara ya Afya, hawawezi kukubali kutoa leseni kwa kiwanda kidogo ambacho hakifikii kiwango cha utengenezaji kinachotakiwa.

Na. 25

**Ajira Katika Asasi Zinazomilikiwa na Wageni**

**MHE. PHILIP A. MAGANI** aliuliza:-

Kwa kuwa muda mrefu kumekuwepo na malalamiko ya tuhuma za ubaguzi katika ajira yaliyopelekea migomo ya wafanyakazi kama wafanyakazi wa Hospitali za Hindu Mandal na Aga Khan za Dar es Salaam na *Friendship Textile Mills;* na kwa kuwa katika malalamiko hayo yako madai kuwa wafanyakazi wenye asili ya Kiasia hupata marupurupu mazuri kuliko wale wa asili ya Kiafrika hata kama wana sifa za utaalam zilizo sawa au pengine zaidi; na kwa kuwa baadhi ya makampuni au asasi hizo hazitoi hata barua za ajira kwa wafanyakazi wenye asili ya Kiafrika na hivyo kuwakosesha marupurupu pamoja na mafao baada ya kustaafu kazi:-

(a) Je, Serikali imefanya utafiti wowote kuhusu hizi zinazoashiria ubaguzi wa rangi ili kubaini ukweli wake?

(b) Endapo utafiti umefanywa na ukweli wa tuhuma hizo kubaini, je, Serikali imechukua hatua zipi za kisheria dhidi ya asasi zenye tabia hiyo?

(c) Je, Serikali imeweka utaratibu gani wa kuhakiki utekelezaji wa sera za ajira katika makampuni mbalimbali na watu binafsi ili kuhakikisha wananchi hawanyanyaswi, kubaguliwa wala hawapunjwi haki zao za ajira?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Philip Alfred Magani, Mbunge wa Ruangwa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia sehemu ya ukaguzi viwandani, huwa inafuatilia katika makampuni na asasi ambazo zinalalamikiwa kwa vitendo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na unyanyasaji, ubaguzi na kutolipwa ipasavyo. Kwa kwa mfano, Kiwanda cha *Kioo Limited,* walipolalamikiwa hatua za ukaguzi zilichukuliwa lakini haikuwa rahisi kubaini tatizo hilo kwa kupitia uchunguzi wa wazi. Utatuzi wa tatizo unategemea ushirikiano wa wafanyakazi hasa kupitia vyama vyao mahali pa kazi, ambao wanaweza kupata ushahidi wa unyanyasaji huo ili ukaguzi na hatua za kisheria zichukuliwe. Sheria zetu haziruhusu ubaguzi.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu utafiti wa asasi zenye tabia hizo ni kwamba, Serikali haijapata kesi zenye vithibitisho kamili ili ziwakilishwe kwenye vyombo vya sheria.

(c) Utaratibu uliopo hivi sasa ni kuimarisha ukaguzi maeneo ya kazi ili kuweza kubaini kasoro mbalimbali zilizopo, ikiwa ni pamoja na unyanyasaji au ubaguzi kazini. Sheria mbalimbali za kazi ambazo hivi sasa zinafanyiwa marekebisho zitazingatia hoja zinazotolewa na wadau wote ikiwa ni pamoja na Vyama vya Wafanyakazi. Tunatarajia kuwa mara sheria hizo zitakapowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu, mambo yote yanayohusu haki za wafanyakazi yatakuwa yamezingatiwa.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa wakati huu ni wa uwazi na ukweli na kwa kuwa lalamiko hili limekuwa ni kubwa sana na kwa muda mrefu hata baadhi ya Mawaziri wetu wametembelea viwanda wakajionea wenyewe. Je, utafika wakati ambapo Wizara husika itatunza takwimu na pengine kama asasi zilizoonyeshwa hapa Bungeni kuona viwango vya watumishi waathirika na watumishi wanaoingia wanavyovipata na wakati huo huo kujua ni watu wangapi wanaajiriwa katika viwanda mbalimbali au katika maeneo mbalimbali ambapo malalamiko yanazidi kuwa makubwa na watu kuleta migomo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, narudia kusema kwamba, ili Wizara iweze kutambua matatizo yaliyomo katika makampuni na asasi za watu binafsi ni lazima tupate ushirikiano wa wafanyakazi. Kwa bahati mbaya mfanyakazi huogopa kueleza ukweli asije akapoteza ajira yake, ndiyo maana tunaweka mkazo zaidi katika Vyama vya Wafanyakazi ambavyo vyenyewe haviwezi kupata adhabu ya moja kwa moja kutoka kwa mwajiri. Kwa hiyo, tunaendelea kushirikiana na Vyama vya Wafanyakazi kuwaelimisha kwamba jukumu la kuwatetea wafanyakazi si la Serikali peke yake, bali kwa ushirikiano wa Serikali na vyama hivyo katika maeneo ya kazi. Kwa hiyo, wakati utafika tu pindi Vyama vya Wafanyakazi vikiamka na kujua wajibu wao barabara badala ya kusubiri matatizo yatokee ndipo waongeze migomo.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Waziri amekiri kwamba walipokuwa wanafanya uchunguzi katika Kiwanda cha Kioo haikuwa rahisi kupata taarifa za unyanyasaji wa wafanyakazi Wazalendo. Je, Serikali au Wizara hii ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, ikijua kabisa kwamba malalamiko haya yapo miaka nenda miaka rudi na ikijua kabisa kwamba Vyama vya Wafanyakazi katika taasisi au makampuni yanayoendeshwa na jamii hii ya Wahindi au watu wanaotoka Asia wakijaribu kukwepa suala hili lisiweze kufika Serikalini, Wizara inaona ni hatua zipi zichukuliwe? Si kuunda Tume ambayo itafanya kazi kwa kina ili kuweza kuwanusuru wafanyakazi wa Tanzania ambao wananyanyaswa katika Taasisi za watu hawa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mbunge wa Kalambo, kama ifuatavyo:-

Tumetafuta njia nzuri zaidi badala ya kuunda Tume, maana kwa huu uchumi binafsi ulivyoonea katika kila kona katika nchi yetu tutakuwa tunaunda Tume kila siku ya Mungu na kutumia gharama kubwa bila sababu. Kwa hiyo, hatua tuliyoifanya ni kuwezesha Vyama vya Wafanyakazi na tunachukua nafasi hii kuwashukuru sana watu wa *ILO* kwa kutuongozea semina za mara kwa mara kwa Vyama vya Wafanyakazi, ili vitambue wajibu wao wa kusaidia wafanyakazi wao maana wafanyakazi wenyewe kama walivyo wakiamua kujitokeza dhahiri watapoteza ajiri zao. Ndiyo maana kule *Kioo Limited,* wametuandikia barua bila saini juu ya malalamiko yao, tumekwenda kupata walau ushahidi kwa mtu mmoja hakuna aliyejitokeza. Kwa hiyo, Vyama vya Wafanyakazi vina wajibu mkubwa katika hili kuliko kuunda Tume. Tutaunda Tume ngapi wakati kila siku ya Mungu malalamiko ya namna hii yanafika Wizarani kwetu.

Na.26

**Tatizo la Ukosefu wa Ajira kwa Vijana**

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE** aliuliza:-

Kwa kuwa nchi yetu inaingia katika tatizo la Ukosefu wa ajira rasmi kwa kasi hasa kwa sababu ya kuongezeka kwa kiasi kikubwa kwa vijana wanaohitimu mafunzo katika Vyuo mbalimbali vya taaluma hapa nchini na nje ya nchi na kwa kuwa inawezekana kabisa kwa kutumia uzoefu uliopatikana kutokana na zoezi la ajira ya Walimu hapa nchini kwamba nchi yetu haina tatizo la ajira bali ni tatizo la upangaji wa ajira:-

(a) Je, Serikali imezingatia ushauri uliotolewa wa kuanzisha *Database* ya vijana na ajira hapa nchini ili kuwajua vijana wote wa nchi hii na kazi wanazofanya?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kukipanua Kituo cha Ajira kilichoko Dar es Salaam kufikia Mikoa yote nchini?

(c) Je, Serikali inasema nini juu ya usumbufu mkubwa wanaoupata vijana kwa kulazimika kusafiri umbali mrefu kwenda Dar es Salaam kuhudhuria usaili?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Kipole, Mbunge wa Msalala, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inazingatia kikamilifu ushauri uliotolewa wa kuanzisha *Database* ya vijana na ajira hapa nchini li kuwajua vijana wote wa nchi hii na kazi wanazozifanya. Ili kuhakikisha kuwa utekelezaji wake unakuwepo pamoja na mambo mengine Serikali ina mipango ifuatayo:-

(i) Kuimarisha Idara ya Maendeleo ya Vijana kwa maana ya kuwa na vifaa vya kisasa vya kutunzia takwimu za vijana. Kuwapo na/au kuwajengea uwezo Maafisa wanaoshughulikia masuala ya vijana katika ngazi mbalimbali; na

(ii) Kuimarisha mtandao unaohusu masuala ya vijana ikiwa ni pamoja na kusisitiza kuwepo na Afisa anayeshughulikia masuala ya vijana kila Mkoa.

(b) Mheshimiwa Spika, kazi ya msingi ya Kituo cha ajira ni kuainisha watafutaji kazi na mahitaji ya waajiri na hivyo kuwawezesha kuokoa muda na fedha kwa kuwapatia waombaji wenye sifa zinazotakiwa kutoka kwenye orodha ya watafutaji kazi. Kwa ujumla, huduma ya Kituo ya uainishaji

inawapatia waajiri unafuu, urahisi wa kuokoa muda na fedha katika kutafuta watu wenye sifa kwa ajili ya kufikiria kujaza nafasi za kazi zilizopo.

Serikali inatambua umuhimu wa kupanua Kituo cha Ajira kilichoko Dar es Salaam kufikia Mikoa yote. Hata hivyo, suala la upanuzi wa Kituo linakwenda sambamba na kuimarisha na kuongeza watumishi ili kukidhi mahitaji ya nchi nzima. Mara hali ya fedha itakaporuhusu Serikali itaendelea kupanua shughuli za Kituo hiki.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa wakati huu ambapo kituo hakijapanua shughuli zake Mikoani ni kweli kabisa vijana wengi huwa wanapata usumbufu wa kuja Dar es Salaam kwa ajili ya kuhudhuria usaili. Mara baada ya kuimarisha Kituo hiki, tatizo hili la vijana na watu wengine kuja Dar es Salaam kwa ajili ya usaili litapungua kwa kiwango kikubwa.

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi niulize swali la nyongeza kama ifuatavyo: Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali juu ya usumbufu wa vijana kusafiri kutoka kule Msalala kwangu na kwingineko mbali na Dar es Salaam, kuja Dar es Salaam ameeleza kwamba linashughulikiwa. Je, kwa kipindi ambacho suala hili linashughulikiwa Serikali inaweza angalau kugharamia posho za siku walau mbili kwa vijana wanaotoka mbali pamoja na kuwarejeshea nauli ili waweze kujikimu wakiwa Dar es Salaam kutafuta kazi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, inachofanya Serikali ni kuwasaidia vijana wetu kuweza kuwatafutia kazi na kuwapa usaili na wakati mwingine tunawapa na mbinu za *interview* zinavyokuwa kule kwa Waajiri kutegemeana na sehemu. Sasa tunapolazimika kuwalipia nauli na posho inakuwa kama vile umembeba mgonjwa wa kidonda unamvusha mtoni unampiga na makonzi, fanya haraka! Utambwaga tu. Mimi nafikiri uwezo huo hatuna, atatuwia radhi sana Mheshimiwa. Lakini naomba kama umeweza kumsomesha mtoto wako akamaliza, jitahidi basi kumsafirisha kama ameitwa kwenye usaili ili umalizie mkia baada ya kula ng'ombe mzima. *(Kicheko)*

Na.27

**Chuo cha Usafirishaji**

**MHE. ASHA ALI NGEDE** aliuliza:-

Kwa kuwa sasa hivi dreva hawezi kupata leseni mpaka awe amepata mafunzo katika Chuo cha Usafirishaji:-

(a) Je, Chuo hicho kina uwezo wa kuchukua wanafunzi wangapi na kwa muda gani?

(b) Je, Serikali haioni kwamba sasa kuna umuhimu wa kujenga Chuo cha aina hiyo kimkoa au kikanda?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha Ali Ngede, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Usalama Barabarani Na.30 ya mwaka 1973 kama ilivyorekebishwa na Sheria ya Usalama Barabara Na.16 ya mwaka 1996, mwombaji wa leseni ya udreva anatakiwa ahudhurie mafunzo ya udreva katika Shule ya Udreva iliyosajiliwa, afundishwe na Mkufunzi aliyesajiliwa. Mafunzo haya hutolewa sio na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji peke yake, bali pia na Vyuo binafsi vilivyosajiliwa huko Mikoani na Vyuo vya *VETA* ambavyo pia vimesambaa katika Mikoa mingi nchini.

Chuo cha Taifa cha usafirishaji ambacho hivi sasa hufundisha madreva wa ngazi mbalimbali zaidi ya 3,000 kwa mwaka, hivi sasa kinajishughulisha zaidi na mafunzo ya kukuza ustadi na kuinua viwango

vya udreva kwa madreva wazoefu, wakati mafunzo ya udreva wa awali hushughulikiwa zaidi na *VETA* na Vyuo vya udreva vya binafsi vilivyosajiliwa.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *VETA* ina matawi katika Mikoa mingi na vile vile takriban katika kila Mkoa kuna Vyuo binafsi vya mafunzo ya udreva vilivyosajiliwa na Serikali, kwa sasa hakuna umuhimu wa kujenga Chuo cha Udreva cha Serikali katika kila Mkoa au Kikanda. Hivi sasa Serikali inafanya jitihada kuimarisha Chuo cha Taifa cha Usafirishaji na Vyuo vya *VETA* ili vitoe mafunzo bora zaidi na kwa madreva wengi zaidi.

**MHE. ALI MACHANO MUSSA:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kumwuliza swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa kuna Maaskari wastaafu wamepata mafunzo katika Vyuo kama vile *Police College* na Vyuo vingine vya kiaskari na vimetoa mafunzo mazuri ambayo yanafanana na Chuo cha Usafirishaji; je, kuna mpango gani wa kuvikubali vyeti vile vya Maaskari wastaafu ili kuondoa msongamano wa kupata mafunzo katika Chuo cha Usafirishaji? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, mafunzo haya yanatolewa kwa mujibu wa sheria ile niliyoitaja na sheria inasema kwamba, mafunzo ya udreva yatatolewa katika Vyuo ambavyo vimesajiliwa na walimu ambao wamesajiliwa. Kwa hiyo, hawa Askari Wastaafu kama wakiweza kuanzisha Vyuo kama hivi na vikasajiliwa, hapana shaka yoyote, watapata fursa ya kutoa mafunzo hayo.

Na.28

**Askari Wanaohamishiwa Kituo Kidogo cha Polisi Mnazi**

**MHE. CHARLES H. KAGONJI** aliuliza:-

Kwa kuwa inasemekana kwamba uhamisho wa baadhi ya Polisi kwenda kwenye Kituo Kidogo cha Polisi Mnazi unafanywa kama adhabu kwa Askari hao kutokana na makosa waliyoyafanya kwenye maeneo mengine na kwamba taarifa hizo zimeungwa mkono na tabia ya baadhi ya Askari hao ya kujihusisha na biashara zaidi kuliko kazi zao:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya jambo hili?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kuchukua hatua za haraka na za makusudi dhidi ya wale wote waliofanya kitendo cha kuwahamishia Askari wenye makosa kama nilivyoeleza hapo juu kwenye Kituo cha Mnazi na kuhakikisha kwamba wanawajibishwa ipasavyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Kagonji, Mbunge wa Mlalo, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni mara chache sana uhamisho hutolewa kwa Askari kama adhabu kwa lengo la kumpatia mtumishi nafasi ya kujirekebisha kitabia. Hata hivyo, hatua hiyo huchukuliwa baada ya mhusika kufunguliwa mashtaka na kujitetea mbele ya Mahakama ya Kijeshi na kupatikana na hatia. Adhabu ya kuhamishwa inapotolewa hutamkwa wazi katika hukumu. Aidha, baada ya kutolewa hukumu hiyo, Askari anayehusika huwa na haki ya kuitekeleza adhabu hiyo au kukata rufaa na kupinga adhabu hiyo ikiwa ataona hakutendewa haki.

Mheshimiwa Spika, Askari waliohamishiwa Kituo cha Polisi Mnazi walihamishwa katika utaratibu wa uhamisho wa kawaida na wala sio kwa adhabu. Hii inatokana na ukweli kuwa hawakuwahi kushtakiwa na kupatikana na hatia kwa makosa yoyote. Hata hivyo, ikiwa ushahidi utapatikana kuwa

Askari hao wamehamishiwa katika Kituo cha Manzi kwa adhabu bila kufunguliwa mashtaka, kujitetea na kuonekana na hatia, Serikali haitasita kuwachukulia hatua za kinidhamu wale wote waliotoa adhabu bila kufuata taratibu na Sheria za Jeshi la Polisi.

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Naamini kwamba, Serikali kama ilivyosema itafuatilia kwa sababu baadhi ya majina na namba za Askari hawa waliohamishiwa maeneo hayo kwa migogoro niliyotaja ninayo. Sasa swali dogo la nyongeza.

Katika Mkutano uliopita tuliuliza na kulalamika kwenye Wizara hii kwamba, Kituo hiki cha Mnazi ambacho kiko umbali wa zaidi ya Kilometa 100 kutoka Makao Makuu ya Wilaya Askari wake hawana nyenzo za kufanyia kazi, hata visu vya mkononi hawana. Tukasema usafiri hawana, hata *radio call* iliyoko kwenye Kituo kile ni ya zamani kiasi kwamba mawasiliano ni magumu, Wizara hii ikaahidi kwamba inachukua hatua. Je, hatua hizo kama zimechukuliwa, hadi leo zimefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Mnazi ni kweli Mheshimiwa Mbunge alileta malalamiko kwamba kiko mbali na Makao Makuu ya Wilaya kwa hiyo, kiimarishwe na tumeshaanza kukiimarisha. Katika kukiimarisha ni pamoja na kuongeza Askari. Wakati ule analalamika kulikuwa na Askari wanne, sasa wako Askari wanane pamoja na kwamba anasema walioongezwa wamepelekwa kama adhabu, sisi tunasema tumeongeza kwa nia njema, hakuna adhabu yoyote na kusema kweli tangu wamekwenda hatujasikia malalamiko ya wananchi wakilalamika kwamba, Askari wale utendaji wao ni mbaya. Kwa hiyo, tumeongeza idadi.

Mheshimiwa Spika, katika nyenzo, tutaanza na *radio call* kwa sababu Bunge hili limetupatia pesa katika bajeti iliyopita bilioni 1.3 kwa ajili ya kuimarisha mawasiliano ya Jeshi la Polisi Mikoani. Kwa hiyo, nina hakika Vituo vingi sasa vitapata *radio call* kwa pesa hizi ambazo tumepewa pamoja na Kituo cha Mnazi. Vifaa vingine kama magari, hivyo uwezo sasa hivi haupo, naomba Waheshimiwa Wabunge wote ambao Vituo vyenu havina magari, msubiri wakati fedha zikitafutwa. *(Makofi)*

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa uhamisho ni sehemu ya ufanisi wa kazi na miaka ya nyuma Serikali ilikuwa na utaratibu mzuri wa kuhamisha wafanyakazi kwenda kwenye *section* nyingine kwa kuleta ufanisi hasa kwa Maaskari na tatizo ambalo linajitokeza Mnazi ni hilo la Askari wengine ama wafanyakazi kukaa kwa muda mrefu mahali na kuzoea mpaka kufanya biashara; je, Serikali ina utaratibu gani wa kurudisha utaratibu wa kuhamisha wafanyakazi wa umma na wasiofanya kazi za Serikali kwa utaratibu ule wa zamani ili kuongeza ufanisi kazini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, uhamisho ni sehemu ya kuleta ufanisi wa kazi katika Serikali na katika Jeshi la Polisi katika kanuni za uendeshaji wa Jeshi lile, Askari akikaa mahali miaka mitatu hadi mitano, kwa utaratibu anatakiwa ahamishwe asizoeane sana na watu wa pale. Lakini kanuni hii tumekuwa tunashindwa kuitekeleza kwa sababu tu ya gharama zake. Hivi sasa bajeti ya Jeshi la Polisi, Bunge hili limekuwa linaiboresha mwaka hadi mwaka. Kwa hiyo, jinsi bajeti inavyoboreka, jinsi sasa ambavyo uwezo wa kugharamia uhamisho utakavyopatikana, tutarejea katika kanuni hii ya kuhamisha Askari kila wanapokaa katika Kituo kimoja kwa muda mrefu kiasi cha kuzoea mazingira ya mahali hapo. Kwa hiyo, jambo hili linakuja lakini inategemea sana na uwezo wetu wa bajeti.

Na.29

**Masoko ya Mazao**

**MHE. ALLY AMANI KARAVINA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika kujibu Swali Na.301 katika Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bunge, Serikali ilisema kuwa bei ya mazao inapangwa na Mkutano wa Wadau wote:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba mfumo huo ni hatari katika nyakati hizi za soko huria kwani wanunuzi ni wajanja na wana utaalamu na uzoefu mkubwa katika biashara ya Kimataifa ikilinganishwa na Wawakilishi wa wananchi na kwamba msingi wa bei ya zao ni bei iliyoko kwenye Soko la Dunia na haihitaji mjadala wa wanakamati?

(b) Je, Serikali inafanya nini kusaidia uratibu wa bei za mazao ya mkulima ili kuhakikisha kwamba hawapunjwi na wanunuzi binafsi?

(c) Kwa kuwa tangu mwaka 2001 Serikali imekuwa ikitoa ahadi ya kuunda Kitengo kinachosimamia masoko ya mazao mchanganyiko, je, ni lini Kitengo hicho kitaanza kutoa huduma hiyo kwa wakulima wa Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mhehsimiwa Ally Amani Karavina, Mbunge wa Urambo Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inaamini kuwa utaratibu wa kupanga dira ya bei ya mazao ya wakulima kwa kuhusisha wadau wote wa zao ni sahihi kwani chini ya utaratibu huo uko uwazi wa kutosha. Dira ya bei yaani bei ya kuanzia majadiliano hupangwa kwa kuzingatia sio tu mwenendo wa bei katika Soko la Dunia lakini pia gharama za uzalishaji kwa mkulima. Wawakilishi wa wakulima hufanya majadiliano hayo ya bei kwa kuzingatia gharama za uzalishaji na faida apatayo mkulima ili aweze kuendelea kulima zaidi. Aidha, Bodi za Mazao pamoja na Wataalam wa Kilimo na Chakula, pamoja na wale wa Wizara ya Ushirika na Masoko ambao wanao utaalamu mkubwa katika biashara za mazao husika, husimamia na kushiriki kikamilifu katika majadiliano hayo ya kupanga dira ya bei kwa lengo la kuhakikisha kuwa wakulima wanapata bei ya kuridhisha. Pamoja na hatua hii, Wizara yangu imeandaa mikakati wa kuwaongezea stadi za biashara wawakilishi wa wakulima katika ngazi mbalimbali ili waweze kuwa na uwezo zaidi wa kujadiliana na kupatana bei kupitia vikao vya wadau.

Mheshimiwa Spika, Sheria zilizoanzisha Bodi za Mazao zinazipa uwezo Bodi hizo kuwanyima au kufuta leseni za wanunuzi wa mazao wanaokiuka sheria, kanuni na taratibu zinazohusika. Kanuni hizo ni pamoja na viwango vya chini vya bei vinavyokuwa vimekubalika na wadau wote. Endapo bei ya mazao hayo katika Soko la Dunia itashuka kwa kiwango kikubwa na hivyo kuwafanya wanunuzi hao kushindwa kununua kwa bei iliyopendekezwa kwenye dira ya bei, wanunuzi hawana budi kuomba ufanyike mkutano wa wadau chini ya usimamizi wa Bodi husika ili kufanya mapitio ya bei na hivyo kupanga dira mpya ya bei.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kuratibu na kuhakikisha kwamba wakulima hawapunjwi na wanunuzi binafsi, Serikali inafanya mambo yafuatayo:-

(i) Kuimarisha Vyama vya Ushirika au Vikundi vya wazalishaji hususan katika masuala ya elimu ya ushirika na stadi za biashara kwa lengo la kumwongezea mkulima uwezo wa kupatana bei anapouza mazao yake;

(ii) Kusimamia sheria, kanuni na taratibu za ununuzi na uuzaji wa mazao kwa lengo la kuhakikisha kuwa bei ya mkulima ni ya kuridhisha na inaendana na hali halisi katika Soko la Dunia;

(iii) Kufanya tafiti mbalimbali za masoko ikiwa ni pamoja na zile za kubaini gharama mbalimbali za kununua na kuuza mazao ili kutoa mapendekezo kwa Vyama vya Ushirika ambavyo ndiyo vyombo vinavyotumiwa zaidi na wakulima katika kuuza mazao yao. Aidha, kutoa taarifa za masoko zilizofanyiwa utafiti kwa lengo la kuwezesha mikutano ya wadau kujadiliana na kupanga dira ya bei kulingana na mwenendo katika soko;

(iv) Kuandaa taratibu ambazo zitawezesha mazao kununuliwa katika Vituo maalum, kwa maana ya magulio na minada ili kuleta ushindani wa haki kwa kukutanisha wanunuzi wengi. Hatua hii

inalenga katika kuondoa mtindo mbaya ambapo mnunuzi anaweza kununua mazao moja kwa moja kutoka nyumbani kwa mkulima; na

(v) Wizara inachukua hatua za kuimarisha Idara ya Masoko kwa kuipatia nyenzo na teknolojia ya kisasa na mawasiliano ya kisasa ili iweze kutafiti juu ya mwenendo wa masoko na bei ya mazao ndani na nje ya nchi ili iweze kutumika kwa wafanyabiashara na wakulima wa mazao.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kushirikiana na Wizara ya Ushirika na Masoko, ilikwishafanya uchunguzi kuhusu uwezekano wa kuunda Bodi ya Mazao mchanganyiko ambayo ingeratibu shughuli za mazao mchanganyiko. Hata hivyo, hatua hiyo imesitishwa kwa muda hadi hapo sera ya masoko inayoandaliwa na Serikali itakapokamilika. Kutokana na Sera hiyo, Serikali itaweza kuamua ni mazao gani yanayofaa kuundiwa Bodi ya Mazao Mchanganyiko na ni yapi yatahitaji kuwa na Bodi ya peke yake.

**MHE. ALLY AMANI KARAVINA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja dogo la nyongeza. Kwa sababu kuna mwongozo wa Benki ya Dunia unaotaka angalau mkulima wa zao alipwe asilimia 60 ya bei iliyoko kwenye Soko la Dunia, je, ni mazao mangapi na hasa mazao yetu makuu ya biashara ambayo yanazingatia mwongozo huo kwa sasa ikiwa ni pamoja na zao namba moja, tumbaku?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumekwishajibu baadhi ya maswali hapa Bungeni, pamoja na maelezo ya Serikali ni kwamba, suala la mkulima kulipwa angalau asilimia 60 ya bei, kusema kweli ni ushauri ambao ulikuwa unazingatiwa wakati ule ambapo uuzaji wa mazao ulikuwa unapitia katika mkondo mmoja wa Vyama vya Ushirika ambapo ilikuwa ni kushauri gharama mbalimbali za ununuzi ziweze kuzingatiwa na Vyama vya Ushirika angalau asilimia hiyo 60 iweze ikazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sasa sio rahisi kusema ni mazao mangapi na ni lini yatafikia kiwango hiki kwa sababu tu ya utaratibu wa soko huria ambapo wanunuzi wa mazao haya wako katika hatua za tofauti tofauti. Kwa hiyo, suala hili haliwezi kutolewa tamko sasa hivi kwa sababu ya utaratibu mpya wa ununuzi wa mazao.

**MHE. DR. JAMES ALEX MSEKELA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa jibu la swali la nyongeza la Naibu Waziri akijibu swali la Mheshimiwa Karavina halijaeleweka, naomba angalau atoe mfano wa zao hata moja na linalokaribia asilimia 60 na kwa nini ametoa maelezo ambayo yanaonesha kwamba tuko mbali sana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, unao mfano huo? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, nataka nirudie yale niliyoyasema. Nimesema kwamba, itakuwa sio rahisi kutoa mfano sasa hivi wa zao hata moja kutokana na mfumo wa sasa hivi wa uuzaji wa mazao katika mfumo wa soko huria. Ingelikuwa ni rahisi kutoa mfano huo kwa wakati ule ambapo mazao yote yalikuwa yanapitia katika mkondo mmoja wa Vyama vya Ushirika, hapo ndipo tulipokuwa tunashauri kwamba, wanunuzi ama zile gharama za ununuzi ziweze kupunguzwa kiasi cha kwamba angalau mkulima aweze kulipwa hiyo asilimia 60. Kwa hiyo, nimesema tu kwamba, kwa sasa hivi si rahisi kutoa hata mfano mmoja kutokana na mfumo wenyewe wa ununuzi wa mazao sasa hivi katika mfumo wa soko huria. *(Makofi)*

Na.30

**Mwelekeo wa Bei ya Korosho**

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA** aliuliza:-

Kwa kuwa Bodi ya Korosho kila mwaka hutangaza mwelekeo wa bei ya korosho kabla ya msimu husika kuanza mathalani Sh.500/= au Sh.550/= kwa kilo na kwa kuwa wakati wa ununuzi wanunuzi

hupinga mwelekeo huo na kununua korosho chini ya bei hiyo mathalani hununua kwa Sh.200/= au Sh.250/= badala ya Sh.500/= au Sh.550/= kwa kilo.

Je, kuna sheria ipi inayoilinda Bodi kuhakikisha mwelekeo wa bei ya korosho unaopangwa kama Sh.500/= na Sh.550/= kwa kilo wanunuzi hawakiuki ili wakulima wanufaike na bei nzuri ya zao hilo?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Korosho imeweka utaratibu wa kuwakutanisha wawakilishi wa wadau mbalimbali wa korosho kabla ya msimu wa ununuzi kuanza. Mkutano huo wa wadau ambao hujumuisha wataalam kutoka Wizara ya Ushirika na Masoko, pamoja na wale wa Wizara ya Kilimo na Chakula hupanga dira ya bei ya korosho za daraja zote mbili kwa kuzingatia hali ya soko la korosho duniani. Lengo kuu la kupanga dira ya bei ni kuwapatia wakulima taarifa ya bei ya wastani wa chini inayotegemewa katika msimu husika kulingana na hali ya soko duniani. Utaratibu huu hauna lengo la kupanga bei maalum ya kununulia korosho bali lengo ni kuwaongezea wakulima uwezo wa kujadiliana na wafanyabishara juu ya bei ya kuuzia korosho zao. Bodi ya Korosho hufuatilia mwenendo wa bei zinazotolewa na wafanyabiashara wakati wa ununuzi na huhimiza wafanyabiashara kuzingatia dira ya bei.

Mheshimiwa Spika, sheria iliyoanzisha Bodi ya Korosho inaipa uwezo Bodi hiyo kumnyima leseni mnunuzi wa korosho anayekiuka sheria, kanuni na taratibu za ununuzi zilizowekwa ikiwa ni pamoja na makubaliano ya dira ya bei yanayofikiwa na Wadau wa Korosho nchini.

Mheshimiwa Spika, endapo bei ya korosho katika Soko la Dunia itaporomoka kwa kiwango kisichotegemewa na hivyo wanunuzi kushindwa kununua korosho kwa bei iliyotarajiwa kutokana na dira iliyowekwa, wanunuzi hawana budi kutumia utaratibu ule ule wa kukutana na wadau wote na kukubaliana dira mpya ya bei chini ya usimamizi wa Bodi ya Korosho. Utaratibu huo ni mzuri kwa sababu una lengo la kuwalinda wakulima wasipunjwe bei na wanunuzi wa korosho.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Hivi Serikali ina kikwazo gani isianzishe Mfuko, yaani *Price Stabilization Fund* ili bei ya korosho inapoteremka Serikali ifidie pale ili wakulima wasipate hasara? *(Makofi)*

Swali la pili ni kwamba, kwa kuwa korosho zinazobanguliwa bei yake ni ya juu lakini kikwazo cha kuwekeza viwanda vya kubangua korosho Mtwara ni umeme ambapo Naibu Waziri anadhani bado umeme Mtwara tunaupata kumbe hatuupati, je, Serikali ipo tayari kuboresha umeme ili viwanda vya korosho vijengwe kwa wingi Mtwara ili bei iwe ya juu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, tumeshawahi kutoa taarifa Bungeni, mipango ya muda mrefu ya kupeleka umeme Mtwara na mipango ya muda mfupi, mipango ya muda mfupi niliitolea taarifa Asubuhi leo kuwa imetekelezwa kwamba Serikali imepeleka jenereta mpya Mtwara kwa nia thabiti ya kuhakikisha kwamba, yale matatizo ya sasa ya kukatika umeme au ukosefu wa umeme yanadhibitiwa tukingojea upelekaji wa umeme ama kutoa umeme utakaotokana na gesi ya *Mnazi Bay* au hii ya Songosongo ambayo tumewahi kutoa taarifa hapa. Kwa hiyo, Serikali ina nia thabiti na sio kwamba inatoa maelezo ambayo haina uhakika nayo. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, kwa kutoa majibu muafaka ambayo yatawezesha kupatikana kwa umeme na kuwezesha viwanda vya ubanguaji korosho kule Mtwara viweze kuendelea.

Sasa swali la kwanza la Mheshimiwa Namkulala, lilihusu mfuko wa kusawazisha bei. Ni azma ya Serikali na kusema kweli hata katika sera mbalimbali ambazo tunazitoa hapa tunahimiza suala la uanzishaji

wa Mifuko hii mbalimbali ikiwemo Mifuko ya mazao pamoja na huu Mfuko wa kusawazisha bei. Kwa hiyo, ni suala tu la ushirikiano na kuweza kuunganisha nguvu zetu kwa pamoja kuweza kuratibu hii mipango ambayo tunaiandaa ili Mifuko hii iweze kuanzishwa na hatimaye iweze kutumika kwa ajili ya kusawazisha bei ikiwa ni pamoja na zao la korosho.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kuna malalamiko mengi ya wananchi kwamba, hawa wafanyabiashara wanapokuja kununua korosho wanakula njama ya kuhakikisha kwamba wanalipa bei ndogo na wakati huo huo Serikali haifanyi kazi yoyote ya kuweza kuwadhibiti ili kuhakikisha kwamba wanatoa bei halisi. Sasa mimi ninachouliza ni kwamba, Serikali imewahi kufanya upelelezi wa suala hili? Kama imefanya upelekezi, kuna hatua zozote zilizochukuliwa kwa wafanyabiashara wale ambao wanaangusha sana bei ya korosho na wanaungwa mkono na wafanyabiashara wenzao?

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nataka nikumbushe yale niliyosema katika jibu la msingi kwamba, Bodi ya Korosho ina uwezo wa kuwanyima leseni au hata kuwakataza hao wanaokiuka hizi taratibu endapo watakuwa wamebainika. Kwa hiyo, nataka kwanza nisikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali haifanyi lolote, Serikali inafanya jitihada kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, hatua mbalimbali zinachukuliwa, moja ni hiyo kwamba, Bodi ya Korosho inasimamia taratibu na kanuni ili kuweza kuwabaini wale ambao wanakiuka. Suala la kwamba mpaka sasa hivi tutoe mfano wa hatua iliyofikiwa, nataka tu nikumbushe kwamba kwenye kipindi cha mwaka 2001 mimi mwenyewe niliwahi kutembelea Mtwara na tukakutana pamoja na wadau na Mheshimiwa Mbunge akiwepo, tukakubaliana kwamba katika suala hili la hawa wanaokiuka taratibu sio suala la kusema tu kwamba Serikali peke yake ndio inaweza ikawabaini. Tukakubaliana kwamba hili ni jukumu letu sote.

Kwa hiyo, Serikali za Mitaa kule watabainisha watu hawa ambao wanafanya hizi njama hasa hizi *cartel* za kupanga bei ya pamoja wakiifahamisha Serikali, hatua zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kuwanyang’anya leseni kama nilivyokuwa nimesema. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Nilimwona Mheshimiwa Lydia Boma au umeridhika? Kama hujaridhika unayo nafasi. *(Makofi)*

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nilikuwa na swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Serikali hii mara nyingi imekuwa inatamka kwamba, itaanzisha viwanda vidogo vidogo kwa vikundi vya akina mama na vijana, je, mpaka sasa hivi ni vikundi vingapi vimeanzisha miradi ya viwanda vidogo vidogo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, unazo takwimu hizo?

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Serikali imekuwa ikihimiza suala la uanzishaji wa viwanda vidogo vidogo na kama ambavyo tumepata majibu hapa kutoka kwa Waziri wa Viwanda na Biashara asubuhi hii, jitihada za Serikali za kuwahamasisha vikundi vya akina mama pamoja na vijana katika uanzishaji wa viwanda vidogo vidogo, nina hakika ni pamoja na hivi viwanda vya kubangua korosho.

Kwa hiyo, tarakimu kamili siwezi kuwa nazo hapa, isipokuwa nataka niwahakikishie kwamba, Serikali inafanya jitihada za kuhakikisha kwamba hivi viwanda vidogo vya kuwasaidia akina mama na vijana pamoja na kubangua korosho, Serikali inavihimiza na kuvisimamia.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha, tunaendelea na shughuli nyingine. Lakini kabla ya hapo kuna tangazo la Kikao cha Kamati, Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Dr. John Samwel Malecela, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba, kutakuwa na Mkutano leo tarehe 4 Februari, 2004 chumba Na. 58, mara tu baada ya kipindi cha maswali.

Tangazo dogo la nyongeza ni kwamba, Bunge tunayo *web site* yetu. Tulikuwa na moja ikatekwa nyara na watu wengine.  Ndiyo sasa tumepata *web site* mpya, ambayo taarifa zote za Bunge zinaweza kupatikana, *Hansard* zote zinapatikana kwenye *web site*, Sheria zinazopitishwa na Bunge hili zinapatikana kwenye *web site* yetu na taarifa nyingine nyingi nyingi, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge kama mna watu nje ya nchi labda wanauliza uliza habari za Bunge, mnaweza mkawashauri watembelee *web site* ya Bunge, ina taarifa zote.  Mwisho wa matangazo.

## HOJA ZA KAMATI

### Taarifa ya Kamati ya Kanuni za Bunge

**MHE. JUMA J. AKUKWETI - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KANUNI ZA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa idhini yako naomba kutoa taarifa ya Kamati ya Kanuni za Bunge na kuliomba Bunge liridhie kupitisha Azimio la Marekebisho ya Kanuni zake.  Sasa nitalisoma Azimo ambalo naomba mlipitishe.

KWA KUWA kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (2) moja ya majukumu ya Kamati za Bunge ni kufikiria na kutoa mapendekezo juu ya mabadiliko katika Kanuni za Bunge;

NA KWA KUWA Kamati ya Kanuni za Bunge ilikutana Jijini Dar es Salaam  tarehe 19 Januari, 2004 kufikiria mapendekezo ya marekebisho ya Kanuni za Bunge kuhusu masharti ya matumizi ya bendera ya Bunge na Kanuni za Uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika kama inavyoonekana kwenye Kiambatisho Na.1 na kwa kauli moja kupitisha mapendekezo ya marekebisho hayo;

KWA HIYO BASI kwa mujibu wa Kanuni ya 121 (1) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2003, Bunge hili la Jamburi ya Muungano wa Tanzania linalokutana katika Mkutano wake wa 14 linapokea na kuyakubali mapendekezo ya marekebisho katika Kanuni za Bunge, Toleo la 2003 kama inavyoonekana katika Kiambatisho Na.1.

Mheshimiwa Spika, kabla sijawasilisha mapendekezo ya marekebisho ya Kanuni za Bunge, ninaomba kwanza kwa niaba ya wananchi wa Tunduru na mimi mwenyewe, nikutakie wewe Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wote, heri ya mwaka mpya wa 2004. *(Makofi)*

Aidha, pia napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa kwake na Mheshimiwa Rais, kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.  Uteuzi huu unaonyesha imani kubwa aliyonayo Mheshimiwa Rais kwa Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere na ni matumaini yangu kuwa uzoefu na umahiri wake, utatoa mchango mkubwa katika kuzidisha ufanisi wa Bunge kwa faida ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kanuni za Bunge iliketi Jijini Dar es Salaam tarehe 19 Januari, 2004 kujadili mapendekezo ya marekebisho katika Kanuni za Bunge hususan kuhusu masharti ya matumizi ya Bendera za Bunge na uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika *(The Pan African Parliament).*

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wake wa Kamati hii ni hawa wafutao: wewe mwenyewe Mheshimiwa Pius Msekwa, Mwenyekiti, Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Margareth Bwana, Mheshimiwa Frank Maghoba, Mheshimiwa Anne Makinda, Mheshimiwa Philip Marmo, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Sophia  Simba, Mheshimiwa Dr. Wilbroad Slaa na mimi nikiwa Makamu wako wa Kamati hiyo.  *(Makofi)*

Pia Katibu wa Kamati hii ni Ndugu Nenelwa Mwihambi.  Kama nilivyoeleza hapo awali marekebisho haya ya Kanuni za Bunge yanahusu pia kuingiza masharti ya matumizi ya Bendera ya Bunge katika Kanuni zetu za Bunge.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama inavyoonekana katika kiambatisho cha kwanza cha mapendezo ya marekebisho ya Kanuni za Bunge, Kamati inapendekeza kuongeza Kanuni mpya mara moja baada ya Kanuni ya 119 ili kufafanua masharti hayo pamoja na mambo mengine yanayohusiana. Maeneo ambayo Bendera za Bunge zinaruhusiwa kupepezwa. Hapa nilipata taabu, kupepezwa au kupeperushwa, lakini Mheshimiwa Khatibu sijui atasema nini, kupeperushwa? Mheshimiwa Khatibu ni Mtaalam wa Kiswahili ananiambia. Nilipata taabu kupata neno hasa.

Aidha, katika mapendekezo ya Kanuni mpya ya 121 muda wa kupeperushwa bendera unapendekezwa kuwa ni kuanzia saa 12.00 asubuhi hadi saa 12.00 jioni. Hii ni kwa upande wa bendera katika Ofisi za Bunge Dodoma, Dar es Salaam, Zanzibar na nje ya Ofisi ya Mbunge, Ofisi yoyote ya Mbunge nje yake inaweza kukuperushwa Bendera ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa upeperushaji wa bendera wakati wa safari, Kamati inapendekeza kuwa Wabunge waruhusiwe kupeperusha bendera katika magari yao muda wote wa safari hata baada ya saa 12.00 jioni, utaishusha tu ukifika kule unakokwenda.

Mheshimiwa Spika, lengo la kuondoa Miji ya Dodoma, Dar es Salaam na Manispaa ya Zanzibar katika maeneo yanayoruhusiwa kupeperusha Bendera ya Bunge ni kupunguza wingi wa magari yenye bendera katika miji hiyo na hivyo kuepusha kuwachanganya wananchi. Leo tuko zaidi ya 200 kila mmoja na bendera yake huko mjini inaweza kuwa tatizo kidogo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inatoa mapendekezo kuhusiana na matumizi yasiyoruhusiwa ya Bendera ya Bunge kama inavyofafanuliwa katika Kanuni mpya ya 122. Aidha, Bendera ya Bunge itasambazwa na Ofisi ya Bunge katika utaratibu utakaowekwa hivyo, haitaruhusiwa Kampuni au mtu yeyote kutengeneza au kuuza Bendera za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa ufafanuzi naomba nieleze kuwa Waheshimiwa Wabunge kuwa, wana hiari ya kupeperusha Bendera ya Bunge wakati wakiwa katika Mikutano ya Hadhara inayohusiana na majukumu ya Bunge. Mikutano hii ni ile iliyotambuliwa katika Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge ya Mwaka 1988.

Mheshimiwa Spika, Bunge ni chombo kilinachowakilisha wananchi, hivyo hapana budi kiheshimiwe. Aidha, Kamati inaamini kuwa vitendo vyovyote vinavyoonyesha kashfa kwa Bendera ya Bunge vinavyohusiana moja kwa moja na dharau kwa Bunge kama Taasisi hivyo mapendekezo yanatolewa kuwa Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge ya 1988 ifanyiwe marekebisho ili kuingiza vitendo vya kukashifu Bendera ya Bunge kama moja ya makosa yanayostahili adhabu chini ya Sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na marekebisho haya ya kuongeza Kanuni mpya nne mara baada ya Kanuni ya 119, Kanuni za 120, 121, 122 na 123, sasa zinarekebishwa ili zisomeke kuwa Kanuni za 124, 125, 126 na 127.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inapendekeza kuongeza kwa nyongeza ya tano kuhusu Kanuni za Uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika *(Pan African Parliament).*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Mkataba Mdogo wa Mkataba unaoanzisha Jumuiya ya Uchumi ya Afrika kuhusiana na Bunge la Afrika *(Protocol to the Treaty Establishing the African Economic Community), in other words inaitwa The Abuja Treaty Relating to Pan African Parliament.* Kila nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika au *African Union* itawakilishwa na Wabunge watano watakaochaguliwa na Wabunge wa nchi husika kutoka miongoni mwao.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya pili inayohusiana na sifa za Wagombea, Kamati inapendekeza kuwa pamoja na sifa ya Ubunge katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mgombea awe anazimudu kwa ufasaha lugha zinazotumika katika Bunge la Afrika kama zilivyoelezwa katika Ibara ya 17 ya Mkataba unaotajwa awali ambazo ni pamoja na Kiingereza, Kifaransa, Kireno na Kiarabu ili kuhakikisha kwamba atakayewakilisha nchi yetu, ataiwakilisha nchi yetu kikamilifu akizijua lugha moja katika hizo kwa ufasaha ili aweze kufanya mawasiliano

Mheshimiwa Spika, kuhusu taratibu za kupata wagombea, Kamati inatoa mapendezo katika sehemu ya tatu. Aidha, ili kupata idadi ya Wabunge watano wanaohitajika, Kamati imependekeza kuwa wagombea wagawanywe katika makundi manne kama inavyofafanuliwa katika kifungu cha tano (a) yaani kundi la Wabunge Wanawake, Wabunge kutoka Zanzibar, Wabunge wa Kambi ya Upinzani na Wabunge kutoka Tanzania Bara, kundi ambalo litatoa Wabunge wawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza taratibu za uchaguzi kuwa kama zilivyofafanuliwa katika sehemu ya 4 ambapo msimamizi wa uchaguzi au *Returning Officer,* ambaye ni Katibu wa Bunge, atatoa tangazo la siku ya uchaguzi ambayo itakuwa ni katika siku ambazo Bunge linaendesha vikao vyake.

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo mapendekezo ya msingi yaliyotolewa na Kamati yangu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipatia nafasi hii ya kuwasilisha mapendezo ya Kamati. Pia nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati hii kwa ushirikiano na maoni yao yaliyowezesha kukamilisha mapendezo haya ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio yangu kwamba, Waheshimiwa Wabunge wataipokea kwa dhati na kuikubali hoja hiyo iliyopo mbele yenu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja imeungwa mkono na Mheshimiwa Simpasa.

Kama mnavyojua Waheshimiwa Wabunge, hoja zinazoletwa na Kamati hazina Msemaji wa Upinzani wala wa Serikali, huwa tunaingia moja kwa moja kwenye mjadala. Ila nikumbushe kwamba, tulizijadili Kanuni hizi hasa za bendera tangu Mkutano uliopita katika vikao vyetu vya *briefing* na nadhani tukaelewana vizuri. Kwa hiyo, nafikiri hakutakuwa na maneno mengi, lakini ningependa kumshauri mtoa hoja kwamba, kwa kuwa leo ndiyo itakuwa mara ya kwanza, umma wa Tanzania unasikia habari za Bendera ya Bunge, pengine tutakapokwisha kuzipitisha Kanuni, uitishwe mkutano wa Waandishi wa Habari kuitangaza rasmi Bendera ya Bunge ili ijulikane kwa wananchi wote. *(Makofi)*

Naona Mheshimiwa Mahanga ulikuwa na ombi la kuchangia kidogo.

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kweli ni kuchangia kidogo sio zaidi ya dakika tatu, nne.

Mheshimiwa Spika, kwanza nitoe pongezi kubwa sana kwa Kamati yetu ya Kanuni, kwa kazi nzuri ambayo imefanywa na niseme kwamba kwa kweli tumejadili jambo hili kwa muda mrefu, tumekubaliana nami naunga mkono sana suala hili la Bunge au Wabunge kuwa na bendera yao. *(Makofi)*

Hii kwa kweli inatupatia heshima kubwa sana na kuonyesha kwamba sisi ni nguzo katika nguzo ambazo zinaongoza Taifa hili. Ninalotaka kusema dogo ni hili la kutopeperusha bendera Dar es Salaam, Dodoma na Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sababu iliyotolewa kwamba zitakuwa nyingi kwa sababu maeneo haya mara nyingi vikao vya Kamati au vya Bunge vinafanyika, zinaweza zikawa ni sababu nzuri. Lakini tungelingalia vizuri na hasa kama kweli tunasema kwamba bendera zitakuwa nyingi Wabunge tukiwa Dar es Salaam huwa tunapeperusha bendera, basi angalau wale wa Majimbo yale ya Dar es Salaam, Dodoma na Zanzibar waruhusiwe. *(Makofi)*

Mimi nadhani kama Waheshimiwa Wabunge watakuwa Dar es Salaam, wote wakawa hawakupeperusha lakini mimi nikapeperusha kwa sababu niko Jimboni kwangu, nadhani itaeleweka. Sasa kwa kweli sioni kabisa sababu sisi ambao tuko katika miji hiyo kunyimwa ile nafasi tunapopita kwenye kwenye Majimbo yetu watutatumbue kwamba huyo ndiyo Mheshimiwa Mahanga na ndiyo yuko kwenye

Jimbo lake la Ukonga, Dar es Salaam akiwa anapeperusha bendera. Mimi hilo tu nilitaka niliseme, liangaliwe hilo kwa kuwa-*exempt* wale wenye Majimbo, si wengi wenye Majimbo kwenye maeneo hayo matatu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nadhani nimepata ombi lingine kutoka kwa Mheshimiwa Dr. Msekela, unaweza kuchangia.

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ingawa nilichelewa kidogo kuomba. Nami nilitaka kulizungumzia hilo hilo ambalo Mheshimiwa Dr. Mahanga amemaliza kulizungumaia. Kwa kweli kama hii ni Bendera ya Bunge, kwa ajili ya kuwatambulisha Wabunge, basi ni vema ikafanya hivyo.

Sasa mji mkubwa kama Dar es Salaam kwa kweli ni tofauti kwa mfano na mji kama Dodoma. Tuseme Dar es Salaam na Zanzibar ni tofauti na Dodoma. Dodoma unaweza kumvumilia Mheshimiwa Saggaf, akapeperusha peke yake. Lakini kwa Dar es Salaam ukisema Mheshimiwa Simba apeperushe Ilala tu peke yake na Mheshimiwa Dr. Mahanga na kadhalika utakuwa unawapa tabu kubwa sana.

Lakini ukisema pia wasipeperushe ina maana hawatapeperusha kamwe hizi bendera. Labda kama watakuwa wanatoka Dar es Salaam kuja Dodoma kwa shughuli za Bunge hapa. Kwa hiyo, ni haki tu kama alivyosema Mheshimiwa Mahanga kwamba, Wabunge hawa wa Dar es Salam, kwa sababu ya Jiografia ya Mji wenyewe ulivyo, wapewe nafasi ya kupeperusha, lakini inategemea kwa sababu watafanya hivyo pale inapobidi wafanye hivyo, kwamba tuwapatie *descretion* kwamba hawatafanya mahala ambapo hawalazimiki kufanya, kupeperusha bendera hata kama anakwenda kupata moja, mbili, jioni nafikiri hawatapeperusha.

Mheshimiwa Spika, nafikiri nimeeleweka. Haja yangu ni hiyo tu. Ni kwamba tujaribu kuona kwamba matumizi ya bendera hii yanawafikia hata wale ambao wako kwenye hii miji mikubwa, hususan Dar es Salaam na Zanzibar.

Kwa Dodoma kwa kweli sikuwa na wasiwasi kwamba Mheshimiwa Saggaf lazima kwa kweli atapeperusha bendera tu hapa. Ahsane sana. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, mimi nitachukua muda mfupi tu. Kwanza, nampongeza Makamu Mwenyekiti kwa kuwasilisha hoja. Katika maelezo ya Makamu Mwenyekiti na Naibu Spika alisema kwamba, isipokuwa kwamba Mbunge hatapepea bendera kwenye gari lake atakapokuwa Dodoma, Dar es Salaam na kwa mujibu wa Waraka huu na Zanzibar.

Katika maelezo amesema Manispaa ya Zanzibar. Sasa akisema Zanzibar maana yake ni Unguja na Pemba na katika maelezo amesema ni Manispaa ya Zanzibar. Nafiri angetufafanulia ni Manisfaa ya Zanzibar au ni Zanzibar. Ukisema Zanzibar maana yake ni Unguja na Pemba kwamba sote kule hatutaruhusiwa kupepea bendera. Tulitaka ufafanuzi huo. Ahsante.

**SPIKA:** Mtoa hoja wamekwisha wachachangiaji? *(Kicheko)*

**MHE. MOHAMED ABDULLY ALY:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kuniona na kunipa ruhusa. Ingawa imeshasemwa lakini naomba kurudia kusema tena, sirudii yale yale nitasema kwa namna nyingine maana kurudia hairuhusiwi.

Zanzibar ni kisiwa kidogo sana. Ni kisiwa kidogo, vimo visiwa vingi tu. Watu wanajua Unguja na Pemba lakini kuna Tumbatu, kisiwa vile vile kule. Hofu niliyoipata mimi ni kwamba sisi Zanzibar, Wabunge hatutafaidika na ladha nzuri na rangi nzuri ya Bendera yetu ya Bunge kwa sababu hatatuweza kupeperusha bendera hiyo tukiwa katika Manispaa ya Zanzibar.

Sisi tupo ndani ya Manispaa ya Zanzibar, lakini wengine Mfenesini wako nje ya Manispaa. Kwa tafsiri sahihi kwa hii Manisapaa wao wataweza kuteremsha. Hatuna Ofisi, hatutaweza kupeperusha

Bendera ya Bunge. Vile vile hatutaweza kuweka juu ya meza kwa sababu hatuna Ofisi, sasa hatutafaidika katika gari, hatutafaidika katika Ofisi, hatutafaidika katika meza, sasa bendera hiyo ukitupa sisi uturuhusu tukashone mashati, kwa sababu hatutaitumia mahala popote? Kwa hiyo, naomba rasmi Zanzibar muifikirie tena kwa sababu bendera na sisi tuna haja nayo kama wenzetu. *(Makofi)*

Zanzibar katika Manispaa tuko Wabunge 13 kama sikosei. Rais anapeperusha bendera kule na Waziri Kiongozi. Kwa hiyo, naomba na sisi mturuhusu tufaidike. Tukienda kule angalau tuwe nayo bendera.

Pili, ninaloliomba kuhusu hizi lugha ambazo ambazo zitatumika huko katika Bunge la Afrika, nilivyosikia zamani, sina hakika kama ni Kiswahili kimekubalika kule, sina hakika lakini na Kiswahili kama kimekubalika kitumike kule. Kwa hiyo, hapa kama kimekubalika huko ni sawa. Naomba na hapa tusije tukatumia Kiingereza tu. Maana yake wenzetu Wafaransa huko wakienda kwao wanatumia Kifaransa, Waingereza wanatumia Kiingereza. Iwe sisi Watanzania lazima tutumie Kiingereza, kwa nini lugha yetu tusiitumie? Kwa hiyo, naomba na hilo lifikiriwe, kama imekubaliwa huko lugha yetu, tupewe nafasi na sisi hapa tuweze kuitumia tusiwe kuulizwa hapa tukaja kubabaika. Naomba nafasi hiyo tupewe.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache nakushukuru. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JUMA J. AKUKWETI - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KANUNI ZA BUNGE:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza napenda kuwashukuru sana wale Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia, wengine wamechagia kwa maandishi haraka, wengine wamechangia kwa kusema, sasa naomba niwataje, Mheshimiwa Makongoro Mahanga, Mheshimiwa Dr. James Msekela, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mheshimiwa Mohamed Abdully Ally. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja za Waheshimiwa hawa Wabunge wote ni nzito na kama utakumbuka vizuri wakati unakiongoza kikao kile hizi ndizo hoja ambazo zilijitokeza hata kwenye Kamati. Zilijitokeza sana na zikachambuliwa sana. Hazikuwekwa kwenye mapendekezo si kwa sababu hazikuwa hoja nzito, hoja hizi zilikuwa nzito wote waliziona, lakini ulikuwa unaangalia namna ya kufanya kwamba hasa kwa sisi Wabunge, mimi natoka Tunduru, mwingine anatoka Tarime, mwingine kwingineko. Wote tukikusanyika hapa tukapeperusha hapa, Kamati yenu ikafirikia ni kweli ni nyingi mno.

Sisi wanachama wa Chama wa Chama Mapinduzi najua mnakumbuka tumeruhusiwa kupeperusha Bendera ya Chama cha Mapinduzi, lakini sioni watu wanapeperusha. Ni kwa sababu tu naona kama jamani kila mtu akianza kupeperusha hapa zitakuwa nyingi sana. Lakini hakuna aliyekwambia usipeperushe. Sasa hii ni kwa sababu ni bendera ya Serikali, Kamati ilidhani ni vizuri jambo hili likaangaliwa kwa makini. Hata hivyo, hoja ambayo Mheshimiwa Makongoro Mahanga, ameisema na wengine kwamba, je, anapokuwa Ukonga mle Jimboni kule ndani Kiwalani, unapopitapita ufanyefanyeje?

Mheshimiwa Spika, sasa nadhani utalitazama hilo, utakaa kwa wale wanaotoka maeneo yale, anapopita Jimboni mwake mle kwa wapiga kura wake, basi wasiseme kwamba Mbunge wetu ndiyo huyu. Itabidi liangaliwe.

Nikubali tu kwamba, limepokelewa, Kamati ni ya watu wengi Mheshimiwa Spika, ndiyo kiongozi wetu, watalitazama kwa uzito ambao umelileta na kwa sababu wote ndio mmelileta, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, hoja yake ile ile lakini akataka ufafanuzi je, Zanzibar yote kwa maana na Pemba, ukikaa Konde kule usipeperushe, ukiwa Makunduchi usipeperushe. Nadhani nia haikuwa hiyo hasa, ni kwa sababu wote tutakuwa pale. Wote tutakwenda pale, patakuwa na *over crouding* kubwa. Kwa hiyo, nadhani ndiyo nia ya Azimio lenyewe.

Mheshimiwa Spika, moja ambalo amelisema Mheshimiwa Mohamed Abdully Ally, suala la lugha za kutumia. Kama mnavyofahamu wote Waheshimiwa Wabunge, mnafahamu uwezo wa kujenga hoja ni lugha. Lugha ukiiweza ni nyepesi kujenga hoja. Kwa hiyo, Kamati ilidhani ni vizuri kwamba awe anaijua lugha. Si lazima uwe na lugha ya *Shakespear* hata kidogo. Lugha ambayo unaweza ku-*communicate* vizuri, ukawa *comfortable* na wenzako, uifahamu hiyo lugha.

Sasa nimezungumza juu ya Kiswahili mpaka sasa tunavyoongea bado Kiswahili siyo lugha ya lile Bunge. Bado siyo lugha ya lile Bunge. Lakini naamini Serikali inafanya jitihada kukisukuma Kiswahili katika maeneo mbalimbali ya mawasiliano katika Afrika ili nacho kiwepo. Lakini mpaka hivi sasa bado lugha ni zile ambazo nimezitaja, Kireno, Kiingereza, Kifaransa na Kiarabu, ndizo lugha za Bunge lile. Kwa hiyo, ni vizuri Wajumbe wetu tunapowapeleka wawe lugha zile wanazifahamu. Unaweza kuwa na bahati ukajua Kiarabu na Kiingereza, hiyo bahati yako, ukawa unafamu Kifaransa na Kiingereza ni bahati yako. Lakini bado lugha moja ukiifahamu kwetu sisi inatosha. Kiswahili tutaendelea kuomba Mungu kama kitakubaliwa au hapana kwa siku za baadaye.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, naomba nichukue nafasi hii kuwatakia kheri wale wote wanaogombea kupata nafasi ya kutuwakilisha kule Bunge la Afrika na kuwatakia mafanikio mazuri. Naamini kampeni zitakuwa zile za kawaida za kiungwana maana sisi ni familia moja kama wote mnavyofahamu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kabla sijawahoji labda niongeze tu kidogo. Tafsiri aliyoitaja Zanzibar, maneno aliyotumia mtoa hoja ndiyo sahihi. Ni Manispaa ya Zanzibar nzima, ni Manispaa ya Zanzibar.

La pili, niseme tu kwamba, kwa kuwa hii ni hoja ya Kamati, mtoa hoja asingeweza kuji-*commit* kwamba, tuliyoyasikia yatatekelezwa. Itabidi mawazo yaliyotolewa yarudi kwenye Kamati yakafikiriwe tena na Kamati na utaratibu wetu ni kurekebisha Kanuni kila tunapoona inafaa kufanya hivyo.

Kwa hiyo, nashauri Bunge likubali mapendekezo kama yalivyokuja wakati mawazo yaliyotolewa yanaendelea kufikiriwa na Kamati na yanaweza yakaletwa wakati mwingine baadaye.

Sasa tuiamue hoja ya Kamati ya Kanuni za Bunge.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Kanuni za Bunge ilipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Hoja imeafikiwa, mapendekezo yamepitishwa na sasa yatakuwa sehemu ya Kanuni zetu.

## HOJA ZA SERIKALI

## MAAZIMIO

### Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Nasaba za Mimea kwa ajili ya Kilimo na Chakula wa Mwaka 2001 uitwao *" The International Treaty on Plant Genetic Resources for Food and Agriculture, 2001"*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hiki ni kikao chetu cha kwanza, nakuomba uniruhusu nikutakie wewe, Waheshimiwa Wabunge na Bunge lako Tukufu, kheri na fanaka katika mwaka huu mpya wa 2004. Ninaomba pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana ndugu yetu Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa kujiunga na sisi. Tunamkaribisha kwa mikono miwili na tunamhakikishia ushirikiano wetu wakati wowote atakapouhitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likubali kuridhia Mkataba wa Nasaba za Mimea kwa ajili ya Kilimo na Chakula unaojulikana kwa Kiingereza kama *The International Treaty on Plant Genetic Resources for Food and Agriculture, 2001.* Naomba niishukuru sana Kamati ya Kilimo na Ardhi, kwa kuupitisha Mkataba huu wakati wa Mkutano wa Kumi na Tatu na

Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Eliachim Simpasa, nina hakika atapata nafasi ya kutoa maoni ya Kamati mbele ya kikao hiki.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni miongoni mwa nchi chache duniani zenye utajiri mkubwa wa nasaba anwai za mimea *(Plant Genetic Diversity).* Baadhi ya nasaba hizo zimekuwa zikichukuliwa na Taasisi na nchi mbalimbali bila kuwepo na Mikataba au utaratibu wa kisheria ambao ungeiwezesha nchi yetu kufaidika na nasaba hizo.

Mheshimiwa Spika, nasaba za mimea ni viasilia vya jeni *(gene),* (tumepata tatizo sana kutafsiri *gene* katika lugha ya Kiswahili), ambavyo vinaweza kuwa katika hali ya seli moja moja, mkusanyiko wa seli *(tissue),* vipando *(cuttings)* mbegu au mimea mizima mizima, vyenye matumizi halisi au yanayotarajiwa *(actual or potential use).* Mimea hiyo inaweza kuwa ni ile inayotumiwa na binadamu na mifugo au jamii zake ambazo bado ziko maporini hazijaanza kufugwa na binadamu. Aidha, matumizi ya nasaba za mimea hiyo yanaweza kuwa ya kilimo na chakula, kutengeneza viuatilifu, dawa za binadamu na mifugo, kemikali za viwandani, mapambo au kutunza mazingira.

Mheshimiwa Spika, jeni za mimea na viumbe vingine, ndizo zinazofanya viumbe hivyo au mimea hiyo iwe na sifa maalum za maumbile au tabia. Kwa mfano, kuwa na ukinzani dhidi ya magonjwa, kuzaa mbegu, majani, matawi na kadhalika kwa wingi. Katika uzalishaji wa mimea mipya *(breeding)*, wanasayansi hujitahidi kuhamisha jeni zinazofanya kiumbe fulani kuwa na sifa maalum kutoka kwenye kiumbe hicho na kuzihamishia kwenye kiumbe kingine ili kukifanya kiumbe hicho kingine kijumuishe sifa hizo miongoni mwa sifa zake.

Katika kilimo na ufugaji, kuna mifano mingi ya uhamishaji wa jeni kutoka mmea mmoja kwenda kwenye mmea mwingine na hivyo hivyo kwa mifugo. Kwa mfano, mwaka wa 1937 jeni za mhogo pori wa Tanzania *(Manihot Glaziovii)* zilihamishiwa kwenye mhogo wa kawaida ili kuufanya uwe na ukinzani dhidi ya ugonjwa wa batobato ya mhogo *(Cassava Mosaic Virus Disease).* Kazi hiyo ilifanywa kwenye Kituo chetu cha Utafiti wa Kilimo cha Amani kilichoko Tanga. Aidha, jeni kutoka kwenye mpunga pori wa Tanzania *(Oryza Barthii* na *Oryza Brachyantha),* zilihamishiwa kwenye mpunga wa Japan na wa nchi nyingine mbalimbali ili kuupa uwezo wa kujikinga na athari za wadudu waharibifu wa majani ya mpunga waitwao *Brown Leaf Hoppers.*

Mheshimiwa Spika, juhudi za Serikali za kulinda utajiri wa nchi na mimea zilianza kwenye miaka ya 1980 Tanzania ilipojiunga na Mkataba wa Hiari wa Kimataifa wa Nasaba za Mimea chini ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo *(FAO)* uitwao *The International Undertaking on Plant Genetic Resources for Food and Agriculture, 1983.* Mwaka wa 1992 Tanzania ilishiriki katika majadiliano ya Rio yaliyozaa Mkataba wa Kimataifa wa Bioanwai *(The Convention on Biological Diversity, 1992)* na hatimaye kuuridhia Mkataba huo mwaka wa 1996. Mkataba wa Kimataifa wa Bioanwai unahusu hifadhi, matumizi endelevu na mgawanyo wa usawa na haki wa manufaa yatokanayo na matumizi ya Bioanwai.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Bioanwai ulibadilisha mfumo wa zamani uliozingatia matumizi ya Bioanwai kama urithi wa pamoja na kuruhusu kila nchi kutumia mamlaka yake ya dola na mikataba kati ya nchi moja na nyingine *(Bilateral Agreements)* ya kulinda na kusimamia matumizi ya Bioanwai (zikiwemo nasaba za mimea) zilizoko ndani ya mipaka yake. Hata hivyo, kutokana na umuhimu wa nasaba za mimea kwa ajili ya kilimo na chakula, mwaka wa 1994 Jumuiya ya Kimataifa iliona haja ya kushirikiana katika kuhifadhi, kuhimiza matumizi endelevu na kurahisisha ubadilishanaji wake bila kulazimika kuwakeana mikataba kati ya nchi moja na nyingine. Azma hiyo ilitekelezwa kwa kurekebisha Mkataba wa Hiari wa Kimataifa wa Nasaba za Mimea wa mwaka wa 1983 ili uwe na nguvu za kisheria na uwiane na Mkataba wa Kimataifa wa Bioanwai wa mwaka wa 1992, hususan mgawanyo na manufaa yatokanayo na matumizi ya nasaba za mimea kwa ajili ya kilimo na chakula kwa usawa na kwa haki.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa nasaba za mimea kwa ajili ya kilimo na chakula, kati ya mwaka wa 1994 na mwaka 2001, Tanzania ilishiriki kikamilifu katika majadiliano

yaliyosababisha kufikiwa kwa makubaliano ya Mkataba wa Kimataifa wa Nasaba za Mimea kwa jaili ya Kilimo na Chakula, ambao unawasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu umegawanyika katika sehemu saba na una vifungu yaani *articles* 37 na nyongeza 2.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya kwanza inaainisha lengo kuu la Mkataba, ambalo ni kuhifadhi, kuhimiza matumizi endelevu na kugawana kwa usawa na haki, manufaa yatokanayo na matumizi ya nasaba za mimea kwa ajili ya kilimo na chakula. Aidha, madhumuni makuu ya Mkataba ni kuweka utaratibu utakaoziwezesha nchi zinazoendelea ambazo ni chimbuko la sehemu kubwa ya nasaba za mimea asilia, kunufaika na matokeo ya uendelezaji wa nasaba hizo utakaofanywa na nchi zilizoendelea.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ya Mkataba inayojumuisha Ibara ya nne hadi ya nane, inazungumzia mambo muhimu yanayopaswa kuzingatiwa, hususan katika maeneo mawili yafuatayo:-

(i) Mbinu zinazopaswa zizingatiwe katika kuhifadhi na kuhimiza matumizi endelevu ya nasaba za mimea kwa ajili ya kilimo na chakula; na

(ii) Utaratibu wa kuhamisha nasaba za mimea kutoka nchi ambazo ni asili ya nasaba za mimea hiyo kwenda nchi zinazotaka kuendeleza nasaba hizo.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu ya Mkataba inahusu haki za wakulima. Chini ya Ibara ya 9, Mkataba unatambua mchango wa wakulima wote wa ulimwenguni na hasa wakulima wadogo katika kuhifadhi na kuendeleza nasaba za mimea kwa ujumla, hususan katika kulinda elimu ya jadi, kushiriki katika maamuzi yanayohusu nasaba za mimea na kunufaika kutokana na matumizi ya nasaba za mimea kwa ajili ya kilimo na chakula, kama yatakavyoainishwa katika sheria ambayo baadaye tutaomba Bunge hili Tukufu liitunge

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne ya Mkataba inayojumuisha Ibara ya 10 hadi ya 13 inahusu Mfumo wa Kimataifa wa kubadilishana na kunufaika na nasaba za mimea kwa ajili ya kilimo na chakula, yaani *Multilateral System of Access and Benefit Sharing.* Mazao yatakayohusika chini ya mfumo huu yametajwa katika Kiambatanisho Na. 1 cha Mkataba huu ambacho mmekwishagawiwa. Mazao yaliyowekwa kwenye Kiambatisho hicho ni yale yaliyokubaliwa na wanachama wa *FAO* kuwa ni muhimu kwa ajili ya usalama wa chakula duniani. Aidha, mazao mengine yataongezwa kwenye orodha hiyo na Baraza la Wanachama baada ya kuridhika kuwa yana manufaa kwa wanachama wote.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya nasaba za mimea chini ya mfumo huu yatakuwa kwa ajili ya hifadhi, utafiti na mafunzo. Aidha, kwa mujibu wa Ibara ya 20, kubadilishana nasaba za mimea kutafanyika kwa kutumia Mkataba maalum wa pamoja wa uhamishaji wa nasaba za mimea *(Material Transfer Agreement),* utakaopitishwa na Mkutano wa kwanza wa wanachama. Mfumo wa Kiamtaifa wa kubadilishana na kunufaika na nasaba za mimea utakuwa na manufaa yafuatavyo kwa nchi yetu:-

(i) Kurahisisha upatikanaji wa nasaba za mimea kutoka kwa nchi wanachama;

(ii) Utawezesha kubadilishana taarifa zinazohusu nasaba za mimea kwa ajili ya kilimo na chakula;

(iii) Utawezesha kupatikana teknolojia kutoka nchi zilizoendelea ambazo ni wanachama wa Mkataba huu;

(iv) Utawezesha kujenga uwezo wa kuhifadhi na kutumia nasaba za mimea kwa ajili ya kilimo na chakula;

(v) Utawezesha kugawana kwa usawa na haki manufaa yatokanayo na matumizi ya kibiashara ya nasaba za mimea kwa ajili ya kilimo na chakula; na

(vi) Utawezesha kunufaika na matumizi ya nasaba za mimea zilizochukuliwa na nchi au taasisi za Kimataifa kabla ya Mkataba huu kutiwa saini.

Mheshimiwa Spika, chini ya sehemu za tano na sita, Mkataba unatambua na kuweka mkazo katika utekelezaji wa Mpango Kamambe wa Uendelezaji Nasaba za Mimea wa Mwaka 1996 *(The Global Plan of Action for Conservation and Sustainable Utilization of Plant Genetic Resources for Food and Agriculture, 1996).* Chini ya Ibara ya 18, nchi wanachama wataweka mkakati wa kupata fedha kwa ajili ya kutekeleza mpango huo na kuweka utaratibu wa kugharamia mipango ya Kitaifa inayohusu nasaba za mimea kwa ajili ya kilimo na chakula, hasa katika nchi zinazoendelea.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya saba ya Mkataba ambayo inajumuisha Ibara ya 19 hadi ya 35, inahusu masuala ya kitaasisi na taratibu za kuwa wanachama. Mkataba huu ulikuwa wazi kwa ajili ya kusainiwa kuanzia tarehe 3 Novemba, 2001 hadi tarehe 4 Novemba, 2002. Kwa mujibu wa Ibara ya 27, nchi ambazo zilichelewa kuusaini zinatakiwa kuomba ruhusa ya kuwa wanachama yaani kuomba *accession* kwa Mkataba huu. Aidha, chini ya Ibara ya 28, Mkataba utaanza kufanya kazi baada ya nchi 40 kuwasilisha nyaraka zake za kuuridhia au kuomba uanachama, yaani kuomba *accession*. Hivi sasa jumla ya nchi 32 zimekwisha kuridhia Mkataba huo.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu Tanzania ikawa miongoni mwa nchi hizo 40 wanachama wa kwanza ili iweze kushiriki katika kutunga kanuni za utekelezaji wa Mkataba huo. Kwa mujibu wa Ibara ya 21 ya Mkataba, kikao cha kwanza cha Baraza la wanachama kitahusika na uandaaji wa taratibu na kanuni za Baraza. Aidha, kikao hicho kitajadili na kupitisha Mkataba wa Kuhamisha Nasaba *(Material Transfer Agreement)*. Mkataba huo, pamoja na mambo mengine, utaainisha haki na wajibu wa nchi wanachama katika uhamishaji wa nasaba za mimea. Kwa hiyo, tungependa tuwepo katika kikao hicho.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa Mkataba wa Kimataifa wa nasaba za mimea kwa Tanzania, hususan katika maendeleo ya kilimo na katika kuhakikisha kuwepo kwa uhakika endelevu wa upatikanaji wa chakula, kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Serikali inaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Nasaba za Mimea wa Mwaka 2001, uitwao *The International Treaty on Plant Genetic Resources for Food and Agriculture, 2001* na hivyo kuiruhusu Tanzania iwe mwanachama wa Mkataba huo kwa kupitisha Azimio lifuatalo:-

KWA KUWA Tanzania ni mwanachama wa Mkataba wa Kimataifa wa Bioanwai wa Mwaka 1992 *(The Convention on Biological Diversity, 1992)* tangu mwaka wa 1996;

NA KWA KUWA Mkataba wa Kimataifa wa Nasaba za Mimea kwa Ajili ya Kilimo na Chakula wa Mwaka 2001 unalenga katika kutekeleza Mkataba wa Kimataifa wa Bioanwai wa Mwaka 1992 kwa kuweka utaratibu wa kuhifadhi na kuhimiza matumizi endelevu ya nasaba za mimea na kuhakikisha kwamba nasaba hizo zinavunwa kwa madhumuni ya kuendeleza kilimo na zinatumiwa kwa haki na usawa;

NA KWA KUWA Tanzania ina utajiri mkubwa wa nasaba anwai za mimea na imekuwa na bado ina nia ya kulinda na kunufaika na utajiri huo kwa kushiriki kikamilifu katika majadiliano yaliyowezesha kuwepo kwa Mkataba wa Kimataifa wa Nasaba za Mimea kwa ajili ya Kilimo na Chakula wa mwaka 2001;

NA KWA KUWA kuridhia Mkataba huo kutaiwezesha Tanzania:-

(a) Kusimamia matumizi na hifadhi ya nasaba za mimea yetu;

(b) Kutunga na kutekeleza sheria ya kudhibiti uhamishaji haramu wa nasaba hizo;

(c) Kuimarisha utafiti wa mazao kwa kupata teknolojia sahihi na nasaba za mimea kutoka nchi za nje bila kulazimika kuwekeana mikataba na nchi moja moja;

(d) Kunufaika na matumizi ya nasaba za mimea zilizochukuliwa na nchi au taasisi za Kimataifa kabla ya Mkataba huu;

(e) Kunufaika na fedha za kugharamia utekelezaji wa Mpango Kamambe wa Kimataifa wa Nasaba za Mimea; na

(f) Kutambulika kwa haki za wakulima wa Tanzania ambao ni wachangiaji wakubwa katika kulinda na kuhifadhi mimea yetu.

KWA HIYO BASI kwa kuzingatia umuhimu na faida ambazo Tanzania itapata kutokana na kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Nasaba za Mimea kwa ajili ya Kilimo na Chakula wa Mwaka 2001, Bunge hili katika Mkutano wake wa Kumi na Nne, kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, sasa linaazimia kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Nasaba za Mimea kwa ajili ya Kilimo na Chakula wa Mwaka 2001 *(The International Treaty on Plant Genetic Resources for Food and Agriculture 2001).*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. EDWARD N. NDEKA (k.n.y. MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, Mheshimiwa Mwalimu Eliachim Simpasa, naomba kutoa maoni ya Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi kuhusu Azimio la kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Nasaba za Mimea kwa ajili ya Kilimo na Chakula wa 2001 uitwao *The International Treaty on Plant Genetic Resources for Food and Agriculture.*

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa niaba ya Wajumbe wote wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni ya Kamati kuhusu Azimio la Mkataba wa Kimataifa wa Nasaba za Mimea kwa ajili ya Kilimo na Chakula wa Mwaka 2001 uitwao *The International Treaty on Plant Genetic Resources for Food and Agriculture.*

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu uliipangia kazi ya kuchambua Azimio la Mkataba wa Kimataifa wa Nasaba za Mimea kwa ajili ya Kilimo na Chakula kwa mujibu wa kanuni ya 88(9) Toleo la mwaka 2003. Kamati ilikutana Dodoma tarehe 11 Novemba, 2003 na kutekeleza jukumu hilo. Aidha, maoni ya Kamati kuhusu Azimio la Mkataba huu sasa nayatoa kwa mujibu wa Kanuni ya 70(2). Lakini kabla sijafanya hivyo, napenda kuwatambua Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wajumbe wa Kamati hii, waliochambua na kutoa mchango mkubwa kuhusu Azimio la Mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe hao ni Mheshimiwa Eliachim J. Simpasa, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Makamu wa Mwenyekiti, Mheshimiwa Anatory Choya, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Robert K. Mashala, Mheshimiwa Paul Makolo, Mheshimiwa Masoud Abdulla Salim, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Musa A. Lupatu, Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar, Mheshimiwa Joel N. Bendera, Mheshimiwa Edward N. Ndeka, Mheshimiwa Gwassa A. Sebabili, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Salama Khamis Islam, Mhesimiwa Abdillahi O. Namkulala, Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha na Mheshimiwa Philip Magani.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaunga mkono hoja ya Serikali ya kuleta Azimio la Mkataba unaolenga katika kuhifadhi, kuhimiza matumizi endelevu na kugawa kwa usawa, haki na manufaa yatokanayo na matumizi ya nasaba za mimea kwa ajili ya kilimo na chakula. Aidha, Kamati imeridhika

kuwa madhumuni ya Mkataba ambao ni kuweka utaratibu utakaoziwezesha nchi zinazoendelea ambazo ni chimbuko la sehemu kubwa ya nasaba za mimea asilia kunufaika na matokeo ya uendeshaji wa nasaba hizo unaofanywa na nchi zilizoendelea, yana manufaa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja, Kamati inapendekeza kutoa maoni mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Azimio la Mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua ukweli kwamba, nchi yetu ina utajiri mkubwa wa nasaba za mimea hasa kwenye maeneo ya safu za milima ya Mashariki *(The Eastern Arch Mountains).* Hivyo, Kamati inasisitiza kwamba, kuna haja kwa Serikali kuhakikisha kwamba mkazo unawekwa katika kulinda na kuhifadhi nasaba za mimea yetu kwa ujumla na hasa nasaba zile ambazo zinapatikana hapa Tanzania peke yake.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini ukweli kwamba, Mkataba umeorodhesha mimea michache iliyoko Tanzania ili ilindwe chini ya Mkataba huu. Kamati inakubaliana na maelezo ya Serikali kwamba, kuna umuhimu wa kuwa makini katika kuweka chini ya Mkataba, mimea inayopatikana hapa Tanzania peke yake.

Ili kuipa Serikali nafasi ya kuweka masharti ya manufaa ya kunufaisha mimea hiyo katika makubaliano na nchi moja moja. Hata hivyo, ili kuhakikisha kuwa kunakuwepo na udhibiti wa kutosha na ili kunufaika ipasavyo na Mkataba huu, Kamati inaishauri Serikali iandae na kuleta sheria Bungeni, itakayosimamia hifadhi na matumizi endelevu ya nasaba zetu za mimea.

Aidha, ili kufanikisha azma ya kuendeleza nasaba za mimea, Kamati inaishauri Serikali kuunda chombo mahususi cha kusimamia na kutekeleza masuala yote ya nasaba za mimea ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa Mkataba huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati pia imebaini kuwa Mkataba wa Kimataifa wa Nasaba za Mimea kwa ajili ya Kilimo na Chakula una umuhimu wa pekee kwa Tanzania, hususan katika kuongeza usalama wa chakula na utafiti wa kilimo kwa kunufaika na mimea ya nchi nyingine wanachama iliyoorodheshwa kwenye Mkataba bila ya gharama yoyote.

Aidha, kwa kujiunga na Mkataba huu, Tanzania inaweza kupata teknolojia, mafunzo na matokeo ya utafiti kutoka kwa wataalamu wa nchi nyingine wanaotumia mimea hiyo.

Mheshimiwa Spika, awali Kamati ilihoji ikihofia uwezekano wa kuhusisha masuala ya mazao yaliyorekebishwa ki-*genetic (GMOs)* katika Mkataba huu. Hata hivyo, Kamati imeridhika na maelezo ya Serikali kwamba, Mkataba huu haulengi masuala ya *GMOs* bali unalenga kuhakikisha kwamba kunakuwepo na matumizi endelevu ya nasaba za mimea ya kilimo na chakula kutokana na uendelezaji wa utafiti katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhika kwamba, Mkataba katika Ibara ya 9 unatambua haki za wakulima. Kutokuzuiwa kutunza mbegu kutoka mazao yao wenyewe, kuheshimu na kulinda elimu ya jadi ambayo imekuwa ikitumika kwa miaka yote, kulinda na kuhifadhi mimea, kurudishiwa sehemu ya mrahaba utakaopatikana kutokana na matumizi ya nasaba za mimea kutumiwa kibiashara kwa utaratibu utakaowekwa na Sheria za nchi. Kusaidiwa wakati wa majanga makubwa kwa kupatiwa mbegu nje ya utaratibu wa kawaida ili waweze kuendeleza uzalishaji wa chakula na kuendelea kutunza nasaba za mimea yao ya asili kwa njia asilia.

Hata hivyo, Kamati ina wasiwasi kwamba, Mkataba huu hauonyeshi haki hizo za wakulima zitalindwaje. Mkataba umeziachia nchi wanachama kuchukua jukumu la kutunga sheria ya kuweka utaratibu wa kulinda haki hizo za wakulima. Kwa kuzingatia hili, Kamati inasisitiza kuwa Serikali ifanye haraka kuandaa na kuleta Bungeni Muswada wa Sheria ya kulinda na kusimamia matumizi endelevu ya nasaba zetu utakaohakikisha kwamba haki za wakulima zinalindwa ipasavyo na sheria.

Aidha, sheria hiyo ianzishe Mfuko wa kuwasaidia wakulima kunufaika na haki zao zilizoainishwa katika Mkataba huu na sheria nyingine za nchi zinazogusia nasaba za mimea. Chanzo kimojawapo cha fedha za Mfuko huu kiwe ni fedha zinazotolewa kutokana na matumizi ya nasaba hizo kibiashara, pamoja na michango ya hiari ya nchi wanachama.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhika kuona kwamba, Mkataba unaweka utaratibu wa Tanzania kunufaika na nasaba za mimea yake zilizochukuliwa na nchi na Taasisi mbalimbali za Kimataifa. Aidha, Kamati inaishauri Serikali iweke utaratibu mzuri wa kuainisha nasaba za mimea yetu yote, iweke utaratibu mzuri na ianze kutekeleza kwa haraka iwezekanavyo mara baada ya Mkataba huu kuridhiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Kamati inaridhika kuwa kwa kuridhia Mkataba huu, nchi, wakulima na wataalamu wetu, watanufaika kwa kupata teknolojia na mafunzo kutoka kwa nchi wanachama hususan kupitia Mpango wake Kamambe wa Kimataifa wa Hifadhi na Matumizi Endelevu ya Nasaba za Mimea kwa ajili ya Kilimo na Chakula, kama sheria ya utekelezaji wa Mkataba huu itatungwa.

Kuridhiwa kwa Mkataba peke yake hakutoshi, Serikali bado ina jukumu kubwa la kuhakikisha kwamba, inaweka utaratibu wa kisheria na Vyombo au Taasisi maalum za utekelezaji wa Mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maoni hayo, naomba nichukue fursa hii kwa niaba ya Wajumbe wote wa Kamati, kumpongeza Waziri wa Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Charles Keenja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Prof. Pius Mbawala, kwa ushirikiano wao wakati Kamati inachambua Mkataba huu.

Pia, nawashukuru wataalam kutoka Wizara hiyo kwa kusaidia Kamati kutekeleza kazi hii kwa ufanisi. Naomba kwa namna ya pekee kuwashukuru Wabunge, Wajumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi kwa umakini wao wakati wa kuchambua Azimio la Mkataba huu ingawa walikuwa wamepata katika muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba nirudie kusema kwamba naunga mkono hoja ya Waziri wa Kilimo na Chakula.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. THOMAS NGAWAIYA - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi, Waziri wa Kilimo na Chakula, Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi, pamoja na Bunge Zima. Kwa kuwa ni mara ya kwanza basi niseme kheri ya mwaka mpya.

Kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba niwasilishe maoni kuhusu Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Nasaba za Mimea kwa Ajili ya Kilimo na Chakula wa mwaka 2001 uitwao *The International Treaty on Plant Genetic Resources for Food and Agriculture, 2001.*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupapatikia ubora huu wa mbegu haina maana yoyote kama Serikali haitatoa umuhimu au kipaumbele kwenye sekta hii ya kilimo. Kwa kuwa wataalamu wetu wote hawalimi inatuwia vigumu kufaidi utaalamu wa wataalamu hao ukizingatia kuwa kilimo ni uti wa mgongo na mbegu bora ndio msingi wa uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, katika utafiti wetu hakuna Wizara yenye wasomi wa hali ya juu kama walivyo katika Wizara ya Kilimo na Chakula. Ilikuwa ni mategemeo yetu kwamba mbegu zinazozalishwa na wataalamu wetu huko kwenye Vyuo vya Utafiti kama vile Uyole, Ukiriguru, Lyamungo na kadhalika kwamba hawa wataalamu wangekwenda moja kwa moja kwa wakulima vijijini ili wafanye *demonstration* ya mbegu hizo huko kwani hii ingewapa motisha wakulima na pia wangepata uzoefu na elimu kwa urahisi zaidi na hivyo kukuza Pato la Taifa kwa haraka zaidi na kuondosha kabisa baa la njaa.

Mheshimiwa Spika, tunaitaka Serikali ije na sera ya kuwawezesha wataalamu wote wa kilimo kwenda ku-*demonstrate* utumiaji wa mbegu bora ambazo tunazizungumzia hapa. Pia tunashauri hawa

Maafisa Ugani wawe na ujuzi utokanao na mabadiliko ya mara kwa mara kwa kushirikiana na hawa wataalamu watafiti. Kambi ya Upinzani tunapendekeza tafiti zote wapewe maeneo makubwa ya kulima kama mfano.

Aidha, wataalam wote wapate *promotion* kwa kuonyesha mashamba yao na wawezeshwe na wasihamishwe hamishwe kwenye sehemu zao za kazi kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu ili waweze kuonyesha yale ambayo wame-*demonstrate* na wananchi wayaone. Bila mambo kama haya kutekelezwa na Serikali njaa itakuwa haiishi Tanzania. Tunaonekana kituko mbele ya Mataifa tunapoomba chakula cha njaa na ni aibu kubwa Watanzania kufanya hivyo. Lakini kwa mkataba huu na misingi hii tunaona kwamba kama Serikali itakubali mawazo yetu basi hali itabadilika kwa muda mfupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 2 kifungu cha 5 (1)(a) kinachohusu kufanya *survey and inventory* ya nasaba. Ukiangalia hali halisi ya nchi yetu na wakulima wetu ni dhahiri kuwa si rahisi tukafanya wenyewe kwani fedha na utaalamu vinahitajika na hayo Mashirika yatakayoletwa kusaidia kujua nasaba zetu, yatataka yafanye kazi yenyewe kwa kuhusisha wataalam wetu ambapo *control* kubwa itakuwa kwao. Hivyo kwa kuwa hii ni biashara nina wasi wasi faida inawezekana ikawa kwao badala ya kuwa kwetu zaidi au sawa sawa na hii itatokea kwa kuwa kwenye mkataba hakuna chombo kilichopewa mamlaka ya kutoa fedha kusaidia utafiti huu wa nasaba kwa ukusanyaji na utunzaji wa nasaba hizo na badala yake waanze kuhangaika kama sehemu ya 6 kifungu cha 18(3) kinavyoelezea.

Kwa haraka unaweza kugundua kuwa fedha zitatoka kwenye biashara ya hizi nasaba za nchi maskini. Kambi ya Upinzani inaiomba Serikali iwe makini kutoka kwenye mtego huu ambao ni mwendelezo wa utandawazi wa biashara na uchumi wa dunia ya kukandamiza zaidi nchi changa, hasa ukizingatia kuwa nchi tajiri haziruhusu nchi maskini kutoa ruzuku kwa wakulima wake. Naomba tuliangalie jambo hili kwa makini.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 7(b) pamoja na mambo mengine kwenye kifungu hicho kuhusu *documentation* haikueleza kuwa hiyo *documentation* itafanyika wapi. Kwani kwa kuwa kiutaratibu ni vyema vitu vyote vikawa *documented* vikawa kwenye maandishi ili wao wakija wasipate mwanya wa kupata nasaba ambazo bado ziko kwa wakulima na kuzi-*document* wao na kufanya ni mali yao na wakulima na Taifa letu tukakosa haki hiyo japo ni mali yetu. Nina maana hapa bado kuna nasaba kwa wakulima ambazo hazikuandikishwa mahali popote. Inawezekana katika mkataba huu wakaingia wageni na kuziandikisha kujifanya ni mali yao. Sasa Serikali iangalie elimu ili hawa watu waweze kuelimishwa tuandikishe zile ambazo hazijaandikishwa kwenye orodha yetu.

Mheshimiwa Waziri ni muhimu sana kuwa makini kwani mambo yote yatawahusu wakulima walioko vijijini na Serikali au Wizara hawajui hazina na nasaba zote zilizopo kutokana na mazingira na miundombinu ya Taifa letu. Tunaweza kujikuta tunapoteza makubwa zaidi kuliko tunayoweza kupata kutoka kwenye ushiriki wa mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 3 kifungu cha 9(2) *(Farmers Right)* kuhusu haki ya mkulima kwenye faida za nasaba. Kutokana na historia, haki hizi mara kwa mara wakulima wanaweza kuibiwa na Mashirika yanayofanya tafiti katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu kama tulivyokwishaeleza hapa juu. Tafiti hizi zimeachwa katika *National Level* (Taifani) badala ya elimu kwenda kule chini kama nilivyoelezea hapo juu.

Kambi ya Upinzani imeona kwamba ili haki iwe kwa wakulima na wafaidike ifanyike *awareness campaign* ya makusudi ya kuwaelimisha wakulima kwa njia mbalimbali mfano Redio, *Television* na magazeti kuhusu ushirikishwaji wao na haki zao. Kwa njia hii itakuwa ni rahisi hata kufanya *documentation* ya nasaba kwani wao wenyewe watatoa maelezo kuhusu upatikanaji na uendelezaji wa nasaba kwenye mazingira ya asili.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kambi ya Upinzani inashauri kuwepo na chombo au mamlaka ya kuwawakilisha wakulima kutetea na kusimamia haki zao kama zilivyoainishwa ndani ya mkataba tunaouridhia. Tungeshauri kazi hii ingefaa ifanywe na Maafisa Ugani *(Extenstion Officers),* lakini hao Maafisa Ugani sasa hivi hawaonekani vijijini. Tunaishauri Serikali iangalie upya kuhusu kwenda

sambamba na utekelezaji wa mkataba huu. Basi tuangalie upya sheria ya kuweka Maafisa Ugani vijijini kama ilivyokuwa zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona kwamba kwa manufaa ya Taifa letu kunatakiwa kuanzishwe chombo maalum kitakachoshughulikia uchunguzi, utafiti wa nasaba zinazopatikana nchini kwetu, kitu kinachotusaidia na sisi kuwa *active participants* kwenye mkataba huu wa Kimataifa wa nasaba za mimea. Nimeeleza kuwa zaidi ya asilimia 80 ya mimea yetu mfano migomba, mahindi, mchele na kadhalika sio mimea asili Tanzania . Hivyo ni vyema tukaliona hilo lisije likatusumbua.

Mheshimiwa Spika, mkataba huu unatukumbusha ugomvi uliopo kuhusu *Genetic Modified Organ (GMO).* Kwa hiyo, suala la kutunza uasili wa nasaba za mbegu ungeifanya Serikali kuchangamka ili kupata taarifa za ujuzi sahihi kuhusu mambo haya mawili kwani inaelekea kuna nchi kama Marekani zinakwenda kinyume na mkataba huu na juzi hapa Serikali ya Marekani imetoa mahindi ya njano je, tuna uhakika gani si ya *GMO* na wakati huo huo Serikali inalitaarifu Bunge kuwa imeomba mbegu kutoka kwa wafadhili nje? Je, kama watatupatia mbegu ambazo ni *GMO* yaani *Genetic Modified Organ* tufanyeje wakati ambapo tumekwisharidhia mkataba huu. Naomba Serikali itoe tamko rasmi kuhusu *GMO.*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika Jumuiya ya Ulaya wanahitaji vyakula na mazao yasiyotiwa madawa sisi tunaweza kunufaika zaidi na hilo kwa sababu walaji katika soko la dunia ndiko wanakokwenda. Mwisho nataka Serikali iwe wazi kuhusu *GMO* kwamba Kitaifa tunalipokeaje jambo hili maana *Genetic Modified* ina upana mkubwa. Je, Tanzania iko tayari kuendelea na mambo ya *GMO* au tunayapiga vita au namna gani. Serikali itueleze Tanzania Kitaifa tuna msimamo gani katika kulipokea hili jambo la *Genetic Modified Organs?*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo Kambi ya Upinzani inaunga mkono kuridhiwa kwa mkataba huu mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. DR. ALEX J. MSEKELA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Azimio hili. Mimi naomba nianze kwa kuwatakia kheri ya mwaka mpya Waheshimiwa Wabunge wote.

Mheshimiwa Spika, dhana nzima ambayo inawasilishwa kwenye Azimio hili kwa kweli ni ya kupongezwa kwamba kimsingi tunataka kuweka na ndivyo ilivyo kwamba tumejiwekea taratibu duniani sasa za kutunza uasili wa mimea au uoto ambao tunao.

Nafikiri kwa kiwango fulani imetokana na kutambua athari ambazo zinaweza zikatokea na kuletwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia katika upande wa mimea. Maana yake sasa hivi kuna wafanyabiashara haswa haswa wana maabara kubwa kubwa tu kwenye nchi zilizoendelea ambao wanajaribu kubadilisha mimea kwa ajili ya manufaa yao ya muda mfupi

Mimi nafahamu na nafikiri sote tunafahamu kwamba mimea kwa jinsi ilivyo na uasili wake pamoja na binadamu akiwa ni sehemu ya uasili huo iko *balanced.* Unaposababisha mabadiliko ya makusudi kabisa kwa mfano kwa njia ya *GMO* ina maana lazima hata kama hukua na dhamira hiyo utakuwa unambadilisha na binadamu. Sasa kwa kuwa Azimio lenyewe nia yake ni hiyo ni kutunza uasili wa mimea.

Mheshimiwa Spika, lakini hapa ukiangalia haielezi wazi wazi kwamba kutakuwa na *limitations* gani katika *attempt* za kuzuia hii *fast encroaching genetic modification* ya mazao haya.

Mimi nilikuwa naomba muwasilishaji hapa wa Azimio letu ajaribu kutufafanulia kidogo kama kuna viwango ambavyo vinaweza kuwa vinaonekana tayari kwa sababu hatuwezi kukataa, *GMOs* tayari zipo na nafikiri mimi kwa mawazo yangu sio kitu kizuri, wafanyabiashara wanasema ni kitu kizuri kwa sababu wanapata fedha lakini tunafahamu kuna athari kubwa tu za kiafya ambazo zinapatikana lakini pia na *adaptation* ya *surroundings* pia inakuwa ngumu. Kwa hiyo, inafanya maisha kwa ujumla yanakuwa ni magumu.

Sasa nilikuwa naomba niseme kwa sababu Azimio hili haliweki kiwango au *limit* ya *GMOs* kuna viwango vya namna hiyo. Ningependa kwa kweli nifahamu walau kwa nchi yetu, je, ina viwango vya namna hiyo au inatazamaje suala hilo?

Mheshimiwa Spika, katika *para* ya 2 ya hili Azimio linasema sisi ni wanachama wa mkataba wa hii *The Convention on Biological Diversity* ya 1992, sasa hili Azimio linataka kuja kutekeleza ile *Convention* ya mwaka 1992. Anasema: "Kwa kuweka utaratibu wa hifadhi na kuhimiza matumizi endelevu ya nasaba za mimea," ningependa hapa afafanue kidogo. Unaposema kuhifadhi na kuhimiza matumizi endelevu ya nasaba za mimea mnamaanisha nini hasa. Katika sababu ambazo zinafanya Mheshimiwa Waziri aseme kwamba sisi tunastahili kuridhia hili Azimio sehemu ya (b) anasema: "Kuridhia mkataba huu kutaiwezesha Tanzania kutunga na kutekeleza sheria za kudhibiti uhamishaji haramu wa nasaba hizo."

Sidhani kama hii ni faida ambayo tunaipata kwa sababu *we can always do this* hata bila ya huu mkataba. Lakini ukiunganisha na ile sehemu ya (d) anasema: "Kunufaika na matumizi ya nasaba za mimea zilizochukuliwa na nchi au Taasisi za Kimataifa kabla ya mkataba huo. Sasa hapa nilikuwa naomba nifahamu hii maana yake nini? Je, ni suala la mrabaha kwa yale ambayo yalichukuliwa awali au ni kitu gani. Ningependa nifahamu haswa? Kwa sababu tunafahamu kuna mimea mingi tu, mimea ya madawa ambayo imewahi kuchukuliwa siku za nyuma bila nchi ya uasili ya hiyo mimea inafaidika na sijui kama ndiyo nia ya Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, vinginevyo, napenda niwapongeze sana Serikali kwa kuleta Azimio hili na kwa kweli mimi nataka nirudie maneno ninayosema ni kwamba uasili wa mimea kama ulivyo na binadamu mwenyewe akiwa sehemu ya mazingira hayo unaleta *balance* ambayo ikiwa *destabilised* na *GMOs,* kwa mfano, tayari inaleta *knock off effect* kwenye vitu vingi tu pamoja na magonjwa ambayo kwa kweli awali yalikuwa yanatibika kirahisi sasa yanashindwa kutibika.

Sasa nafikiri hii ni *challenge* kubwa ya wao wenyewe kusimamia na kuona kwamba hili kweli litatekelezwa. Lisiwe ni Azimio tu ambalo tumeliweka hapa kwa ajili tu ya kwenda na wenzetu, hapana. Nafikiri ni kitu kizuri sana ambacho mmekubali kukileta hapa na mimi nawapongezeni lakini muhimu zaidi ni jinsi gani mtajizatiti nyie katika kusimamia hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono Azimio, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Azimio hili muhimu kwa Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tunagusia suala zima la kilimo, nataka niitumie nafasi hii kuwapa pole Watanzania wote ambao maeneo yao yamefikwa na ukame.

Vile vile niipongeze Serikali na Wizara hii ya Kilimo na Chakula kutokana na ishara ambazo wananchi wetu hawakuyumba wamebakia watulivu pamoja na kuambiwa kwamba tuna janga kubwa la njaa katika Taifa letu.

Kwa kweli hatuna budi kuipongeza Serikali kwa kuweza ku-*organize* vizuri wananchi wetu na kwa kweli hawakufadhaika juu ya janga hili. Kwa taarifa ambazo tumepata kwenye *briefing* zilionyesha kwamba Serikali inajitahidi katika kuhakikisha kwamba, kama tamko ambalo ametoa Mheshimiwa Rais atahakikisha kwamba mwananchi hata mmoja haathiriki na njaa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, mimi nataka niliunge mkono Azimio hili kwa asilimia mia. Kwa kweli niitake Wizara husika na Serikali kwa sababu tunazungumzia suala zima la kilimo tuwe makini katika kulisimamia.

Mheshimiwa Waziri amewasilisha Azimio hili na Kamati inayohusika iliwasilisha na upande wa Upinzani umewasilisha taarifa yao kwa hiyo kama maeneo haya matatu yalivyowasilisha niombe Mashirika yaliyohusika na mkataba, Serikali pamoja na wakulima na wao kuweka *joint* moja ili kuleta

mabadiliko na mafanikio makubwa ya kilimo katika Taifa letu hili la Tanzania. Kama maeneo haya matatu yalivyowasilisha taarifa zao hili hapa na kwa kweli zote zikienda pamoja na tunapopitisha Azimio hili lilete faida kubwa kwa Taifa letu la Tanzania hasa suala la kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika Azimio hili ambalo tunaliridhia mkataba wa Kimataifa wa Nasaba za Mimea kwa Ajili ya Kilimo na Chakula wa mwaka 2001 ambao unaitwa *The International Treaty on Plant Genetic Resource for Food and Agriculture 2001,* wananchi wanasikia tunachokizungumza na tuna uhakika watajenga matumaini makubwa kwa mafanikio makubwa baadaye na hasa tukiangalia Mheshimiwa Waziri alipokuwa anawasilisha alizungumzia kwamba kuwepo kwa haki za wakulima wadogo wadogo. Hawa ndio leo hii wanaokumbana na njaa katika Taifa hili kwa sababu kama ukulima wao ungekuwa mkubwa tunaamini kwamba Taifa letu tungeweza ku-*control* hali iliyoko kwa wakati huu.

Kwa hiyo, kwa kutumia Azimio hili ningeishauri Serikali iwe makini sana katika kulifanyia kazi na kuleta mabadiliko kuanzia miaka inayokwenda mbele kwamba nchi yetu iepukane na balaa kubwa la njaa kama hili la sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, kidogo nikimnukuu Mheshimiwa Waziri Mkuu juzi alipotoa *briefing* kuelezea suala la chakula, alisema kwamba hata kuna Mataifa yanashangaa hapa duniani kwamba Tanzania inaambiwa ina njaa.

Nikimnukuu Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya, alitoa wazo kwamba ipo haja ya Wizara hii husika ya Kilimo na Chakula na sisi Wabunge tukae, tujadili hili suala. Mimi niki-*refer* ile ya jana nilizungumza kwamba kwa ziara ile ya Mkoa wa Kagera tulipokwenda juzi sisi Kamati tulikuwa tunaulizana katika gari Mkoa wa Kagera tu pekee vyanzo vya maji kama ingekuwa Wizara ya Kilimo inatumia sawa sawa Mkoa ule na maeneo mengine Tanzania ina maji kama yale ingehakikisha kwamba ingekuwa na uwezo wa ku-*cover* matatizo katika Taifa letu la Tanzania. Kwa hiyo, ipo haja ya Wizara hii kujenga mikakati ya kuweza kukuza kilimo cha hali ya juu katika Taifa letu hili la Tanzania kuyatumia kama maji ya *Lake Victoria,* Mto Kagera na vile vyanzo vingine vidogo ambavyo Mheshimiwa Spika vinaweza kulipatia Taifa letu maendeleo makubwa kwa siku za baadaye.

Mheshimiwa Spika, katika Azimio hili vile vile linasema kwamba mkataba huu wa Kimataifa wa Nasaba za Mimea ni kwa ajili ya Kilimo na Chakula, *special* ni kwa ajili ya kilimo na chakula. Kwa vile nchi yetu ilivyo kubwa tuna maji ya kutosha tayari hapa Wizara imeji-*commit* kwamba sasa hivi itaweza kusimamia kushughulikia suala zima la kilimo ili kuleta mabadiliko makubwa kwa Taifa letu hili.

Moja linalowawezesha wakulima wetu walioko ndani ya nchi tusisubiri labda waje wakulima wakubwa kutoka katika Mataifa ya nje ili kuja kuwekeza katika masuala ya kilimo.

Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, alipokuwa akiwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani hapa alisema kwamba Wizara hii ina wataalamu wakubwa sana. Kwa hiyo, wataalamu hawa waingie katika maeneo, wajenge miundombinu ambayo itakuza kilimo kwa faida ya Taifa hili kwa nguvu za pamoja kabisa Serikali, Mashirika ya Kimataifa na wananchi wenyewe wakaingia katika maeneo ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ukiendelea mkataba huu unasema unalenga katika kutekeleza Mkataba wa Kimataifa wa Bioanwai wa Mwaka 1993 kwa kuweka utaratibu wa kuhifadhi na kuhimiza matumizi endelevu na kuendeleza kilimo zinatumiwa kwa haki na usawa. Sasa haki na usawa ni kuwawezesha watu wadogo wadogo, *serious* kabisa. Hili linawezekana.

Jana bahati Wizara ya Maji wametia saini nafikiri mkataba wa kupeleka maji kutoa Ziwa Victoria wa shilingi bilioni 80, hebu tujaribu vile vile kupeleka katika Mikoa ya Shinyanga sijui na maeneo mengine. Hivi Wizara ya Kilimo na Chakula, tutafute mkoa mmoja tuteue na kwa bahati nzuri katika ziara yetu sisi tuliokwenda Kagera tumeona Magereza wana uwezo mkubwa wa kushughulikia kilimo. Mashamba yote ya Magereza tuliyoyakuta pale Kagera yana uwezo wa kulima mahindi na kila kitu. Basi japo kutoa ruzuku katika maeneo yale.

Mimi napendekeza kwa Serikali tuchague eneo moja tuwawezeshe kuwapatia nyenzo, matrekta na uwezo mkubwa, pampu ya kuweza kutoa maji Ziwa Victoria na maeneo mengine tuhakikishe kwamba katika hii mimea ambayo tunakusudia kuiendeleza ni kuzalisha chakula cha kutosha katika Taifa hili. Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie kwa uwazi.

Mheshimiwa Spika, katika eneo lingine katika Azimio hili kuna sehemu inaelezea kuwa Tanzania ina utajiri mkubwa wa nasaba na za mimea na imekuwa na ina nia ya kulinda Kimataifa na kunufaika nao kwa kushiriki kikamilifu katika majadiliano yaliyowezesha kuwepo kwa Mkataba wa Kimataifa wa Nasaba za Mimea kwa Ajili ya Kilimo na Chakula, umeonyesha kwenye Azimio hili Mheshimiwa Waziri.

Tumekiri kwamba Tanzania inao utajiri mkubwa moja ni *resources* za *water* katika Taifa letu la Tanzania, ni utajiri mkubwa sana. Mungu alivyotupenda, maji karibu mengi sana kama mfano Mto Kagera. Tumepata msaada kutoka ndani ya Rwanda na Burundi yamo ndani ya nchi yetu ya Tanzania, tuvitumie vyanzo hivi. Tutakuwa tunafanya kosa kupitisha maazimio yakawa hayaleti uzalishaji katika Taifa hili. Kwa hiyo, kila utajiri tulionao tunaamini tuufanyie kazi kwa faida ya Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, katika Azimio hili limebainisha maeneo matano ambayo tutakaporidhia mkataba huu tutaiwezesha Tanzania. Lakini mimi nataka nichukue maeneo mawili. Katika yale yameanza "A" mpaka "E".

Mimi nitaanza na eneo "C" ambalo limezungumza kwa kuimarisha utafiti wa mazao kupata teknolojia halisi nasaba za mimea kutoka nchi za nje bila ya kulazimika kuwekeana mikataba na nchi. Hili kwanza hii faida tusimalizie ndani ya Serikali kwa Serikali itakapokuwa tumeitengeneza na wenzetu katika Mataifa hizi nasaba za mimea moja kwa moja tuwasiliane na wakulima wetu walioko vijijini na tuwatake watendaji wetu wa vijiji wasimamie kilimo wawasaidie hawa wakulima wadogo wadogo. Kasoro moja ambayo tunaiona tunakosea inawezekana watendaji wa vijiji kuna maeneo maalum waliwekewa kuyafanyia mkazo pengine kwenye kodi wakati ule nilipokuwa nafanya kazi, pengine kwenye elimu, lakini suala la kilimo kwa nini.

Mheshimiwa Spika, kama Kagera ndizi kule ni nyingi sana halafu bahati mbaya wana mchezo mbaya wale ukigombana naye tu mtu anatema migomba yote hata ikiwa na miaka 20. Chakula wanacho laiti ingekuwa hawana chakula kile na migomba kiasi kile kufulu ile wasingelifanya hata siku moja.

Kwa hiyo, Serikali ifanye utafiti kwa suala kama hili hasa Kagera. Pale sheria watendaji hawasimamii. Tulipita sehemu moja tulikuta shamba limekatwa na yule mama anaambiwa ahame pale kabisa kwa tofauti tu baina ya mumewe na watoto. Sasa wananchi wanalima mazao faida hawaioni, sheria ziko mikononi mwa watu binafsi.

Kwa hiyo, iwekwe sheria ngumu kwa sababu mbegu ya mhindi inaonekana, lakini ya mgomba sijui inatoka ndani ya nini. Unaweza kwenda dukani ukanunua zile mbegu za mahindi, mtama na kadhalika ukaenda kupanda, je, mgomba unatoka wapi? Ni lazima uwe mgomba. Sasa wenzetu wanalima sana migomba. Tunaomba Mheshimiwa Waziri, alione hili katika suala la faida.

Mheshimiwa Spika, nimechukua (e): "Kutambulika kwa haki za wakulima wa Tanzania ambao ni wachangiaji wakubwa katika kulinda na kuhifadhi mimea yetu." Mlinzi yeyote yule anapewa motisha. Inawezekana kulikuwa na mbegu hata Wizara inaonyesha hapa kwamba kuna nyingine ililazimika wakazitafute kwa wakulima wa kawaida Vijijini wazirudishe katika vitalu vyao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, muwape motisha na motisha kubwa ni kuwawezesha wakulima. Hatutafika kwa kupitisha tu Maazimio. Tuwasimamie, tuwasaidie ili wao wawe watunzaji wakubwa wa mali kama hizi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nataka nirudie kuwapa pole Watanzania wote katika maeneo yaliyopata baa la njaa, lakini pia ni lazima tuwapongeze kwa ustahimilivu mkubwa. Wananchi wamesababisha Serikali yetu kutulia kwa sababu hawakuyumba na nimtake Waziri aendelee kulifanyia

kazi Taifa hili, sasa alete mabadiliko makubwa ya suala la kilimo katika Taifa hili ili hali halisi ionekane wazi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Azimio hili. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PHILLEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie kidogo tu katika Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, Azimio hili kwa kweli limechelewa, lilitakiwa lije miaka mingi iliyopita. Nasema hivyo kwa sababu nimekuwa nikisoma magazeti ya Uingereza ambapo sasa wana ugomvi mkubwa kati ya Kisiwa cha Uingereza na *Europe* hasa kwa hizi *Genetic Modified Seeds.* Nimesoma Uingereza kupitia Shirika lake la *Development,* Tanzania na nchi moja ya Asia. Tanzania ilichaguliwa miaka zaidi ya 20 ikifanyiwa majaribio ya *Genetic Modified Seeds* na fedha nyingi sana za Uingereza zimetumika hapa Tanzania. Sijui Mheshimiwa Waziri atatuambia *experiments* hizo zilikuwa zinafanywa wapi. Zilikuwa zinafanywa katika hizi sehemu zetu kama Uyole ambako ndiko tunakotoa mbegu au zilikuwa zinafanyika wapi na madhara ya miaka 20 ambayo Tanzania imepata ni kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, ninasema hivyo kwa sababu kule Kilimanjaro kuna mbegu nyingine za miti zilipandwa zikafanya hata ile miti ambayo ni *original* kuanza kupukutika na kuharibika. Siyo hiyo tu, kuna mimea mingine ikipandwa mahali inaharibu ile mimea yetu ya asili na hii imekuwa ikiendelea kwa miaka mingi. Wenzetu walioendelea kama kule Amerika si rahisi uingize mbegu ya namna yoyote kule. Sijui kama sisi tuna mpango au tuna uwezo wa kuzuia watu kuingiza mbegu ambazo zinaweza ku-*interfere* na mbegu zetu za asili katika nchi hii!

Mheshimiwa Spika, nimetoa hiyo tahadhari kwa sababu Serikali haijawahi kusema au kukubali ya kuwa nchi hii imekuwa ikitumiwa kama *experiment* ya *GM Products* kwa miaka zaidi ya 20.

Mheshimiwa Spika, nimetoa tu hilo wazo na naunga mkono hoja hii kwa sababu itatusaidia na ilikuwa ije siku nyingi. Sina mengi zaidi ya kuongeza, nilitaka tu ku-*raise that awareness* ili Serikali iweze kutuambia kiwango cha madhara na *extent* ya kwamba ni kiasi gani tumefikia katika madhara hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante na ninaunga mkono Azimio hili. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi uliyonipa. Ninasimama kuunga mkono hoja ya kutaka Bunge Tukufu liridhie huo Mkataba unaojihusisha na kulinda mimea (Azimio la Mkataba wa Kimataifa wa Nasaba za Mimea kwa Ajili ya Kilimo na Chakula wa 2001).

Mheshimiwa Spika, ningependa kwanza niseme kwamba ukienda kwa utaratibu uliofanyika na Jumuiya ya Kimataifa kupata Mkataba wa Kimataifa wa Bioanwai *(Conventional Biological Biodiversity, 1992)* ambao ulihusu kile ambacho Dr. Alex Msekela alichokisema, uasili au mimea na uoto wa asili ambao hata sisi viumbe tunaoitwa binadamu ni sehemu ya Bioanwai. Mkataba ule ulijihusisha na mimea yote na viumbe vyote hai, Mkataba wa Rio wa mwaka 1992.

Mheshimiwa Spika, hoja iliyo mbele ya Bunge hili Tukufu imechukua sehemu katika Mkataba ule wa Rio wa Bioanwai. Ukisoma ibara ya 3 ya Mkataba inasema hivyo kwamba: *"This treaty relate to plant genetic resources for food and agriculture,"* mimea inayohusika na chakula na kilimo katika ule ujumla wa bioanwai katika dunia yetu. Kwa hiyo, hili nafikiri ni muhimu kwa sababu tunachokizungumzia hapa ni eneo mahsusi na imeelezwa ni nini hasa, ni kwa nini tunalenga huko.

Mheshimiwa Spika, tukisoma Mkataba wenyewe ibara ya kwanza inazungumza ni kwa nini tunalenga huko, lakini zaidi ni pale ambapo inahusika na nasaba ya mimea na kujielekeza kwenye suala la kilimo na chakula na namna ya kugawana manufaa yanayotokana na mimea hiyo na chakula kwa kuzingatia huo Mkataba wa Kimataifa wa Bioanwai na inaendelea kuzungumzia haki za wakulima pamoja na uendelevu wa hizi nasaba za mimea.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba, jambo la kwanza unaloliona kwa mfano katika ibara ya 5 ni kwamba, hizi nasaba za mimea ambayo ni raslimali lakini unajikita kwenye kilimo na chakula, ni lazima raslimali hizi (nasaba za mimea hii) itumike kwa namna ambayo unafanya *conservation.* Lakini pia kwa sababu mimea iko kwenye maeneo mawili ya kilimo na chakula una *conservation,* una *exploration, collection, characterization, evaluation and documentation* ili uweze kupata ujuzi zaidi wa mimea iliyo katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, najua Waheshimiwa Wabunge wamechangia na kusema, hivi hili suala kama alivyokuwa anazungumzia Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo hapa, suala la *Genetically Modified Organisms* au *GMO* kwa kifupi, ni vipi?

Mheshimiwa Spika, kwanza niseme hili ambalo Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, amesema kwamba yaelekea nchi yetu kwa miaka 20 kumekuwa kunafanyika majaribio ya jambo hili.

Napenda kusema kwamba, sisi katika Ofisi ya Makamu wa Rais ambao tunafanya kazi ya kuratibu shughuli zote hizi hasa inapohusiana na masuala ya mazingira hili halipo, hatunalo na hatujalipata rasmi, kama lipo labda linafanyika kinyemela.

Kwa jinsi alivyoliweka ni kwamba, tulipaswa kulijua kwa sababu anasema ni kama kulikuwa na Serikali ya nje na sisi, lakini sisi katika Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kweli hilo halipo na halipo kwa sababu kwanza, Jumuiya ya Nchi za Ulaya mpaka hivi sasa wanafuata msingi uliowekwa katika kile kinachoitwa *agenda 21 (Pre-cautionary principal)* kwamba kama kuna jambo linasemwa lakini huna ushahidi kamili haikuzuii kuchukua tahadhari ya kujilinda.

Mheshimiwa Spika, katika suala hili la *Genetically Modified Organism (GMO)* ambayo inahusu mbegu, mimea, wanyama hasa viumbe wa baharini na majini mpaka hivi sasa kuna kambi mbili. Kuna kambi moja inayosema vitu hivi vina manufaa kwa binadamu, kama ni mimea, kama ni mazao yake yanastahimili maradhi, yanakua upesi na yanastahimili ukame. Kwa hiyo, mahali ambapo kuna matatizo ya upungufu wa chakula pengine litasaidia.

Lakini kambi ya pili inasema, hatuna hakika ya madhara ya mazao ya *GMO* kwa matumizi ya binadamu. Sasa ninachojua, katika Jumuiya ya Ulaya wanachokisema ni kwamba, hatujapata uhakika wa madhara ya *GMOs* kwa afya ya binadamu kwa hiyo tuchukue tahadhari, ndicho ninachokijua. Sasa, ningeshangaa kweli kama moja ya nchi za Jumuiya ya Ulaya wangekuja wakafanya majaribio hapa kwetu bila jambo hili kufahamika rasmi. Hilo nilitaka nilieleze kwa namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, niseme kitu kimoja ambacho ni kweli Waheshimiwa Wabunge wamesema itabidi pengine itungwe sheria ya kutekeleza mkataba huu ambao tunaupitisha kuwa Azimio, lakini pengine itabidi tufanye kile wanachokisema Waingereza. Upo msemo unaosema: *"Heathen Slowly, Festina Lente"* kwa Kilatini, usifanye haraka sana.

Mheshimiwa Spika, ninachofahamu na kama nilivyosema, tunazungumzia mazao, nasaba ya mimea ya chakula na kilimo ambayo ni sehemu ya Mkataba ule mkubwa wa Bioanwai. Kama sikosei mwezi huu wa pili katika nchi ya Malaysia unafanyika Mkutano wa nchi wanachama wa Mkataba wa Bioanwai kuzungumzia masuala yanayohusu ni vipi mkulima wa kawaida ujuzi wake *(indigenous knowledge),* uzoefu katika kuhudumia mazao na mimea hii ya kilimo pamoja na mimea mingine, maana sasa ule ni Mkataba mkubwa, ujuzi wake uthaminiwe vipi na upewe hadhi inayostahili kama inavyozungumzwa katika Mkataba huu ambao Azimio liko mbele ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, mkutano huo ambao ni mwendelezo wa majadiliano ili hapo baadaye pengine itabidi Jumuiya ya Kimataifa ije na Mkataba wa kusema namna ya kuenzi ujuzi wa mkulima mdogo mdogo *(indigenous knowledge)* na *local communities* pengine tuwe na Mkataba mahsusi wa Kimataifa.

Majadiliano yanaendelea na mkutano wa Kuala Lumpur nafikiri tarehe 18 na 19 Februari ni wa kuiagiza Kamati inayoendelea na mjadala huu kwamba tunavyoona sisi Jumuiya ya Kimataifa twende hatua moja, mbili, tatu hadi kufikia Mkataba.

Kwa hiyo, tunapofikiria kutunga sheria ninaamini tunaweka msingi katika kupitisha Azimio hili na kuridhia Mkataba ulio mbele ya Bunge lako Tukufu. Lakini ninaamini kabisa yale majadiliano katika ngazi ya Kimataifa yatatusaidia katika kuja kutunga sheria hapo baadaye. Hili nilitaka niliseme hivyo katika kujaribu kuweka mambo sawa.

Kuhusu hili suala la *GMO* kama nilivyolieleza kwa muhtasari, ukisoma Mkataba inaelekea kwamba Mkataba huu kwa namna moja au nyingine unalenga kuendeleza mashaka ya kutokubali suala la *GMO* kichwa kichwa. Ukisoma ile ibara ya 5 sehemu ya (d), (e) pamoja na (f), unapozungumzia juu ya maneno pale *Genetic Integrity,* basi hali ya kubadilisha *gene* za mmea ambacho ndicho kinachofanyika katika *Genetic Engineering* kwa Mkataba huu unaona kama utaratibu huo unawekwa pembeni. Kwa hiyo, pengine hatuna sababu ya kuhofia sana.

Mheshimiwa Spika, isitoshe katika suala hili zima la *GMO* nchi moja katika Bara letu la Afrika ambao wamepiga hatua ni Cameroon, wao wanayo sheria na Waheshimiwa wanaopenda tunaweza kuonana nikawapa fursa ya kuiona sheria ile. Kinachozungumzwa ni *handling.*

Mheshimiwa Spika, kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja amesema *GMO* mambo haya yapo duniani na Makampuni makubwa yanapigia debe. Sasa tujue kwamba suala hilo lipo, lakini la msingi ni *handling* yake. Sheria nzima ukiisoma ni namna ya kupeana taarifa na namna ya kushughulikia hiyo. Kuna sehemu ya *GMO* inayozungumzia *Terminator Process* kwamba, ukibadilisha *gene* ya mmea 'a' mmea ule wa asili utatoweka. Ukifanya hivyo unakiuka Mkataba wa Kimataifa wa Bioanwai kwa sababu lengo lake ni kutunza, kuhifadhi na kuendeleza mimea na uoto wa asili.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nilitaka nitoe ufafanuzi kidogo hivyo kwa lugha yangu ambayo si nzuri sana, lakini nilitaka nichangie kwa hayo. Narudia kusema kwamba naunga hoja mkono. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, nami naomba nichangie kidogo kwa kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula ambayo ameitoa asubuhi hii kuhusu *The International Treaty on Plant Genetic Resource for Food and Agriculture, 2004.*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nasema naunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kuchukua fursa hii kukutakia kheri na kuwatakia kheri Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kheri ya mwaka mpya wa 2004.

Tatu, ningependa kumpongeza Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kujiunga tena na Bunge hili Tukufu. Karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nina machache sana ya kuchangia kuhusu hoja iliyopo mbele yetu. Ya kwanza iliyozungumzwa ni kuhusu *Extension Officers* huko Wilayani. Napenda kutoa ufafanuzi kidogo na mengine atayazungumzia mtoa hoja mwenyewe, Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 1998 Bunge hili hili liligundua kuwa Wataalam wa Kilimo, wakati huo tulikuwa nao kama 7,000 hivi nchi nzima wametapakaa katika Mikoa 20 wakati ule na Wilaya zaidi ya 110, ilikuwa vigumu kuwasimamia kwa karibu na kuwe na tija kama wote wangesimamiwa na Mheshimiwa Waziri kutoka Dar es Salaam.

Hivyo, Bunge Tukufu hili hili likapitisha Azimio la kutoa madaraka Mikoani kuhusu masuala haya, likasema: "Watumishi wote katika ngazi ya Wilaya sasa wapo chini ya Mamlaka ya Halmashauri za Wilaya na Miji, yaani wote isipokuwa wale walioko katika Vyuo vya Mafunzo na Utafiti ndiyo wako moja kwa moja chini ya Mheshimiwa Waziri au Wizara.

Mheshimiwa Spika, sasa huko Wilayani yupo nani? Sisi wote Waheshimiwa Wabunge pamoja na mimi, tunahusika na *District Councils* kusimamia maendeleo ya kilimo na mengineyo. Hivi leo tukija kutoa hoja hapa kuwa mtumishi mmoja wa kilimo Namtumbo ni mvivu hafanyi kazi, nikisema mimi humu Bungeni najisuta mwenyewe kuwa sikai kule Namtumbo. Kama kweli nakaa Namtumbo basi na mimi moja kwa moja nikiwa Diwani wa Halmashauri husika ya Namtumbo sijui tusemeje, kwa sababu suala la kusimamia Watumishi wa Ugani katika ngazi ya Wilaya siyo la Waziri wa Kilimo na Chakula peke yake na wasaidizi wake.

Awali kabisa ni suala la Madiwani wakisimamiwa na Mkurugenzi wao wa Maendeleo, aidha wa Halmashauri au Wilaya. Ndiyo tulivyopitisha humu Bungeni mwaka 1998 kisheria wala siyo eti ushauri shauri tu, hapana! Sheria hiyo ipo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, ninachoomba tukumbushane kuwa Watumishi kama ni legelege, hawafanyi kazi, turejee kwenye sheria ya 1998 tuone kwa nini hatuwasimamii. Madiwani ni sisi hapa Waheshimiwa Wabunge na wenzetu walioko kule.

Kwa kweli uhusiano wa Watumishi wale na Waziri na wasaidizi wake katika ngazi ya Wizara ni ule wa *professional,* lakini kazi ya kila siku, mipango ya kazi, tija yao na ufanisi wao inategemea sana Madiwani huko huko katika ngazi ya Wilaya ambapo sisi Wabunge wote pamoja na mimi tunatoka. Kwa hiyo, naomba tujikumbushe hili na tusilisahau kwa sababu tulilipitisha kisheria humu humu Bungeni mwaka 1998. Hilo la kwanza.

Pili, tumeongea sana juu ya *Demonstration Farms,* ni kweli inatakiwa pawe na mbinu mbalimbali za kusaidia kusimamia wakulima au kuwashauri kwa kutumia *demonstration.* Lakini hilo nalo ni suala la *District Council* kwa sababu sisi Madiwani kama Wabunge tupo. Tunachoomba kifanyike ni kuwa tunapoanza kufanya mipango (fedha na mipango) tuzungumzie na suala la kilimo isionekane kama mmoja yuko huko juu ndiyo asimamie, hapana. Zile *Demonstration Farms* kama ni lazima zifanyike na ninaamini zina umuhimu wake, basi tuhakikishe kwamba suala hili linajadiliwa kwanza kwenye *District Council* na kutoka kule kama unatakiwa msaada *professional* au msaada fulani fulani wa taaluma au mafunzo fulani kuongezea, basi hapo lifike kwa Wizara na Wizara itakuwa tayari kutoa msaada huo. Kwa hiyo, toka mwaka 1998 palitolewa zana na vinginevyo kwa masuala hayo.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge aliyezungumzia suala hili akumbuke kuwa, suala la kusimamisha Watumishi wa Kilimo si suala la Waziri wa Kilimo na wasaidizi wake peke yake, inamuhusu hasa yeye kwa kuwa ndiyo anamsimamia *DED* na *DED* ni wale *lieutenants* wake. Tunaomba tukumbushane hii kisheria. *Professional advice* ni kitu kingine.

Pia kuna suala la njaa. Ni kweli kuhusu suala la njaa anayehusika na kulisha wananchi ni Wizara ya kilimo, lakini tusisahau kuwa tuna Watendaji kama ambavyo Mheshimiwa mmoja ametukumbusha hapa, kuna Watendaji wa kijiji wako kule. Wale Watendaji wameajiriwa na *District Council,* yule *Village Worker* na yule wa Kata ameajiriwa na Mamlaka ndani ya Wilaya husika.

Kwa hiyo, tena tunakumbushana, ipo haja suala hili kuliangalia kwa makini zaidi. Njaa ikitokea isionekane kama kuna mtu mmoja huko juu hataki kufanya kazi, ni sote kwa sababu hakuna mahali ambapo hakuna Diwani na Diwani huyo ni yule wa Kata na yule wa Jimbo ambaye ni sisi Waheshimiwa Wabunge. Tuhimize kilimo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mfano sasa hivi wengi tunaomba msaada wa mahindi na kadha wa kadha, ni sahihi kabisa, lakini ni wachache sana tunasahau kama zao moja linalosaidia sana kupambana na njaa ni zao la muhogo. Mvua zilizopo mwaka huu ukiacha Pwani, Kilimanjaro, Arusha na Morogoro kwa sababu sasa siyo wakati wake, wakati wa kupanda muhogo ni sasa. Tujiulize, je, tumejadili suala la nafasi ya muhogo katika Wilaya zetu husika? Wengine watasema: "Aaah mimi situmii muhogo." Tupande tu, halafu tutawauzia wanaopenda kula muhogo na tukipata fedha tutatafuta chakula tunachokitaka.

Kwa hiyo, napenda kutoa ombi kwamba, wakati tunapata msaada wa chakula kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu tuhusishe na upandaji wa muhogo yaani tuseme, wakati tunatoa mahindi wakati huo huo tuhakikishe kama wananchi wameandaa angalau nusu eka tu ya shamba la muhogo, mbegu zipo za kutosha sana. Kule Bukoba alipozungumzia Mheshimiwa Mbunge mmoja kuna mihogo mingi sana. Pia, kuna shamba letu la mbegu pale Ukiriguru, lipo lingine hapa Hombolo na liko lingine pale Kibaha na karibu Mkoa mzima wa Pwani kuna mbegu za mihogo. Tujiulize, je, sisi tumehimiza suala la kupanda muhogo?

Mheshimiwa Spika, muhogo una *advantage* moja, mvua hata kama siyo nyingi utaota na hata kama kutakuwa na nzige watashambulia majani utachipua tena na hauhitaji ghala na wala hauhitaji mbolea nyingi. Kwa hiyo, pendekezo hili naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tujiandae, kila mmoja atumie fursa hii kuhamasisha kilimo cha muhogo katika Mikoa yetu tunapotoka. Kila palipo na muhogo njaa ipo, lakini siyo kali hadi watu wakafa. Lakini kutegemea maeneo kwa mahindi ni mashaka sana, mvua hazitoshi hata hizi za sasa hivi pengine ni za wasiwasi na mtawanyiko wake ni wa wasiwasi pia.

Mheshimiwa Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuhimize mihogo tunakotoka, tafadhali sana na anayetaka msaada wa mbegu chache tunazo hapo Hombolo na nipo tayari kumpa hizo mbegu. Baadhi yetu wamekuja nimewaonyesha na nimewapatia. Vile vile, kwenye eneo lile la migomba nimeshangaa sana kuwa wakati mwingine *demonstration* inaweza kuwa haiwezekani. Nilikuwa Ngara mwaka 2002, pale kuna shamba la migomba bora, kilichonishangaza hata Madiwani hawakuhitaji kuchukua zile mbegu za migomba bora. Nimekuja Biharamulo nikakuta sehemu kuna *Demonstration Farm* pale, jirani kuna shamba la Magereza wana vindizi ovyo ovyo tu, ilibidi niende pale nikasimama nikauliza: "Ndugu yangu Afisa unaona ile migomba inavyostawi pale?" Akajibu: "Ndiyo." Nikamuuliza tena: "Ni kwa nini?" Akasema "Aah bwana, kupitiwa tu."

Mheshimiwa Spika, niliona shamba la Magereza wamelima mbegu zisizofaa. Si hapo tu, Bukoba Mjini lipo shamba la mbegu bora za migomba, kadhalika watu wa aina mbalimbali, Madiwani, Magereza hawachukui mbegu pale, mimi nilichukua nikapeleka Songea kwa kulipia. Kwa hiyo, hili suala la *demonstration* linahitaji uhamasishaji, inaweza kuwa *demonstration* iko pale watu hawaitumii.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, aliona pale Tengeru kuna migomba ya aina tisa, migomba bora na ingefaa sana katika Mikoa ya Arusha na Kilimanjaro. Kuna Mabwana shamba, kuna Madiwani na viongozi wengine hawaioni, iko barabarani tu! Kwa hiyo, suala la *demonstration* nalo linahitaji kuhamasishwa, ni pamoja na sisi Waheshimiwa Wabunge. Naomba kutoa rai tutumie nafasi zote hata migomba nayo inahitaji kuhamasishwa. Hiyo niliona tujadili na kufikiria hayo.

Kuhusu Magereza tuna wasiliana na Magereza kuzungumzia suala hili la njaa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, tumezungumza na tutachukua uzito unaotakiwa kwa masuala haya ya muhogo kwa sababu hata maafisa wake walikuja Wizarani tukawapeleka Kibaha, wakaonyesha kuwa muhogo uliweza kuvunwa asubuhi saa mbili, saa tatu ukasagwa na kukamuliwa sana saa saba unga ukapatikana na maafisa waliahidi wangeangalia upya suala la kupanda zao la muhogo. Vile vile tuliunda Kamati maalum ya maafisa kilimo na maafisa wa mambo ya ndani hususan Jeshi la Magereza kuona jinsi tunavyoweza kusaidiana na Jeshi la Kujenga Taifa kuinua uzalishaji wa mifugo na mengineyo kwa lengo la kuwa magereza si lazima watumie ile *SGR* peke yake, wangeweza kutumia mihogo kama moja ya zao la kuwalisha ndugu zetu walioko katika magereza.

Mwisho nataka kusema tunayo *National Irrigation Master Plan* mwenyewe nilipokuwa najibu maswali hapa mara nyingi nilikuwa naimba jamani tunaomba *bottom up approach* mtuletee mapendekezo yenu kwa kweli ilikuwa taabu sana kuyapata yale mapendekezo tumetengeneza tumeainisha kama kuna maeneo hekta milioni 43 inafaa sana *prime land* kwa kilimo. Vile vile kuna hekta milioni 29 zinazofaa sana kwa *irrigation.*

**SPIKA:** Naomba umpe nafasi mtoa hoja usimalizie muda wake.

**NAIBU WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga tena mkono hoja hii. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru tena kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kidogo katika yale yaliyotolewa lakini kwa ruhusa yako naomba niwashukuru wale wote waliochangia na wote wameunga mkono hoja nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mchangiaji wa kwanza alikuwa Mheshimiwa Edward Ndeka, ambaye nimetoka kutembelea Jimbo lake hivi karibuni, namshukuru sana kwa mawaidha mazuri sana aliyotoa. Namshukuru sana Mheshimiwa Thomas Ngawaiya kwa kuunga mkono na tutazingatia yale mengi aliyopendekeza, nitazungumzia machache. Mheshimiwa Dr. James Alex Msekela nakushukuru sana, pia Mheshimiwa Omar Mjaka Ali. Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, ambaye ametutahadharisha kwamba huenda kuna watu wanafanya utafiti wa *GMO* huku nchini, tutaomba tuonane ili utupe yale unayojua maana kuishi kwingi ni kuona mengi. Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, nakushukuru sana kwa kufafanua maswali mengi sana yanayohusiana na Mkataba huu pamoja na *GMO* na Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, nakushukuru kwa yale uliyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba kwanza nitoe maelezo mafupi ya utangulizi kwamba hili suala la kuhifadhi nasaba za mimea tuliliona siku nyingi kama Taifa na tuna kituo pale Arusha *TPRI* ambacho kinashughulika na kukusanya na kuhifadhi hizi nasaba za mimea. Naambiwa mpaka hapa tulipofikia kile kituo kina nasaba kama 4,000 ambazo ni nyingi kidogo.

Kwa hiyo, kama kuna mbegu ambayo ilipata kupita nchini huku unayoifahamu na ungetaka kuipanda tena mbegu ile kama siku hizi haionekani ukienda kwenye kile kituo utakuta wameihifadhi. Sasa tunategemea kwamba tukisharidhia Mkataba huu na kwa hiyo, tukajiunga na nchi nyingine duniani, kile kituo kitafaidika kutokana na utaalamu ulio katika nchi mbalimbali juu ya hifadhi ya mimea na vile vile tutafaidika kwa kupata vifaa vya kisasa na misaada mingine ili kiweze kufanya kazi yake vizuri zaidi. Kuhusu lile suala la *GMO* amelizungumzia vizuri Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, mimi labda niseme tu kwamba kuna kazi zinazofanyika sasa hivi za kuandaa kanuni zitakazotawala uingizaji wa *modified organism* katika nchi na hizo kanuni hazijakamilika. Tutaharakisha zikamilike ili baadaye Bunge liweze kutunga sheria za kusimamia suala hilo. Namshukuru sana Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, kwa ufafanuzi aliotoa.

Pia Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, namshukuru kwa yale aliyoona Kagera na kwa kuipongeza Serikali kwa juhudi ambayo kwa kweli inachukua kuhakikisha kwamba wananchi wetu hawaathiriki kutokana na hali ya upungufu wa chakula iliyoko nchini. Tuko wengi ambao siku hadi siku tunasimamia suala hili. Lakini nakubaliana na wewe kwamba tunahitaji kuwa na mkakati wa kitaifa wa kuhakikisha kwamba hatuendelei kuwa na upungufu wa chakula kila mwaka na baada ya kutembelea Kigoma wewe umetembelea Kagera na Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, nafikiri tukilenga kusaidia mikoa hii inaweza ikalisha kwa urahisi sana lile eneo dogo ambalo hukabiliwa na ukame mara kwa mara. Katika Bunge lijalo la Bajeti tutaleta mapendekezo jinsi tunavyokusudia kushughulikia suala hilo. *(Makofi)*

Mimi nakubaliana na Mheshimiwa Edward Ndeka, kwamba kuna haja ya kuleta sheria hapa Bungeni mapema iwezekanavyo na kwa kweli ni sehemu ya Mkataba kwamba kila Taifa liwe na sheria inayosimamia nasaba za mimea. Kwa hiyo, hili tutalifanyia kazi haraka na tutalileta hapa Bungeni na kwa kweli hii ni Kamati yetu ya Kilimo na Ardhi ambayo tunashirikiana nayo kubadilishana mawazo na ina watu makini sana katika suala la kilimo na usimamizi wa shughuli hizi zinazotuhusu. Tutalifanyia haraka sana na baadaye tutarudi kwenye Kamati ili tuweze kukubaliana.

Haya mengine yaliyozungumzwa, mengi tunakubaliana nayo ni ya kutekeleza tu kwa sababu ndivyo inavyotakiwa iwe katika Mkataba. Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, anasisitiza sana suala la maafisa ugani na utafiti kufanya kazi kwa pamoja ili kuweza kupata mashamba ya maonyesho yatakayowasaidia wakulima. Tuliliona hilo tatizo na tulikuwa tumetenganisha idara ya mafunzo na idara ya utafiti tukawa na idara mbili, tukagundua kwamba mafunzo hayafaidiki kutokana na utafiti vile vile utafiti haufaidiki kutumia wanafunzi walioko vyuoni. Ili kutoa ufumbuzi kwa tatizo hili Serikali imeshaamua kuunganisha hizi idara mbili kuwa na idara moja ya mafunzo na utafiti ili kuhakikisha kuwa vijana wanaopita katika vyuo wanakuwa wameshafanya kazi na watafiti na wanafahamu ni tafiti gani zilizofanyika wanazoweza kuchukua.

Hili la maafisa kilimo kushiriki katika kilimo kwa lengo la kwamba watakuwa na mashamba ya maonyesho nina wasiwasi nalo kidogo. Kwanza wakiwa na mashamba makubwa ya kutosha watatumia muda wao katika mashamba yao badala ya kwenda kwa wakulima. Lakini baadhi ya mashamba ya maafisa kilimo niliyoyaona si mazuri sana. Kuna mmoja tuligombana Kigoma kwa sababu tulikuta ana shamba bovu kabisa sasa ananieleza ni bovu kwa sababu ni mbali kutoka mjini na kadhalika. Nikamwambia hapana sasa tunaambizana uongo.

Mimi nafikiri maafisa kilimo tuwaandae vizuri ili waweze kushirikiana na wananchi kuchukua haya matokeo ya utafiti na kuyatumia katika mashamba ya wakulima. Tukiwataka walime mashamba makubwa basi tutapata hasara ya moja kwa moja. Lakini nia ya Mheshimiwa thomas Ngawaiya ni nzuri ungetaka hawa wawe na mashamba ambayo ndiyo bora kuliko mengine wakulima wakajifunze lakini lazima tuwe waangalifu sana. Vituo vyetu vyote vya utafiti vina mashamba makubwa ya mbegu, maana tumejaribu kuzalisha zile mbegu ambazo zimeshazalishwa humu nchini kwa wingi, kwa hiyo, ukienda Siliani na popote utakapokwenda utakuta mashamba makubwa. Lakini tahadhari ni kwamba kilimo cha mbegu zinazotokana na utafiti hakiwezi kuchanganywa na kilimo cha mazao mengine kwa sababu ukifanya hivyo utafanya lile analozungumzia Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, kwamba haya mazao yako mengine yanaweza yakaharibu ile mbegu unayotaka kuzalisha.

Kwa hiyo, unaweza kukuta shamba dogo sana la mbegu fulani tu kwa sababu ziko chache, lakini mashamba mengine makubwa zaidi pale ambapo mbegu zinapatikana kwa wingi. Suala la *Documentation Center* nimeshaeleza. Tuna *Documentation Center* pale *TPRI* naomba mkipitia Arusha, Kamati ya Kilimo na Ardhi ilikuwa Arusha na imetembelea *TPRI,* nina hakika wameona hiki kituo na ninyi ambao mtapita katika eneo lile niwashauri sana mwende mkaone nini kilichoko pale.

Pia Mheshimiwa Dr. James Alex Msekela, amezungumzia masuala mengi sana na mengine ametaka ufafanuzi. Kwa mfano, tunapozungumzia kuhifadhi maana yake ni nini na kuhimiza kilimo endelevu. Bahati nzuri haya masuala yamefafanuliwa katika Mkataba wenyewe. Kwa hiyo, ni kiasi tu cha kusoma kifungu cha sita kitaeleza ni nini ambacho kinamaanishwa kuwa kilimo endelevu. Hili la mimea ambayo imechukuliwa kuna mimea mingi sana imechukuliwa na mara nyingi sana vituo vya utafiti vinajua hiyo mimea ilipo. Kwa hiyo, tukishaingia katika Mkataba huu utatusaidia kuweza kujua ni mimea gani iliyochukuliwa kutoka Tanzania na iko katika nchi gani. Kwa hiyo, tutakubaliana na nchi hiyo, jinsi ya kufaidika wote kutokana na utaratibu huo. Lengo si lazima walipe labda fedha taslimu, inawezekana tutawekeana utaratibu ambao tutaufafanua katika sheria itakayotungwa hapa Bungeni kwa kutuwezesha kufaidika na shughuli hizo.

Hii sheria unasema si faida kuitunga kwa sababu ingeweza kutungwa hata bila kuwa na Mkataba, lakini ukiwa na Sheria ya Tanzania inayotawala mambo ambayo yanahusu Jumuiya ya Mataifa kwa ujumla ambayo hakuna Mkataba unaotusaidia kuhakikisha kwamba inatekelezeka itakuwa tunafanya kazi bure. Kwa hiyo, muhimu sasa ni kwamba tuna mkataba tayari, tutakachofanya ni kutunga sheria itakayotuwezesha kufaidika na Mkataba ule. Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, tumeshazungumzia yale aliyozungumzia, Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, nitakushukuru kama ukitupa maelezo kamilifu zaidi ili mimi na mwenzangu Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, tuweze kufuatilia huu utafiti uliofanyika na kama umefanyika humu nchini, nina hakika tutapata maelezo kamili juu yake. Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, nakushukuru sana kwa ufafanuzi na Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, naomba nirudie kukushukuru sana kwa yale uliyotuhimiza kwamba tulime muhogo kwa wingi kwa hizi mvua zinazonyesha.

Baada ya maelezo hayo mafupi sasa naomba kutoa hoja kwamba Mkataba wa Kimataifa wa Nasaba za Mimea kwa Ajili ya Kilimo na Chakula wa mwaka 2001, uitwao *The International Treaty on Plant Genetic Resources for Food and Agriculture, 2001* sasa uridhiwe na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwa)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Nasaba za Mimea kwa ajili ya Kilimo na Chakula liliridhiwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumefikia mwisho wa mjadala wa hoja hii. Mheshimiwa Waziri, utatoa hoja yako ya pili kipindi cha mchana kwa sasa hivi tuwaruhusu Wabunge wakapumzike.

Kwa kuwa kipindi cha mchana kitaongozwa na Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nitoe taarifa kabisa kuhusu *Order Paper* ya kesho. Kazi ya kesho ukichukulia kwamba hoja ya pili ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo itamalizika leo, kazi ya kesho itakuwa ni Muswada wa *Anti- Dumping* lakini alikwisha tuomba Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara kwamba angependa kwanza Waheshimiwa Wabunge, wapate nafasi ya kuelewa vizuri katika utaratibu wa Semina, ndiyo tulikuwa tumepanga siku ya Jumatatu tufanye semina hiyo, lakini ikaahirishwa kwa sababu nilizozieleza.

Sasa tumepanga kwamba kesho baada ya kipindi cha maswali, tutamruhusu Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, atufanyie semina ya jambo hilo tulielewe kwanza, halafu Muswada wenyewe tutakuja kuujadili kipindi cha mchana ili kusudi tujadili jambo ambalo tunalielewa vizuri.

Baada ya maelezo hayo sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni. *(Makofi)*

*(Saa 06.41 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kulinda Mimea na Mazao Uitwao *"The International Plant Protection Convention - IPPC, 1951"***

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kulinda Mimea na Mazao wa mwaka 1951 unaojulikana kwa Kiingereza kama: *The International Plant Protection Convention, 1951 (IPPC).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina jukumu la kulinda mimea na mazao ya Tanzania dhidi ya visumbufu na magonjwa yanayoweza kuenezwa kutoka sehemu moja hadi nyingine. Visumbufu na magonjwa ya mimea na mazao visipodhibitiwa vinaweza kulisababishia Taifa gharama na hasara kubwa sana. Kwa kuzingatia jukumu hili, mwaka 1997 Bunge hili Tukufu lilitunga Sheria ya Udhibiti wa Visumbufu vya Mimea na Mazao, Na.13 ya mwaka 1997, *uitwao The Plant Protection Act of 1997.*

Kabla ya sheria hiyo kutungwa, katika miaka ya themanini, wadudu waharibifu kama vile dumuzi, kidung'ata wa muhogo yaani *cassava mealy bug* na mnyauko wa kahawa, *tusarium coffee wilt disease* waliingia nchini na kulisababishia Taifa gharama za mamilioni ya fedha kuwadhibiti. Kwa mfano, udhibiti wa dumuzi peke yake uliigharimu Serikali zaidi ya Dola za Kimarekani milioni tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi za nchi moja moja za kuzuia visumbufu na magonjwa ya mimea na mazao haziwezi kufanikiwa bila juhudi za pamoja zilizo chini ya usimamizi wa vyombo vya Kimataifa kuhakikisha kila nchi inashiriki kikamilifu katika kudhibiti visumbufu na magonjwa, hayo ili yasisambae kutoka nchi moja hadi nchi nyingine. Umuhimu huu ulizilazimu nchi wanachama wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo yaani *FAO* kufikia makubaliano wa Mkataba wa Kimataifa wa Kulinda Mimea na Mazao, *The International Plant Protection Convention,* wa mwaka 1951. Mkataba huo uliongezewa umuhimu wake baada ya kutambuliwa na Mkataba wa Shirika la Biashara la Dunia yaani *World Trade Organization (WTO)* wa mwaka 1995 unaohusu afya ya binadamu, wanyama na mimea

uitwao *The Sanitary and Phytosanitary Agreement of 1995.* Tanzania ni mwanachama wa Shirika la Biashara la Dunia na hivyo tunalazimika kutekeleza Mkataba huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba wa Kimataifa wa Kulinda Mimea na Mazao uliidhinishwa na Mkutano wa Sita wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa mwezi wa Novemba, 1951 na ulianza kutumika tarehe 3 Aprili, 1952. Mkataba huo ulifanyiwa marekebisho mwaka 1979 ambayo yalianza kutumika mwaka 1991 na pia Mkataba huo ulifanyiwa marekebisho makubwa zaidi mwaka 1997 ili kuuoanishwa na Mkataba wa WT*O* ule niliosema unaitwa *The Sanitary and Phytosanitary Agreement.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Ibara ya nne ya Mkataba wa Kimataifa wa Kulinda Mimea na Mazao sharti muhimu la kukubaliwa kuwa mwanachama na hivyo kuridhia Mkataba huo ni kuwa na mfumo wa Taasisi wa Kudhibiti Visumbufu vya Mimea na Mazao katika nchi. Kwa upande wa Tanzania tayari tunao mfumo huo uliowekwa na Sheria ya Kudhibiti Visumbufu vya Mimea na Mazao, Sheria Na.13 ya mwaka 1997. Watekelezaji wa sheria hiyo ni kitengo kinachoshughulikia udhibiti wa visumbufu na magonjwa ya mimea na mazao kilichoko kwenye Wizara ya Kilimo na Chakula na Taasisi ya *Tropical Pesticide Research* iliyoko Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya tano ya Mkataba inazitaka nchi wanachana ziwe na utaratibu wa kukagua mimea nas mazao yanayotarajiwa kusafirishwa nje yua nchi zao na.....

*(Hapa Umeme Ulikatika)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** ....... kutoa Cheti au hati ya usafi na afya ya mimea na mazao hayo, yaani *Phytosanitary Certification.* Jukumu hili nalo limejumuishwa katika Sheria Na.13 ya mwaka 1997. Hivi sasa Tanzania inao Wakaguzi wa Mimea na Mazao wanaotekeleza jukumu hili na inao utaratibu wa utoaji wa vyeti vya afya na usafi wa mimea na mazao yanayosafirishwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara za sita na saba ya Mkataba zinazitaka nchi wanachama kuwa na utararatibu wa kuainisha visumbufu hatari ambavyo vinapaswa kudhibitiwa na sheria za nchi husika. Chini ya Ibara ya saba, nchi wanachama zimepewa mamlaka ya kuweka utaratibu wa kukagua, kuruhusu au kukataza mimea na mazao yanayoingia nchini mwao ili kuhakikisha kwamba hayana visumbufu hatari. Masharti yanayopaswa kuzingatiwa wakati wa utekelezaji wa utaratibu huo pia yamewekwa. Kwa mfano, kwa mujibu wa Ibara hii masharti ya ukaguzi au ukatazaji wa uingizaji wa mazao ndani ya nchi lazima yazingatie sababu za kisayansi, sio sababu za kisiasa kwa mfano. Aidha, nchi mwanachama inayoweka masharti hayo lazima itoe taarifa kwa nchi nyingine wanachama kuhusu masharti hayo.

Kanuni za kudhibiti visumbufu vya mimea na mazao za mwaka 1999 zilizotungwa chini ya Sheria Na.13 ya mwaka 1997 zimeweka utaratibu kama huu. Kwa hiyo, kwa upande wa Tanzania tumekwishatekeleza pia jukumu hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara za nane, tisa na kumi za Mkataba zinasisitiza umuhimu wa ushirikiano wa Kimataifa katika kudhibiti usambaaji wa visumbufu na magonjwa ya mimea na mazao kwa kutekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Kutoa taarifa za kuonekana kwa mlipuko wa visumbufu au kusambaa kwa visumbufu hivyo;

(ii) Kushirikiana katika kudhibiti visumbufu hivyo;

(iii) Kuanzisha ushirikiano wa Kimkoa *(Regional Plant Protection Organizations).* Kwa mfano, tuna Shirika la *DLCO (Desert Locust Control Organization)* la Afrika Mashariki na *Red Locust Control Organization la East, Central and Southern Africa,* ambayo tayari yanatumika kufanya kazi kama hizi.

(iv) Kuweka viwango vya Kimataifa vya afya na usafi wa mimea na mazao na kuhakikisha kwamba vinatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 11 hadi 16 za Mkataba zinahusu mambo ya kiutawala na kiutekelezaji. Chini ya Ibara ya 11 na 12, Kamisheni ya kusimamia utekelezaji wa Mkataba na Sekretarieti yake vinaanzishwa na kupewa majukumu haya ya usimamizi. Ibara ya 13 inaweka utaratibu wa kutatua migogoro kati ya nchi wanachama inayohusiana na tafsiri sahihi ya Mkataba. Aidha, ibara ya 14 inafuta Mikataba ya awali iliyokuwa inahusu udhibiti wa visumbufu na magonjwa ya mimea na mazao. Ibara ya 15 inaruhusu nchi wanachama kukubaliana na nchi zisizokuwa wanachama zenye uhusiano maalum na nchi inayohusika *(bilateral relationships)* kutumia Mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 17 Mkataba ulikuwa wazi kwa ajili ya kutiliwa saini hadi tarehe 01 Mei, 1952 na kwa mujibu wa Ibara ya 22 Mkataba ulianza kufanya kazi baada ya nchi ya tatu kuwasilisha nyaraka za kuuridhia. Mkataba sasa una jumla ya nchi wanachama 122 ambazo zimekwishauridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, uanachama katika Mkataba wa Kimataifa wa Kulinda Mimea na Mazao utaiwezesha Tanzania kupata manufaa yafuatayo:-

(i) Kukamilisha maandalizi ya utekelezaji wa Mkataba wa *Sanitary and Phytosanitary* ambao ni sehemu ya Mkataba wa Shirika la Biashara la Dunia *(WTO)*;

(ii) Kuruhusiwa kushiriki katika kuweka masharti na viwango vya biashara ya Kimataifa vya mazao na mimea. Chini ya Mkataba wa Biashara wa Shirika la Dunia, masharti na viwango vya mazao na mimea inayouzwa nje ni lazima yawekwe na Mkataba wa Kimataifa wa Kulinda Mimea na Mazao.

(iii) Kupata fursa ya kushirikiana na nchi wanachama katika kudhibiti magonjwa na visumbufu vya mimea na mazao.

(iv) Kupata misaada ya kitaalamu katika utekelezaji wa sheria ya kudhibiti visumbufu na magonjwa ya mimea na mazao.

(v) Kunufaika na miradi inayofadhiliwa chini ya Mkataba wa Kimataifa wa Kulinda Mimea na Mazao yenye lengo la kuongeza uwezo wa nchi wanachama katika nyanja za ukaguzi wa mazao na mimea;

(vi) Kupata taarifa mbalimbali bila gharama yoyote kuhusu kuwepo kwa visumbufu vya mimea katika maeneo mbalimbali ya dunia na jinsi ya kukabiliana navyo;

(vii) Kupata misaada ya usuluhishi na utaalamu katika migogoro ya kibiashara itokanayo na vikwazo visivyokuwa na misingi ya kisayansi vinavyowekwa na nchi mbalimbali; na mwisho

(viii) Kuweka mfumo unaotambulika Kimataifa wa kudhibiti kusambaa kwa visumbufu na magonjwa ya mimea na mazao unaowiana na kuongezeka kwa biashara ya mazao na mimea inayosafirishwa nje ya nchi au inayoingizwa kutoka nje kutokana na kupanuka kwa soko huria na utandawazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa Mkataba wa Kimataifa wa Kulinda Mimea na Mazao kwa Tanzania, Serikali inaliomba Bunge lako Tukufu likubali katika Mkutano wake huu wa Kumi na Nne kuridhia Mkataba huu chini ya ibara ya 63(3)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka wa 1977 na hivyo kuiruhusu Tanzania iwe mwanachama wa Mkataba huo kwa kupitisha Azimio lifuatalo:-

KWA KUWA juhudi za nchi moja moja za kuzuia magonjwa na visumbufu vya mimea na mazao haziwezi kufanikiwa kama hapatakuwepo na juhudi za pamoja zilizo chini ya usimamizi wa vyombo vya Kimataifa na kuhakikisha kwamba kila nchi inawajibika kudhibiti visumbufu hivyo kikamilifu ili visisambae kutoka nchi moja hadi nyingine;

NA KWA KUWA Mkataba wa Kimataifa wa kulinda Mimea na Mazao wa mwaka 1951, yaani *The International Plant Protection Convention of 1951* ni chombo cha Kimataifa cha kuhakikisha kuwa

nchi wanachama wanaweka utaratibu wa kudhibiti visumbufu vya mimea na mazao ili visiweze kusambaa katika nchi nyingine;

NA KWA KUWA Mkataba wa Shirika la Biashara la Dunia wa mwaka 1995 yaani *The Sanitary and Phytosanitary Agreement* ambao Tanzania ni mwanachama unalazimu kutumia viwango vilivyoko katika Mkataba wa Kimataifa wa Kulinda Mimea na Mazao katika kudhibiti visumbufu na magonjwa ya mimea na mazao;

NA KWA KUWA kujiunga na Mkataba wa Kimataifa wa Mulinda Mimea na Mazao utaiwezesha Tanzania kukamilisha maandalizi ya utekelezaji wa Mkataba wa *Sanitary and Phytosanitary Agreement;*

NA KWA KUWA kwa kujiunga na Mkataba wa Kimataifa wa Kulinda Mimea na Mazao Tanzania itapata manufaa ya kushiriki katika kuweka masharti ya viwango vya kufanya biashara ya Kimataifa ya mazao na mimea; kushirikiana na nchi wanachama kudhibiti magonjwa na visumbufu vya mimea na mazao; kupata misaada ya kitaalam katika utekelezaji wa sheria ya kulinda mimea na mazao; kufaidika na miradi inayofadhiliwa chini ya Mkataba huo yenye lengo la kuongeza uwezo wa nchi wanachama katika nyanja za ukaguzi wa mazao; kupata taarifa zinazohusu kuwepo kwa visumbufu na magonjwa ya mimea na jinsi ya kukabiliana navyo na kupata misaada ya kitaalam ya usuluhishi katika kukabiliana na migogoro ya Kimataifa ya biashara;

NA KWA KUWA Tanzania tayari ina sheria ya kudhibiti visumbufu na magonjwa ya mimea na mazao, Sheria Na.13 ya mwaka 1997 ambayo inakidhi masharti ya utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Kulinda Mimea na Mazao na inatumia sheria hiyo kuzuia kuenea kwa visumbufu vya mimea na mazao nchini, kudhibiti uingizaji nchini na usafirishaji nje ya nchi wa visumbufu na magonjwa ya mimea na mazao na kuhakikisha mikataba ya Kimataifa inatekelezwa;

KWA HIYO BASI, kwa kuzingatia umuhimu na faida ambayo Tanzania itapata kutokana na kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kulinda Mimea na Mazao, Bunge hili katika Mkutano wake wa Kumi na Nne kwa mujibu wa ibara ya 63(3)(a) ya mwaka 1977, sasa linaazimia kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kulinda Mimea na Mazao ya mwaka 1951, yaani *The International Plant Protection Convention, 1951.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Kuhusu mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa unaweza kukaa kwanza tusikilize kuhusu mwongozo.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** *Convention* tuliyopewa inaonesha kwenye ukurasa wa kwanza kwamba *not entered into force.* Mkataba wenyewe ni wa 1997. Sasa nilitaka kujua kama hii ndiyo *text* tunayotaka kuiridhia ama kuna *subsequent conventions* ama *texts* ambazo hii itakuwa imepitwa na wakati. Kama ndivyo hivyo, sioni umuhimu wa kuweza kujadil*i convention* ambayo imepitwa na wakati.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, anachohitaji Mheshimiwa Mbunge ni kuwa na uhakika ili anaporidhia afahamu kwamba huu ndio unao-*exist* sasa hivi au umepitwa na wakati au namna gani. Sasa hili linaweza kujibiwa tu na upande wa Serikali.

Mheshimiwa Waziri, anachotaka kuhakikishiwa ndio hii ambayo tumegawiwa?

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hii *convention* ndio iko *inforce.* Kama nilivyoeleza, Mkataba huu ulikuwa uwe *inforce* baada ya nchi ya tatu kuuridhia na nilieleza pia kwamba hadi wakati huu nchi 122 zimekwisharidhia Mkataba huu. Kwa hiyo, kile kiwango cha nchi tatu kilishapita miaka mingi sana iliyopita. Kwa hiyo, Mkataba uko *inforce.* Kilichotokea ambacho kimeleta hili tatizo ni kwamba tuli-*download* hii kutoka kwenye *internet* na hii *heading* ilikuwa haikufutwa ndio tatizo.

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, Mheshimiwa Mkono, Waziri anasema ni hii na anathibitisha hiyo uliyopewa ndiyo hiyo. Sasa *unless* una nyingine ambayo unaifikiria. Lakini hii uliyokabidhiwa ndiyo hiyo ambayo inatakiwa ijadiliwe na kupitishwa. Sasa baada ya hapo namwita Mheshimiwa Salama aweze kutoa mchango kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi. *(Makofi)*

**MHE. SALAMA KHAMIS ISLAM (k.n.y. MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa maoni ya Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi kuhusu Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kulinda Mimea na Mazao uitwao *The International Plant Protection Convention (IPPC).*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa niaba ya Wajumbe wote wa Kamati ya Kilimo na Ardhi kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni ya Kamati kuhusu Azimio la Mkataba wa Kimataifa wa Kulinda Mimea na Mazao wa mwaka 1951 uitwao *The International Plant Protection Convention (IPPC).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu uliipangia kazi ya kuchambua Azimio la Mkataba wa Kimataifa wa nasaba za mimea kwa ajili ya kilimo na chakula. Kwa mujibu wa kanuni ya 88(9) toleo la 2003, Kamati ilikutana Dodoma tarehe 11 Novemba, 2003 na kutekeleza jukumu hilo. Aidha, maoni ya Kamati kuhusu Azimio la Mkataba huu sasa nayatoa kwa mujibu wa kanuni ya 70(2). Kabla sijafanya hivyo, napenda kuwataja Wabunge ambao ni Wajumbe wa Kamati waliochambua na kutoa mchango mkubwa kuhusu Azimio la Mkataba huu. Wabunge wenyewe ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mwenyekiti; Mheshimiwa Alhaj Shawej Abdallah, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Anatory Choya, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Robert K. Mashala, Mheshimiwa Paul Makolo, Mheshimiwa Masoud Abdulla Salim, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Kidawa H. Saleh, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Mussa A. Lupatu, Mheshimiwa Dr. Suleiman J. Omar, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Edward Ndeka, Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Abdallahi O. Namkulala, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Mwadini A. Jecha, Mheshimiwa Philip A. Magani na mwisho ni mimi mwenyewe ambaye niko hapa mbele yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaunga mkono hoja ya Serikali ya kuleta Azimio na Mkataba huu unaolenga katika kuifanya Tanzania inufaike na juhudi za pamoja za Kimataifa za kulinda mimea na mazao yetu dhidi ya magonjwa na wadudu waharibifu wa mimea na mazao kutoka nchi za nje. Hata hivyo Kamati inaona kwamba Serikali imechelewa sana kuridhia Mkataba huu. Kamati inasisitiza umuhimu wa Serikali kujenga tabia ya kuhuisha *(update),* majukumu yake ya Kimataifa mara kwa mara kwa kuridhia Mikataba ya Kimataifa ambayo ina manufaa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono hoja, Kamati inapendekeza kutoa maoni mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Azimio la Mkataba huu. Kamati inakubaliana na Serikali kwamba kutokana na ukweli kwamba Tanzania kwa kujiunga na Mkataba wa Shirika la Biashara Duniani *WTO* wa *Sanitary and Phytosanitary Agreement* inalazimika kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kulinda Mimea na Mazao ambao ndio utaweka viwango vya mazao yetu yanayouzwa nje. Hata hivyo Kamati inahimiza Serikali kuhakikisha kwamba viwango hivyo vitakavyowekwa vinazingatia maslahi ya wakulima wa Tanzania.Aidha, wakulima waelimishwe kuhusu viwango hivyo ili waweze kunufaika na mfumo wa biashara huria. Kamati inaona pia kwamba kuna haja ya Serikali kutumia wasaa huu kuwaelimisha wakulima jinsi watakavyonufaika na mikataba ya kibiashara ya Kimataifa kama vile Mkataba wa *Sanitary and Phytosanitary Agreement,* sheria ya Marekani ya kuongeza biashara kati ya nchi za Afrika na Marekani, *AGOA* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati iliridhika kwamba kujiunga kwa Tanzania na Mkataba huu ni muhimu sana kwa maendeleo ya Kilimo chetu. Hata hivyo Kamati inahoji kwa nini Serikali imechukua muda wote huo wa miaka zaidi ya 50 kuridhia Mkataba huu. Maelezo yaliyotolewa na Serikali kuwa mkataba huu ulianza kufanya kazi wakati wa Ukoloni na kwamba Tanzania ilipaswa iridhie marekebisho yaliyofanywa kwa Mkataba huo mwaka 1979 ili kufufua uanachama wake lakini haikufanya hivyo kutokana na kutokuwepo na msukumo wa kufanya hivyo kwa wakati huo kwa kuwa kulikuwa na mfumo

wa uchumi hodhi, hayatoshelezi. Maoni ya Kamati ni kwamba hata wakati wa mfumo wa uchumi hodhi, Serikali ilipaswa kuona umuhimu wa kuridhia Mkataba huu unaolenga kulinda mazao na mimea yake dhidi ya magonjwa na wadudu waharibifu wa mimea kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kwamba Mkataba huu hauoneshi moja kwa moja kuhusika kwake katika kuhifadhi mazingira. Kamati inaona kwamba kuna umuhimu katika kutekeleza Mkataba huu hapa nchini wa kuweka mkazo wa kulinda mimea ya asili na mazingira ya nchi yetu dhidi ya mimea hatari inayoweza kuingia nchini kutoka nje na kuharibu mimea yetu ya asili na mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanya maandalizi ya kutosha ya humu ndani ya kutekeleza Mkataba huu kabla ya kuuridhia. Kwa mfano kuwa na sheria na Taasisi zinazohusika na kulinda mimea na mazao, *Sheria ya Plant Protection Act No.13* ya mwaka 1997. Hata hivyo Kamati inaona kwamba kuna haja ya kuifanyia uchambuzi upya sheria hiyo ili kuhakikisha kwamba inakwenda na wakati na inasimamiwa ipasavyo katika kutekeleza Mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla Kamati inaona kwamba kuridhia Mkataba huu kumechelewa sana na labda ndio maana Taifa letu limekuwa likikumbwa na uvamizi wa wadudu waharibifu kutoka nje kama wale waliotajwa na Waziri ambao ni dumuzi, kidung'ata wa mhogo na kadhalika. Kamati inaishauri Serikali isichelewe zaidi kuridhia Mkataba huu. Hata hivyo lazima ijiandae kuhakikisha kwamba wakulima wa Tanzania ambao wameendelea kuwa masikini pamoja na kuanzishwa kwa uchumi wa soko huria na utandawazi wananufaika ipasavyo na Mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maoni hayo, naomba nichukue fursa hii kwa niaba ya Wajumbe wote wa Kamati kumpongeza Waziri wa Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Charles N. Keenja (Mbunge), Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, kwa ushirikiano wao wakati Kamati inachambua Azimio la Mkataba huu. Pia nawashukuru wataalam wote kutoka Wizara hiyo kwa kuisaidia Kamati kutekeleza kazi hii kwa ufanisi. Aidha, naomba kwa namna ya pekee kuwashukuru Wabunge, Wajumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi kwa umakini wao wakati wa kuchambua Azimio la Mkataba huu ingawa walikuwa na muda mfupi wa kuupitia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nirudie kusema kwamba naunga mkono hoja ya Waziri wa Kilimo na Chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (Makofi)

**MHE. THOMAS NGAWAIYA - MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani natoa shukurani kwako wewe mwenyewe Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Waziri wa Kilimo na Chakula pamoja na Watendaji wa Idara ya *Plant Protection,* bila kuisahau Kamati ya Bunge ya Chakula na Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nipongeze hoja ya Kamati ya Kilimo na Ardhi kwa jinsi ilivyotolewa hapa mbele yetu kwani maoni tuliyotoa na mimi nilikuwa mmoja wa Kamati, kwa hiyo naipongeza Kamati. Vile vile nimpongeze Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa kuwa mwenzetu katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tunasema Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kulinda Mimea na Mazao uitwao *The International Plant Protection Convention (IPPC) of 1951.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Mkataba hakuna maelezo ya kumpa Mtendaji wa *Plant Protection* nguvu ya *search* na kukamata pindi anaposhuku kuwa kuna mazao ya mimea yanayoweza kuwa na pests. Vile vile haikuelezwa ni vipi fedha za *emergence* kama *exotic pest* akitokea katika nchi mwanachama itakuwaje katika kukabiliana nao, kwani kunahitajika hatua za haraka na hizo hatua zinahitaji mikakati ya fedha. Aidha, kwenye *importation* ya mimea na mazao ya mimea, wahusika wakuu ni watu wa *custom.* Hivyo ilitakiwa iwe wazi kuwa wanatakiwa kuripoti kwa Maafisa wa *Plant Protection* ili wafanye kazi yao ya ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kudhibiti visumbufu vya mimea na mazao ili visiweze kusambaa nchini ni kazi inayohitaji uadilifu mkubwa na Watendaji wake wawe wamekamilika. Kwa hali halisi ya Watendaji wetu wa Kitengo cha Udhibiti wa Visumbufu vya Mimea na Mazao, mishahara na marupurupu yao hairidhishi kiasi cha kukataa vishawishi kutoka kwa Makampuni au watu binafsi wanaotaka kuingiza mimea au mazao kwa mimea yenye visumbufu hapa nchini kwetu. Hali yao ya kimaslahi ni duni sana.

Kwa hiyo, namshauri Waziri aangalie masuala ya watumishi hao. Madhara na gharama ya kuyakabili matatizo hayo kwa upande wa Serikali huwa ni makubwa mno kwa kuzingatia umuhimu wa kilimo kwa nchi yetu. Kambi ya Upinzani inashauri, ili kuleta ulinganifu na kuondoa matatizo yanayoweza kujitokeza, Serikali iangalie upya motisha kwa Watendaji katika vitengo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 50 za wataalam wetu wapo katika nchi za *SADC* kwa maana ya nchi za Kusini, Botswana, Namibia, Zambia, Angola na kadhalika, kwa ajili ya kukosa huduma bora hapa nchini Tanzania na kule wanafanya kazi nzuri tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na matatizo mengi ambayo tunayo kwenye utendaji wa kudhibiti visumbufu vya mimea na mazao, matatizo makubwa yamegawanyika katika sehemu kuu nne ambazo ni kama ifuatavyo:-

*Institutional issues, documentation procedures, lack of good and clear documentation procedures and management system for surveillance pest listing, pest diagnostic etc., training and facilities and equipment.* Kuna ukosefu mkubwa wa hivyo nilivyotaja hapo vinakosekana katika Taasisi hiyo inayotakiwa kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengine ni kizuizi kwa kutofanikiwa kwa zoezi zima. Hakuna *pest list,* hivyo inabidi kuwe na *inventory for pest.* Njia ya kuingizia mazao haliko salama kwa sababu ya njia za panya. Mipaka yetu haiko salama sana hasa katika kuingiza mazao bila kufuata sheria hii tunayoridhia leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuna *Qualified Personnel Inspectors* mipakani kudhibiti uingizaji wa visumbufu vya mimea. *Plan Protection Act No. 1997* bado watu hawajui na inabidi iwe *published* itangazwe ili iweze kujulikana watu hawaijui labda watasikia leo tunaposema hapa Bungeni. Itangazwe kwa nguvu zote. Hatuwezi kufanya *pest risk analyze* kwa sababu zinazotokana na hoja ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema kama tunataka ushirikiano wetu kwenye mkataba uwe na manufaa kwa Taifa na wananchi wake hatuna budi kuimarisha maeneo niliyoainisha ili na sisi tusiwe watu wa kuletewa msaada wa taaluma na wataalam wakati kuna Watanzania wengi kwenye nyanja hiyo ambayo Serikali haijawa *serious* katika kuwatumia vyema na ndiyo maana wanahamia katika nchi zingine. Pia tuangalie yanayotokea humu ndani ya nchi yetu kama vile visumbufu kwenye zao la kahawa, kama nilivyokwisha eleza Waziri na kutoa taarifa iliyosainiwa na Wataalam huko Moshi na hadi leo Serikali haijachukua hatua yoyote.

Leo tunaridhia hoja hii ya 1951 na sijui ni kwa nini ilichelewa hivi. Labda ndiyo maana Serikali haikuchukua hatua yoyote kwenye visumbufu vya kahawa huko Moshi. Hivyo labda kwa kuridhia huu mkataba huenda tukapatiwa dawa ya kuondoa visumbufu hivyo kwenye kahawa yetu na kuondoa umaskini Kilimanjaro na kwingineko nchini. *(Makofi)*

Inaonekana Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria Na. 13 ya mwaka 1997 ya kuzuia visumbufu bado labda ilikuwa kwenye makabati, kwenye ma-*draw* sasa itolewe upya ili na sisi tuiangalie tena upyaili tulinganishe kwa sababu ni wengi ambao tumeisikia tu lakini hatujana nakala zake ili tuweze kujua inasema nini. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nitamwomba Mheshimiwa Waziri afanye bidii ili tupate hiyo nakala kwa sababu vingine vimefanywa *reference* kwenye hiyo Sheria ya 1997. Baada ya kusema hayo yote na kwa kuwa ilibidi tu-*review* Mkataba kwa kuwa ulianza kutumika 1952 na sisi tukachelewa mpaka leo, na sijui leo tumepeta msukumo gani. Lakini tutumie baraka hizo hizo kuamsha na vingine ambavyo vilikuwa

vimelala. Kwa hiyo, naomba kwa niaba ya Kambi, kuunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge Wasemaji Wakuu kwa hili wamemalizika mpaka hivi nilivyosimama sijapata mtu yoyote anayetaka kuchangia. Sasa namwita Naibu Waziri aliomba na yeye atoe mchango wake. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa na mimi nichangie suala hili lililopo mbele yetu. Nami naanza kwa kusema kuwa moja kwa moja naiunga hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

Nitachangia machache lakini mwenye kutoa hoja nyingi ni mwenye hoja ambaye ni Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula. Tanzania ni mwanachama aliyeshabikia suala la *transprotection* toka mwaka 1997. Kwa kupitisha Sheria ya *Transprotation* ya mwaka 1997 ambayo inashughulikia udhibiti wa visumbufu na magonjwa ya mimea na mazao tumeonyesha *concern* zetu kuhusu suala hili. Tangu mwaka 1997 Sheria hii ilipitishwa humu humu Bungeni, baadhi yetu tulikuwamo.

Tanzania imekuwa ikiimarisha shughuli za udhibiti kama ifuatavyo. Kwanza, mimea na mazao haingii wala haitoki bila idhini ya Wizara ya Kilimo na Chakula kwa zile shughuli za *Signal Factory Certification,* yaani *Signal Factory Certification,* lazima ziwe viwe vinakaguliwa kila kituo cha kuondokea, ukiondoa hiyo njia za panya ambazo hata sizijui idadi. Lakini vituo, viwanja vya ndege, vya mabasi, meli, kuna mtumishi wa Kilimo aliyesomea na kuhitimu rasmi yuko pale. Kwa hiyo, naomba niwaondoe wasiwasi kuwa Wizara ya Kilimo na Chakula ililala tangu mwaka 1951, imekuwa *alert* na tuna wataalam. Zinakotoka na kuingia na hata huo mchele juzi kama ulisikia uliingia mchele ulionekana una wasiwasi ingawa kulikuwa na mamlaka ya chakula kutoka Wizara ya Afya lakini mtumishi wa Kilimo alikuwepo kuchunguza. Kwa hivi naomba niwatoe wasiwasi juu ya suala hili. Vile vile ningependa kuzungumza kuwa Wakaguzi wa Kilimo wamo sio tu katika maeneo hayo kungojea *customs* hapana. Kama ni mmea *actually* iliruhusu chakula, wapo pale kabla ya *customs* na watu wa customs wanawafahamu. Naomba tena nitoe wasiwasi wa suala hili.

Tanzania ni mwanachama hai kwa mashirika ya kimataifa ya kudhibiti wadudu waharibifu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula alishataja hapa, *Basic Locust Control,* makao makuu yake yako Adis Ababa. Sisi ni wanachama. Halafu kuna *Red Locust Control Organization,* hawa nzige wekundi Makao Makuu yake yako Ndola Zambia, sisi wanachama hai. Vile vile haya mashirika yanashughulikia masuala yafuatayo:-

Kuna viwavi jeshi, vikitokea tu, unapeleka huko kwenye *Basic Locust* au nzige wa jangwani tunapata ndege ya kunyunyizia. Bila shaka baadhi yetu wameona hiyo. Na vile vile kuna kwelea kwelea wale ndege waharibifu na wanahusika na shirika hilo hilo na sisi wenyewe tukiwa na madawa. Halafu kuna mapanya waharibifu, *rodent* wapo. Tunashughulikia, kuna panzi kunuka, wapo sana katikati hapa na Singida na kwa taarifa kupitia mashirika hayo *FAO* wametoa taarifa kama mwaka huu Watanzania wawili kwenda kusomea *West Africa* jinsi ya kuwadhibiti panzi kunuka siyo kwa kumwagia kemikali. Kwa hiyo, inaonyesha wazi wazi tumekuwa *high* kweli kweli.

Halafu kuna *meal bug* ile ya mihogo aliyosema Mheshimiwa Waziri na shughuli zingine kama zile za huko Ziwa Victoria. Tanzania inanufaika na udhibiti huo kwani wanachama wetu katika mashirika ya Kimataifa inafanya tusiathirike na wadudu wasumbufu wa magonjwa wa mimea na mazao toka nchi jirani au za kimataifa. Hivyo basi kuridhia mkataba wa *International Plant Protection Convention (IPPC)* tunafaidika kwa mengi na tungekuwa tumefaidika kwa mengi tangu huko nyuma na baadhi ya mashirika haya kama *Red Locust, Desert Locust* yalianza hata kabla ya uhuru wakati wa kikoloni. Kwani tusione kama palikuwa watu na wamelala kabisa hawashughuliki na hili walikuwa wanashughulika. Sisi tunaendeleza kwa kulipia wanachama na vile vile kama Mheshimiwa Waziri alivyosema tunapata misaada ya mafunzo kwa wataalam wetu na wapo waliobobea kwa fani na kiongozi wa kitengo hicho ni *Assistant*

*Director of Crops* anaitwa Ndugu Nyakunga na vile vile ile taasisi ya Shirika la *High* ni wasomi waliobea katika masuala haya.

Kwa hiyo, tunaomba Waheshimiwa Wabunge msiwe na wasiwasi juu ya masuala haya. Tunaridhia lakini kazi imeshaanza huko nyuma. Kama wanachama Tanzania inaendelea na miradi mbalimbali ya kudhibiti wadudu waharibifu na magonjwa na mradi mmoja unaitwa *Integrated Pests Management (IPM)* kwa kupunguza kutumia madawa ya kemikali kwa kudhibiti visumbufu na magonjwa ya mazao kwa kutumia mbinu za kibaolojia kudhibiti wadudu hao. Kwa mfano, hii *cassava meal bug*, tulitumia manyigu kutoka *IPA Nigeria* katika mbinu hizo hizo tulizozizungumza. Halafu hivi karibuni kuna mbawa kavu tunadhibiti wadudu gugu maji katika Ziwa Victoria. Hiyo ni mchango mwingine wa Wizara ya Kilimo bila kutumia kemikali.

Kwa kutumia dawa za miti shamba au *herbs.* Mfano mwarobaini unavyoweza kuhifadhi mbegu za mahindi. Vile vile telefrosia kwa kudhibiti wadudu wa aina ya kupe kwenye mifugo na chuo chetu cha Uyole wameendelea sana kwa masuala haya kwa kutumia mbinu husishi na rafiki wa mazingira. Kwa hiyo, hapa hatutumii kemikali peke yake tunatumia hata madawa yale ambayo ni rafiki kwa mazingira kama nilivyoeleza. Kwa hivi ningependa tena kurudia kusema tusiwe na wasiwasi juu ya masuala ya kitengo hiki kinashughulikiwa vizuri na Wizara na tuna watumishi committed na naomba tuwapongeze sana kwa sababu wamefanya mengi hata kabla hatujapitisha sheria hii. *(Makofi)*

Napenda tena kuwapongeza huko waliko wasife moyo kuwa labda Bunge linafikiri hawajachangia, wamechangia sana katika kuzuia magonjwa mbalimbali kama nilivyokwisha eleza. Baada ya kusema hayo nashukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi kuzungumza na naunga mkono tena hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru tena kwa kunipa nafasi na niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii. Nilikuwa nimetegemea kuwa ingechangiwa na wengi zaidi kuliko walivyochangia. Lakini huenda ni kwa kuwa suala lenyewe ni suala linaloeleweka vizuri na kwa hiyo hawakuona sababu ya kuchangia kwa wingi. *(Makofi)*

Naomba nimshukuru sana Mwakilishi wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, Mheshimiwa Salama Khamis Islam, kwa mawasilisho yake hapa mazuri sana. Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yetu ni Kamati makini kweli kweli na huchambua haya mambo kwa undani kabisa kama ilivyoonekana hapa. Naomba nimshukuru pia Mheshimiwa Thomas Ngawaiya kwa yale aliyotoa. Kuna machache nitakayofafanua lakini namshukuru sana kwa kuiunga hoja mkono na kwa yale *positive* aliyoyasema. *(Makofi)*

Nimshukuru pia Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala kwa mchango wake. Ametukumbusha kuwa anajua mbawa kavu na wadudu wengine wanaotusumbua. Jambo moja ambalo limejitokeza hapa zito sana ni kwa nini Tanzania ilichelewa kuridhia Mkataba huu. Sasa ningeomba nitoe maelezo kwa ufupi kabisa, kama mtakavyokumbuka suala la kusimamia masuala haya ya uingiza wa mazao lilikuwa ni la jumuiya ya zamani ya Afrika Mashariki, hata Kituo cha *TPRI* kilikuwa ni moja ya Taasisi zilizokuwa chini ya Jumuiya ile.

Kwa hiyo, ile Jumuiya iliposambaratika mwaka 1977 tulipata matatizo ya kuanza kuanza kuandaa mazingira mapya ya kuchukua zile kazi ambazo zilikuwa zinafanyika. Na imefanyika kazi nzuri sana kwa sababu hadi kufikia sasa tuna sheria, tuna kanuni, tuna assasi na Taasisi ambazo zinashughulikia masuala haya. Na naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba kila mahali watakapokwenda watakutana na wataalam wa Wizara ya Kilimo wakidhibiti uingizaji na utoaji wa mimea kutoka Tanzania.

Leo asubuhi Mheshimiwa Ngawaiya alikiri mbele ya Bunge hili kwamba Wizara ya Kilimo ina wataalam wengi wasomi na ni kweli kabisa. Lakini mchana huu amesahau akasema hatuna competent staff. Nafikiri alighafirika tu kidogo. *(Makofi/Kicheko)*

Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kweli moja ya mambo ambayo tunaweza tunaweza kusema kwa uhakika kabisa ni Wizara iliyo na wasomi wengi sana waliobobea katika nyanja zinazowahusu na kwa hiyo katika eneo hili pia tuna wataalam waliosomea na kila wiki wanatoka nje kwenda kujifunza mbinu

mpya za kupambana na majukumu hayo. Lakini la pili, wale ambao wamesafiri kwa ndege kwa mfano kutoka Ulaya siku za karibuni, mkikaribia Tanzania wanawatangazia kabisa kwamba abiria wote muwe waangalifu msiwe na mimea katika *luggage* zenu kwa sababu mnaweza mkawa *searched* katika *port of entry,* jambo ambalo halikuwepo zamani. Zamani ulikuwa ukija watapulizia mbu lakini hawatazungumzia mambo ya mimea. Siku hizi wanakuonya tangu ukiwa angani kwamba kama umebeba mimea muwe tayari kui-*declare.*

Mwezi Novemba nilitoka Italy ambako nilipata sample ya mbegu ya mtama, ilibidi niiache uwanja wa ndege, wakaenda kuchukua wataalam wakaipeleka ili waende wakaioteshe na kudhibiti kuhakikisha kwamba ile mbegu haikuwa na visumbufu vya mimea. Kwa hiyo, tumeanza kuwa *very serious* na suala hili na pamoja na mishahara midogo. Lakini jamani mnafahamu Wabunge mnatakiwa wakati mwingine tujipongeze hapa. Mnafahamu katika hii miaka mitatu iliyopita Bunge hili limeidhinisha pesa nyingi sana za kuongeza maslahi ya watumishi. *(Makofi)*

Na kwa niaba yao naomba niwashukuru sana sana sana, watumishi wetu sasa hali zao ni nzuri, hatujafikia kiwango cha juu kabisa. Ni nzuri sana kuliko zilivyowahi kuwa wakati wowote. Na nalishukuru sana Bunge hili na Waheshimiwa Wabunge kwa sababu mmekuwa mnauliza maswali hapa na kuhakikisha kwamba mnafuatilia kwa karibu sana uboreshaji wa maslahi ya watumishi wa kilimo.

Mheshimiwa Ngawaiya, maslahi haya yamekuwa yakiboreka kila wakati. Lakini sina maana ya kusema vishawishi vitakuwa vimekwisha. Maana hata matajiri hushawishiwa na wakashawishika. Kwa hiyo, tutaendelea kusimamiana kwa taratibu zilizowekwa lakini nina hakika kwamba tunakwenda vizuri kabisa. Sasa uingizaji wa mimea katika nchi hauwezekani kabisa. Kama mtu akitaka kuagiza mahindi kutoka Afrika ya Kusini agizo la kwanza analopewa ni kwamba ni lazima alete *pytosanitary certificate* kutoka Afrika ya Kusini kuonyesha kwamba mahindi hayo hayana wadudu.

Lakini njia za panya zipo na tunajua zipo. Wakati mwingine unakuta punda kabeba gunia wala hana mtu anayemfuata. Sasa ukimwuliza *pytosanitary certificate* utapata matatizo kidogo. Lakini kwa ushirikiano kati ya nchi zetu, tutafika mahali ambapo kila nchi itakuwa inasimamia kwa ukamilifu hivi visumbufu vya mimea na mazao ili kuhakikisha kwamba hakutakuwepo wadudu wengi wa kuingia nchini. *(Kicheko)*

Nakubaliana na Mheshimiwa Ngawaiya kwamba ni kweli alizungumzia juu ya visumbufu vya kahawa na nataka nimhakikishie kwamba TACRI wanashughulikia tatizo hilo tayari. Lakini ni vizuri zaidi ukawa unatazama masuala haya kitaifa maana wewe ni mwakilishi wa Upinzani Kitaifa ili kuhakikisha kwamba unaona na vile visumbufu vingine vya muhogo vilivyoko Kagera na Kigoma na kwingineko, lakini nakushukuru sana kwa mchango huu mkubwa.

Naomba vile vile niwahakikishie, Mheshimiwa Islam na Mheshimiwa Ngawaiya kwamba tutachukua, mara mkisha kubali kuridhia Mkataba huu, tutachukua hatua za haraka sana kuhakikisha kwamba tunafanya hivyo, kwa sababu tungetaka tujiunge na jumuiya ya Kimataifa kudhibiti uingizaji wa magonjwa humu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tukubaliane. Unafahamu vyakula vyetu vingi sana vinakwenda nchi za jirani, vingi sana. Unapokuwa na upungufu na wao wakawa na unafuu si una haki na wewe ukapata kidogo kutoka kwao? Lakini wataalam wetu wakasimamia na nataka kukuhakikishia kwamba tuna vituo 27 vya kusimamia. Kwa hiyo, tumeruhusu kwamba mtu yoyote anayetaka kuingiza chakula nchini aingize kupitia katika Vituo hivi hamna kodi, hamna jambo lolote atakalofanyiwa, isipokuwa tu kukagua kuhakikisha kwamba vinakidhi mahitaji haya kama ilivyoelezwa. Kwa hiyo, kama kuna mtu yoyote ambaye ana chakula Kenya, Uganda sijui wapi anataka kuingiza huku nchini, apitie tu njia za kawaida, asiende kwenye vichochoro kwa sababu hakuna kodi wala hakuna kitu chochote kitakachomzuia kuingia na ukaguzi utafanyika haraka inavyowezekana na kumruhusu aingize chakula hicho nchini. *(Makofi)*

Alizungumzia vile vile kwamba matatizo yetu ni manne, tunakosa *institutional frame work.* Hii nimesema hapana, si kweli. Tuna *institution* za kusimamia hii, kuna sehemu maalum kwenye Wizara

inayosimamia. Mheshimiwa Naibu Waziri amekueleza na Mkuu wa sehemu hiyo na *TPRI* ni moja ya *organizations* ambayo kazi yake kubwa ni hii. Tuna watumishi karibu kwenye mipaka yote na *port* zote za *entry,* viwanda vya ndege, bandari na kila mahali. Kwa hiyo, *institution* ipo.

*Funding* na pengine inawezekana siyo ya kutosha sana, tungepata pesa zaidi tungefanya zaidi. Lakini kadri ya mapato ya Serikali yanavyoongezeka, mmeona nyinyi wenyewe, tunaongeza fedha kwa ajili ya kugharamia shughuli mbalimbali zinazofanyika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nafikiri tunakwenda vizuri. *Tranning* ndiyo, hii nimeshasema kwamba watumishi wa Kilimo ni watumishi waliosomeshwa sana na mpaka leo wanaendelea kwenda kwenye mafunzo mbalimbali juu ya njia bora zaidi za kushughulikia haya masuala na *documentation,* nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Ngawaiya kwamba *documentation* ipo na tuna orodha kabisa ya visumbufu vikuu ambavyo vinatutatiza na vimetajwa katika zile Kanuni za mwaka 1999. Kwa hiyo, kwa kweli kama ni maandalizi tu nafikiri tumejiandaa vizuri kupambana na matatizo haya yanayotupata.

Sasa wataalam wetu je, wana *powers* za kukagua hiyo. *Yes* wana powers. Wana power chini ya Sheria yetu. Chini ya Sheria Na. 13 ya mwaka 1997, wanaweza wakakagua mazingira yoyote wakati wowote ambao ni wakati muafaka. Sio waje wakakukague saa 9 za asubuhi, wakati unaota njozi za kukaribia kupambazuka. Kwa hiyo, wana uwezo wa kukagua na wana uwezo wa ku-*confiscate* mimea yoyote au mbegu zozote ambazo mtu atakuwa nazo, ambazo atahisi kwamba huenda zinaweza zikatuingizia magonjwa. Kwa hiyo, hizo *powers* wanazo na wala hawana tatizo kabisa.

Lakini tunaomba watu wanaotaka kuingiza mimea nchini lazima wapate hati hizo zinazotakiwa huko huko wanakoleta hiyo mimea kabla ya kuingiza huku nchini na tukiwa na matatizo na mimea hiyo, itanyang'anywa na kwenda kuwekwa mpaka turidhike kwamba hiyo mimea hatuingizii wagonjwa.

Sina hakika kama Mheshimiwa Ngawaiya kama nusu ya wasomi wote wa Tanzania wako nchi za *SADC.* Ingekuwa hivyo, ingekuwa hali ya hatari kweli kweli. Tangu tupate uhuru tumesomesha sana. Hawa walioko huko sidhani kama watafika hata *one percent* ya watumishi tuliosomesha. Lakini wanakwenda huko wakifikiri *the pastures are greener* kuliko zilivyo hapa. Lakini watu wanaanza kutambua kwamba nyumbani mazingira sasa hivi ni mazuri na wanaanza kurudi kufanya kazi hapa hapa.

Haya mengine nimekwishajibu. Hii Sheria itangazwe, tutaangalia nini tufanye kwa kweli ili Sheria iweze kujulikana. Tatizo letu kubwa sana la Sheria ni kwamba tukishazipitisha hapa Bungeni mara nyingi sana hazitafsiriwi katika Kiswahili na kuwekewa utaratibu wa kuzisambaza. Lakini kuna Sheria ambazo zinagusa maisha ya wananchi. Ni vizuri zikawekewa utaratibu wa kuzitangaza ili zieleweke vizuri. Nakubaliana na Mheshimiwa Islam, nakubaliana na Mheshimiwa Ngawaiya juu ya tatizo hili.

Waheshimiwa Wabunge, tumeshachelewa kuridhia huu Mkataba. Ninachoomba sasa kwa dhati kabisa mruhusu uridhiwe. Sasa naomba kutoa hoja ya kwamba Mkataba wa Kimataifa wa Kulinda Mimea na Mazao uitwao *The International Plant Protection Convention* kwa kifupi *IPPC* wa mwaka 1951 sasa uridhiwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kulinda Mimea na Mazao liliridhiwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Azimio limetolewa na limeungwa mkono, wote wameafiki. Azimio hilo limepitishwa rasmi na Bunge hili. *(Makofi)*

Sasa baada ya kufika hapo hatuna shughuli nyingine kwa jioni hii. Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 11.58 Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi tarehe 5 Februari, 2004 Saa Tatu Asubuhi)*